**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao Cha Kumi Na Sita – Tarehe 5 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samueli J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni Kuhusu Makadirioo ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Mbunge atakayeuliza swali la kwanza nina matangazo kuhusu wageni kama ifuatavyo:-

Kwenye *Gallery* upande wa kushoto yupo mgeni wa Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, ambaye ni Ndugu Francis Kombe, Meneja wa *Mbinga Coffee Company*. Ahsante sana.

Mheshimiwa Anna Lupembe ana wageni wake kutoka Mpanda, Mzee Maraki, pamoja na mkewe. Wale pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

Huyu Mheshimiwa hakujitaja lakini anasema kuna wageni wanaotoka *Social Action Trust Fund,* wakiongozwa na Mama Beatrice Mgaya, ambaye ni *Branch Manager.* Taasisi hii inatoa mikopo kwa wafanya biashara na faida inayopatikana inasaidia watoto yatima waliopo katika Mazingira Magumu. *(Makofi)*

Mama Beatrice Mgaya, yuko wapi sijui. Ni upande ule. Kulingana na maelezo haya Waheshimiwa Wabunge huyu mama ni vizuri sana kumfahamu. Kwa sababu kuna mikopo hapa. Baada ya hayo sasa namwita Mheshimiwa Mpina swali la kwanza. *(Makofi)*

Na. 147

**Matatizo katika Kituo cha Afya Mwandoya**

**MHE. JOYCE M. MASUNGA (K.n.y. LUHANGA J. MPINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya Mwandoya kilijengwa siku nyingi na ndicho tegemeo pekee kwa wananchi wa Kisesa lakini kina matatizo mengi likiwemo la ukosefu wa huduma ya kuongeza damu na ukosefu wa *ambulance.*

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka *ambulance* kuokoa maisha ya wanawake wajawazito na watoto na wagonjwa wengine kuwapeleka hospitali ya Wilaya zaidi ya kilometa sita (6)?
(b) Je, ni lini Serikali itaongeza waganga wa taaluma mbalimbali kwani sasa kuna *Clinical Officer* tu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha Kituo hicho ili kiweze pia kutoa huduma ya kuongezea wagonjwa damu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mpina, Mbunge wa Kisesa, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kituo cha Afya cha Mwandoya kilijengwa mwaka 1974 na kilianza rasmi kutoa huduma mwaka 1976.

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali langu Na. 17 la Mheshimiwa Damasi Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, tarehe 29 Machi, 2006 na swali Na. 138 la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, la tarehe 4 Julai, 2006 nililieleza Bunge lako Tukufu

kwamba, Serikali imeshaona tatizo la magari ya kubebea wagonjwa katika vituo vya Afya. Na katika tathmini yake imeonekana kwamba mahitaji halisi ni magari 300. Hivyo katika mwaka wa fedha 2005/2006 Ofisi yangu imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua magari ya kubebea wagonjwa na magari hayo yameshanunuliwa. Pia katika mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi yangu imeendelea kutenga fedha shilingi bilioni 1.8 ili kuendelea kununua magari ya kubebea wagonjwa na kuendelea kuyasambaza katika Halmashauri mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Afya, Ikama katika kituo cha Afya ni watumishi 37 wa kada mbalimbali. Idadi ya watumishi waliopo katika kituo cha Afya Mwandoya ni 14 kwa hiyo kuna upungufu wa watumishi 24, ikiwa ni pamoja na upungufu wa Daktari Msaidizi mmoja na Afisa Tabibu wawili.Aidha, tatizo la upungufu wa watumishi wa Afya ni la nchi zima na Serikali imeanza kulitafutia ufumbuzi. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 wataalam wa Afya wataajiriwa moja kwa moja kutoka Vyuoni kwa wale watakaohitimu bila kufanya usaili. Hivyo, tunategemea utaratibu huu, utapunguza matatizo ya watumishi wa Afya nchini ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya cha Mwandoya.

(c) Mheshimiwa Spika, kupitia mradi wa ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za Afya nchini Serikali itaboresha vituo vyote vya Afya nchini ikiwa ni pamoja na kituo cha Afya Mwandoya ili kiweze kutoa huduma ya kuongezea wagonjwa damu na ukarabati huu unafanyika kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imeanzisha mpango wa kuwa na Benki ya damu kikanda, kwa sasa benki hizo zimeanzishwa katika maeneo ya Kanda ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya. Pamoja na kuanzisha mpango huo Serikali imeweka vipimo maalum vya kuchunguza mambo yote muhimu kwa ajili ya usalama wa binadamu wakati wa kutoa damu. Kuwepo kwa vituo hivi kutasaidia Meatu kupata damu pale inapobidi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana wa Waganga, *Clinical Officers* na kwa kuwa kuna vyuo ambavyo vilikuwa vinafundisha Maafisa Afya Wasaidizi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba vile vyuo ambavyo vilikuwa vinafundisha Maafisa Afya Wasaidizi, kama vile Kagemu, Ngudu, Mpanda viweze kuchukua Waganga ili kuwafundisha tupate waganga wengi na kupeleka katika Vituo vya Afya?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika kujaribu kutatua matatizo ya uhaba wa wafanya kazi sasa hivi tuko katika zoezi la kuvipitia vituo vyote vilivyopo ili tuviangalie kwa maana ya kutaka kuvikarabati na kutazama uwezo wake na pia walimu na kuongezea vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Halafu vile vile tunaangalia vituo ambavyo vimefungwa ikiwa ni pamoja na alivyotaja na kingine Nachingwea katika zoezi zima la kujaribu kuongeza ikama na usaili wa vijana wetu *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa TAMISEMI, nina swali dogo la nyongeza hasa linalohusiana na suala la *ambulance* tatizo lililozungumziwa Kisesa linafanana na Jimbo langu la Iramba Magharibi, ila sasa linafanana kwa namna tofauti katika Tarafa ya Shelui, Kituo cha Afya cha Mgongo na Tarafa ya Ndato, halafu Tarafa ya Kinyangiri. *(Makofi)*

Hivi vina magari na magari haya yapo ya wagonjwa yapo makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya. Lakini magari haya yameshindwa kupelekwa vituoni kwa maelezo kwamba kinangojewa kibali kutoka TAMISEMI. Sasa nauliza hii kauli ina ukweli kiasi gani na kama ina ukweli ni lini TAMISEMI itatoa kibali ili magari hayo yaende kwenye vituo vya afya?

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inachofanya ni kupeleka magari kwenye Halmashauri ambazo kwa vigezo tunaona ina sahihi kupewa gari au magari. Suala la gari liende Tarafa ipi ili kuwahudumia wananchi wa eneo hilo ni suala la Halmashauri yenyewe na kamwe hatujaweka masharti yoyote kwenye magari haya. Nadhani nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kupitia kauli hii Bungeni kwamba waamue wapi wanaona gari likae kwa sasa. *(Makofi)*

Na. 148

**Hospitali ya Wilaya ya Morogoro Mjini**

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa jimbo la Morogoro Mjini wapato 228,863 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 wanayo matatizo makubwa ya kupata matibabu ya kufaa na ya haraka wanapougua kwa vile Manispaa ya Morogoro haina Hospitali ya Wilaya na kuwa, Mji wa Morogoro ni njia panda ya barabara ziendazo Mikoa mbalimbali na pindi kunapotokea ajali majeruhi hupelekwa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Manispaa ya Morogoro inapatiwa Hospitali ya Wilaya ili wananchi hao waweze kupata huduma za afya kwa wakati muafaka?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba, Kituo cha Afya cha Sabasaba ambacho kipo katikati ya Manispaa kinaweza kuboreshwa ili kiwe Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Nibuka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji wa Morogoro ni njia panda ya barabara ziendazo mikoa mbalimbali na pindi zitokeapo ajali majeruhi hupelekwa katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Kwa kulitambua hilo mwezi Septemba 2004 Serikali ilikabidhi kituo cha Sabasaba kilichopo Morogoro Mjini kwa Manispaa ya Morogoro na hospitali ya Mazimbu kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Aidha, ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya Mkoa Manispaa ya Morogoro imeandaa mipango ya kukikarabati na kukipanua Kituo hicho ili hatimaye kiwe na hadhi ya Hospitali ya Wilaya.

(b) Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo cha Afya Sabasaba kinaweza kuboreshwa na kuwa hospitali ya Wilaya itakayotoa huduma bora kwa wagonjwa katika Manispaa ya Morogoro. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imetenga jumla ya sh.28,000,000/= na mwaka 2006/2007 zimetengwa jumla ya sh. 26,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza ukarabati na upanuzi wa kituo cha afya hicho. Hata hivyo Serikali pia kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa katika fedha za ukarabati wa vituo vya afya na zahanati, kwa mwaka huu 2006/2007 imetenga jumla ya shilingi milioni 113 kwa ajili hiyo. Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuishauri Manispaa ya Morogoro kutumia fedha hizo kwa ajili ya upanuzi wa kituo hicho cha afya ili kiwe na hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya kupunguza msongamano katika hospitali ya Mkoa wa Morogoro.

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Napenda pia nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye matumaini makubwa. Lakini kuboresha kituo cha afya kuwa hospitali ya Wilaya kinahitaji pesa nyingi za kutosha na kwa maelekezo yake ni kwamba pesa alizotaja zingeweza kuboresha kituo hiki iwe hospitali ya Wilaya, anaweza kuwahakikishia wananchi wa Morogoro kwamba Serikali itaongeza pesa za kutosha ili shughuli hizi ziweze kufanikiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ili kile kituo cha afya cha Sabasaba kiweze kukamilika na kuwa hospitali ya Wilaya zinahitaji shilingi milioni 800. Kama nilivyosema kwenye jibu langu msingi kwamba Serikali imejitahidi kutoa hizo shilingi 113 na Halmashauri pia inashauriwa kuongeza kiasi ili hiyo hospitali iweze kukarabatiwa na kupanuliwa kwa awamu mpaka hapo itakapofikia kuwa hospitali kamili ya Wilaya. *(Makofi)*

Na. 149

**Matumizi ya Maji Kiwanda cha Mtibwa**

**MHE. MAGDALENA SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya jukumu la Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata maji safi na salama na kwa kuwa kiwanda cha Sukari cha Mtibwa kilichopo Morogoro kwa muda mrefu kimekuwa kikilalamikiwa kumwaga maji machafu kwenye mto Wami na hivyo kusababisha adha kubwa kwa wananchi na wanyama wanaotegemea mto huo, ikiwa ni pamoja na kukosa maji safi ya kunywa, kuathirika kwa mazao mashambani na viumbe vilivyo ndani ya mto huo:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa kiwanda hicho ili kuondoa tatizo hilo kwa wananchi?

(b) Je, Serikali imeandaa mikakati gani ya kupambana na matatizo kama hayo ambayo yapo pia kwa viwanda vingine vilivyojengwa jirani na makazi ya watu?

(c) Je, kwa kuwa kiwanda hiki kimejengwa jirani sana na vyanzo vya maji na kinatumia maji mengi sana kuendesha shughuli zake kila siku. Je, kiwanda hiki kinashirikishwaje katika kuhifadhi vyanzo hivyo vya maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-
(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilituma wataalamu kuchunguza chanzo cha uchafuzi ili kuona jinsi kiwanda kinavyomwaga maji machafu kwenye mto Wami na mazingira yanaoharibiwa kwa ujumla. Baada ya wataalam kuona kasoro zilizo kuwepo, Wizara yangu iliuagiza uongozi wa Kiwanda kurekebisha kasoro hizo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kiwanda kilitekeleza mapendekezo yaliyotolewa na wataalam kama ifuatavyo:-

(i) Kutoruhusu maji machafu kumwagwa moja kwa moja mtoni.

(ii) Kutenganisha mifumo ya maji taka na ile ya maji ya mvua.

(iii) Kukarabati mabwawa ya maji machafu kuongeza kina cha tuta.

(iv) Kuchimba visima virefu vinne katika eneo hilo ili kubaini kama uchafuzi juu ya ardhi umeathiri rasilimali za maji chini ya ardhi. Ukaguzi uliofanyika tarehe 21/3/2006 ulionyesha kuwa viwango vya usafi wa majitaka vinavyotakiwa kimataifa *(WHO)* na kitaifa vimefikiwa. Bado Wizara inaendelea kusaidiana na Kiwanda kuboresha mfumo wake wa majitaka. Katika jitihada za kuhakikisha kuwa kiwanda kinatekeleza mapendekezo ya wataalam, mnamo tarehe 4 Juni, 2006 Naibu Waziri alifanya ziara kwenye kiwanda hicho na kubaini kuwa bado mitaro na kuta za mabwawa ya majitaka inahitaji kukarabatiwa. Hivyo, aliagiza ukarabati huo ukamilishwe Septemba 2006 pamoja na uchunguzi wa madhara ya majitaka kutoka Kiwandani kwa wananchi na mifugo ya kijiji jirani cha Lukenge ili tuweze kuona jinsi tunavyoweza kukabiliana na tatizo hilo kikamilifu

.(b) Mheshimiwa Spika, ili kulinda vyanzo vya maji nchini visiathiriwe na uchafuzi kutoka viwandani, Wizara yangu imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuanzisha Ofisi za Mabonde 9 ili kuweka usimamizi wa karibu na wenye ufanisi zaidi. Aidha, viwanda vyote hukaguliwa mara kwa mara ili kubaini mwenendo wa viashiria vya uchafuzi kulingana na sheria ya maji.

(ii) Kurekebisha sheria ya Maji kwa kuiongeza adhabu kwa wachafuzi wa vyanzo vya maji mara kwa mara ili kuhakikisha vyanzo vinalindwa.

(iii) Kuanzisha mpango maalum wa kukagua viwanda vyote nchini ili kuhakikisha kuwa kila kiwanda kinakuwa na mtambo wa kusafisha majitaka kabla ya kuyamwaga.

(iv) Miradi yote mipya, kunatakiwa kwa mujibu wa sheria kufanya tathmini ya athari za mazingira *(Environmental Impact Assessment)* na kutekeleza mpango/mkakati wa kudhibti athari za miradi hiyo katika mazingira na jamii inayozunguka eneo husika.

(c) Mheshimiwa Spika, katika ushirikishwaji wa Kiwanda cha Mtibwa katika kuhifadhi vyanzo vya maji ni kwamba pamoja na kiwanda kuzingatia masharti ya Hati ya kutumia maji, bado kimeshauriwa kutumia mbiunu za kisasa za umwagiliaji ili kupunguza matumizi makubwa ya maji. Aidha, Wizara imekiagiza Kiwanda hicho kupanda miti na kuboresha mazingira yake ili kuhifadhi vyanzo vya maji vilivyopo pamoja na hatua nyingine zilizotajwa hapo juu. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa suala la Mtibwa ni la muda mrefu na matatizo yaliyotokea maeneo ya Mtibwa ni ya muda mrefu na hii inadhihirisha wazi kuwa kiwanda cha Mtibwa kuendelea kusambaza maji ya kunywa kwa kijiji jirani cha pekee cha Lukenge na kusahau kwamba maji ya Wami yanatumika katika maeneo mengi yakiwepo ya Morogoro na Bagamoyo.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutoa wataalam wake wachunguze tatizo hili kwa makini ili kuweza kunusuru maisha ya wananchi badala ya kungoja athari zitokee ndipo hatua zichukuliwe?

Pili, kwa kuwa mto huu unapita katikati ya eneo la hifadhi ya jamii la *Wami Management Area* ambalo limetengwa na wananchi kwa muda mrefu kwa juhudi zao na mara kwa mara kila mwaka viumbe wa majini wakiwemo samaki hufa na kuelea lakini kila wanapokilalamikia kiwanda kimekuwa hakichukui hatua. Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kuathirika kwa hifadhi hii ni kukatisha tamaa wananchi ambao wanahifadhi maliasili kwa ajili ya manufaa na maendeleo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu athari za maji. Mimi nilikuwa ni mmojawapo niliyekwenda kutembelea kiwanda hicho na kwa kweli nilishuhudia mwenyewe jinsi ambavyo kiwanda kimetenga mifereji. Kuna mifereji ya aina mbili, kuna mifereji ya majitaka ambayo yamekwenda moja kwa moja kutibiwa katika mabwawa 6. Na kuna mfereji wa maji ya mvua. Na kwa hali hiyo mimi nilithibitisha kwamba athari zozote kwa wakati huu kwa kweli ni ndogo. Lakini hata hivyo, tulikubaliana ya kwamba Kiwanda cha Mtibwa washirikiane na wataalam wetu kwenye maabara za maji ili kuhakikisha kwamba majitaka yanayotibiwa ni salama yakiingia kwenye mito. kuhusu maji kwamba bado baadhi ya viumbe kama samaki vinaathirika humo na pia maji haya yanakwenda mpaka sehemu mbalimbali ambazo watu wanatumia. Wakati nilipokwenda nilichukua uongozi wa Mtibwa nikaenda nao mpaka kijiji cha Lukenge kwenda kufanya mashauri, kutathmini athari zilizotokea. Athari hizo tulipotathmini tuliona ng'ombe walikufa na baadhi ya samaki walikufa pia na mimea ilikauka.

Lakini hata hivyo, Menejimenti ya Mtibwa ilikubaliana kulipa fidia kufuatana kila mwananchi alivyoamua kiasi gani kapoteza na jumla ya fidia ilipopigwa hesabu ilikuwa milioni 19 na majina ya wananchi wote yaliorodheshwa na sasa Kiwanda cha Mtibwa kiko kuwafidia wale wananchi mbalimbali. Lakini hapo hapo lilitokea suala lingine la kuhusu kwamba hawa samaki wanawezaje wakafa na mimea ikakauka.

Meneja wa Mtibwa aliweza kuulizia na akasema kwamba yeye ana wasi wasi kwamba kuna chanzo kingine au sumu nyingine inayoua viumbe hawa kwa sababu samaki pale watu wanakula na hawaathiriki na pia ng'ombe wanakunywa yale maji hawaathiriki. Basi wakaulizwa wananchi wa Kijiji cha Lukenge kwamba je, mnapovua mnatumia kitu gani?

Wananchi walijibu wakasema kwamba ili wapate samaki wengi wanatumia dawa inayoitwa *Thiodan* ambayo ni sumu. Kwa hiyo, hapo hapo wananchi mbele ya mimi kama shahidi walikubali kwamba wenzao wanapovua wanatumia *thiodan* sasa hapa ikajulikana kwamba pia *thiodan* ni sumu huenda yale maji yakiingia *thiodan* na yenyewe ni chanzo nyingine cha kuua viumbe.Basi tukakubaliana ya kwamba uchunguzi huo sasa ufanywe na maji yaangaliwe upya. Tuone kama ile sumu ya *thiodan* ipo na wananchi pale mbele ya Serikali yao ya Kijiji walionywa kwamba wasitumie tena *thiodan* katika kuvua samaki. *(Makofi)*

Na. 150

**Uchimbaji wa Visima vya Maji**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa upo uharibifu mkubwa wa mazingirsa juu na chini ya ardhi na kwa kuwa, wananchi wa Dar es Salaam na Miji mingine yenye uwezo kifedha huchimba visima katika nyumba zao ili kuondokana na tatizo la maji:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge ni kwa kiasi gani maji hayo ya visima ni safi na salama?

(b) Je, Serikali inatoa maelekezo gani ya kitaalam juu ya uchimbaji wa visima hivi?

**SPIKA:** Kwa wale ambao hawakuelewa kwa nini Mheshimiwa Kidawa anashangiliwa kiasi hicho hasa walioko kwenye *Gallery* huyo ndiyo Katibu mpya wa Oganaizesheni ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Maji chini ya ardhi hupatikana kwenye miamba inayohifadhi maji *(aquifers)* ambayo ina uwezo wa kutunza na kupitisha maji. Maji chini ya ardhi hutokana na mvua na maji ya mito ambayo hupenya kwenye michanga na mipasuko na hatimaye kuhifadhiwa kwenye miamba na kwa hali hiyo maji hayo ni safi na salama. Hata hivyo, shughuli nyingi za binadamu juu ya ardhi kama utupaji taka ovyo, matumizi holela ya mbolea na ujenzi wa makazi karibu sana na visima vya maji, vinaweza kuchafua vyanzo hivi vya maji. Hii ni kwa sababu mvua husomba uchafu huo na kuuingiza kwenye miamba ya kuhifadhi maji.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha usalama wa maji ya visima Wizara yangu imeweka utaratibu ambao unatakiwa kufuatwa. Utaratibu huu unahakikisha kuwa uchimbaji wa visima na matumizi ya maji yake yanazingatia maadili ya taaluma ya maji chini ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kuwa wanaotaka kuchimba visima vya maji ni lazima wafuate utaratibu kama ufuatavyo:

(1) Wapate ushauri wa kitaalamu wa utafutaji wa maeneo yanayofaa na uchimbaji wa visima vya maji ufanywe toka Wizara yangu kupitia wakala wa uchimbaji visima na ujezi wa mabwawa *DDCA*.

(2) Watumie wataalam wa maji chini ya ardhi ambao *hydorgesty* na makampuni yaliyoruhusiwa na Wizara yangu kufanya utafutaji wa maeneo yenye maji na uchimbaji wa visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufuata taratibu nilizozitaja, napenda pia kuchukua fursa hii kuwafahamisha wananchi wote kama ifuatavyo:

(1) Wananchi wasikubali kuchimbiwa visima vya maji kwenye maeneo yenye msongamano wa wakazi, madampo ya takataka, mifereji ya maji taka na mashamba ambako mbole za samadi na za viwandani zinatumiwa kwa wingi.

(2) Wahakikishe kuwa maji ya visima yanafanyiwa uchunguzi wa kemikali na kibiolojia kwenye maabara za maji kabla ya kuanza kuyatumia na uchunguzi kama huu urudiwe mara kwa mara kabla ya kuanza kuyatumia na uchuguzi kama huu urudiwe mara kwa mara ili kujihakikishia ubora na usalama wake.

(3) Wananchi wote kwa ujumla, washirikiane na Serikali kuwachukulia hatua watu binafsi ama makampuni yasiyofuata taratibu za uchimbaji visima, zilizowekwa na Serikali.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa, utaalam unatolewa na kwa kuwa pengine wananchi watafuata huo utaalam na kwa kuwa, visima vinasaidia sana Serikali katika ule mzigo wa kusambaza maji?

Je, Serikali iko tayari kufanya tathimini ni kiasi gani wananchi wanaojichimbia visima wenyewe wanasaidia mzigo huo Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba kuna wananchi wengi ambao wanajichimbia visima holela holela, kwa hali hiyo sio rahisi kufahamu idadi yao ni ngapi, lakini kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameomba kwamba kama Serikali tupo tayari kufanya uchunguzi huo na kufahamu kwamba visima jumla viko vingapi na ahadi kwamba Wizara yangu itachukua ushauri huo na kuona kitu gani tutafanya kwa ajili ya kujua hesabu ya visima.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu wa environemtal *Impact Assessment* katika viwanda mbalimbali hapa nchini. Kumekuwa na malalamiko ya wananchi wanaoishi kando kando ya migodi wa Bariki huko Nyamongo, mifugo inapokunywa maji inakufa na watu wapatao wawili hivi wameathirika vibaya na mmoja amefariki kutokana na maji hayo na inawezekana kwamba zile kemilikali zinazotumika ku-*extract gold* kama zinakuwa zimemwagwa mle. Sasa swali ni hivi.

Je, Serikali imeshafanya hiyo *Environment Impact* kwenye mgodi ule kwa sababu maji hayo pia yanateremka kwenda mto na mto Mara na Mto Mara unakwenda *Lake Victoria,* na kama bado. Je, ni lini inatarajia kufanya hivyo ili kupunguza kutoelewana baina ya wananchi na mgodi na hilo suala la mazingira.

**SPIKA:** Waheshimiwa kuna wengine walikuwa wanadhani kwamba hili ni kama swali jipya sio. Mkirudi kwenye swali utaona kwamba sehemu ya (a) inaulizia maji kuwa safi na salama. Kwa hiyo, mimi naliona ni swali safi na Serikali inabidi ijibu. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hakuna mgodi hapa nchi unaopewa ruhusa kuanza kazi bila ya kuwasilisha Serikalini, *environmental impact* assessiment, kwa maana ya kwamba ni kwa jinsi gani kazi yao ya kutafuta madini ya uchimbaji madini inaweza kuwa na athari, kwa mazingira ikiwemo. Kwa hiyo mgodi wowote ambao unapata leseni na huu ambao ameutaji Mheshimiwa Mbunge unayo leseni, umefanya hivyo, na Serikali imeridhika kwamba ina uwezo wa kutunza mazingira, lakini pia, wakati hadi wakati wachunguzi wa Wizarani na pia kutoka kwenye taasisi inayohusika na mazingira, hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuona jinsi mwenendo wa uchimbaji madini unaweza ukawa pengine unaathiri mazingira.

Serikali imekwenda mbele zaidi kwa kuanzisha tuzo maalum ya Rais kwa wenye migodi ili wahakikishe kwamba kila mwaka wale ambao wanafanya vizuri katika sekta ya mazingira wanapewa tuzo. Lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametaja mgodi mahususi, wa Nyamongo ambao ameutaja, sisi tuko tayari kufuatilia kama yeye alivyosema kama aliyoyasema yana ukweli wowote na Serikali itachukua hatua. Lakini napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba upo utaratibu madhubuti, upo utaratibu kamili na tunaufuatilia kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Na. 151

**Huduma ya Umeme**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa kijiji cha Tandala kilichopo katika Wilaya ya Makete kina hospitali kubwa ya Ikonda, Chuo cha Ualimu cha Tandala, Shule ya Sekondari na pia kuna idadi kubwa ya wananchji na kwa kuwa kijiji hicho hakina umeme:-

Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kupeleka umeme kutoka Makete umbali wa kilomita 30 tu ili kuboresha huduma hii kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inaona umuhimu wa kupeleka umeme kutoka Makete kwenda katika maeneo mbalimbali Wilayani humo, kama ilivyodhamiria kuvipatia umeme vijiji vyote nchini.

Umeme wa gridi ulishafikishwa Makao Makuu ya Wilaya ya Makete. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, umeme haukuweza kufikishwa katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa maeneo aliyoyataja yamejumuishwa katika mradi wa *Energizing Rural Transformation (ERT)* ambao Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kuufadhili.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii na pia namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo

kwa yanaridhisha. Lakini kwa kutambua ufinyu wa Bajeti kama alivyoainishwa yeye mwenyewe na kwa kutambua tatizo la umeme katika hospitali ya Ikonda na wananchi Tandala, mwezi wa tano nimeongea na wadau mbalimbali, mmoja wapo wakiwa ni wamiliki hospitali hii ya Ikonda, na wameahidi kimaandishi kwamba wako tayari kuchangia sasa hivi. (*Makofi*)

(a) Je, na maandishi hayo nimewakilisha kwenye ofisi yake. Je, Serikali iko tayari kuchangamkia ofa hii ambayo kimsingi watakaofaidi ni wananchi wa Makete? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa jana tumefahamishwa kwamba ipo haja ya kuweka vipaumbele kwenye baadhi ya maeneo kwa kuzingatia matatizo ama uchumi uliopo katika maeneo hayo. Sasa nataka kujua kwamba. Je, Serikali haioni umuhimu wa kusambaza umeme katika Kata ya Makete, kwa kutumia kigezo cha matatizo makubwa ya UKIMWI ambayo yameacha watoto yatima wengi, wajane wengi na kufanya vile kungewavutia wawekezaji na hivyo kupunguza matatizo haya katika Wilaya yangu ya Makete? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, kwa jitihada za kufuatilia maendeleo katika Wilaya ya Makete. Pia ningependa kumshukuru kwa kuisaidia Wizara yangu, kumtafuta mfadhili ambaye yuko tayari kutusaidia kusambaza umeme katika maeneo ya hosipitali na Wilaya kwa ujumla hapo Makete, ningependa kumfahamisha ni kweli barua yake tumeipokea na Wizara yangu inaifanyia kazi kuangalia ni namna gani ambavyo tutaweza kushirikiana naye pamoja na hao wafadhili, kuhakikisha kwamba umeme unasambazwa katika maeneo ya Makete.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kusambaza umeme kwa kutumia viapumbele, ni kweli Wizara yangu inaangalia nchi nzima uwezo wetu wa kifedha katika kuangalia ni wapi tuanze kusambaza umeme, na naomba nimhakikishie sio tu kwamba tunaangalia Makete peke yake lakini tunaangalia nchi nzima katika kupanga wapi tuanze kupeleka umeme kutokana na hali ya kifedha tuliyonayo.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, kwa vile tatizo kubwa Wilaya ya Makete ni ajira kwa vijana, kuwafanya vijana wengi kuondoka katika wilaya na kuwaacha wanawake na wazee peke yao ili kutafuta ajira nyingine na kwa vile Wilaya ya Makete sasa hivi wanavuna mbao ambazo hazina soko na zinachukuliwa kwa bei dogo sana, kwa sababu hakuna viwanda vya kuweza kupasua mbao kwa sababu ya ukosefu wa umeme.

Je, Serikali haioni kwamba wakati wakitafuta huo mradi wanaofikiria kuanzisha mradi wa kutumia umeme jua au kuhakikisha kwamba kuna vyanzo vingine vya maji ambavyo vinaweza kusambaza umeme na kuweza kuwapatia vijana ajira ikiwa ni pamoja na kupasua mbao na miradi mingine midogo midogo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikubaliane naye umuhimu wa umeme kusambazwa vijijini kwa ajili ya kuleta maendeleo na ni kwa sababu hii Serikali kama alivyojibu vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri ina mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini. Ili kubadilisha hali ya maisha ya wananchi wetu na tunaweza tukaibadilisha kwa kutumia tu nishati hii muhimu.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tunawasilisha Bajeti yetu hapa tutatoa dira hiyo na mwelekeo wa namna gani tuna shughulikia suala la nishati na mwaka huu kwa kweli Serikali imetenga fedha nyingi kwenye sekta ya nishati. Napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni muhimu tutafute vyanzo mbalimbali vya kuhakikisha tunazalisha umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mara nyingi tumekuwa tukisema hapa Bungeni lakini pia kupitia hotuba ya Bajeti tutakayoitoa hapa, pia kuna mpango ambao tutausema juu ya vyanzo hivi mbalimbali na kama atakumbuka Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, hata Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anawasilisha Bajeti yake hapa alizungumzia suala la nishati mbadala na kutoa unafuu maalum kwa vifaa vya umeme nuru *(SOLAR)* ili wananchi wetu vijijini waweze kupata umeme ambao unaoweza kutosheleza mahitaji yao. *(Makofi)*

Na. 152

**Mradi wa Umeme wa *Mnazi Bay***

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza

Kwa kuwa, Serikali imeibua mradi wa umeme wa *Mnazi Bay* kwa ajili ya kuipatia umeme mikoa ya Mtwara na Lindi:-

(a) Je, mradi huo unajengwa na Kampuni gani, umefikia hatua gani na lini utamalizika?

(b) Je, Wilaya zote za Mikoa ya Mtwara na Lindi ikiwemo ya Liwale zitanufaika na mradi huo na kama sio ni kwanini?

(c) Je, utakapokamilika mradi huo utamilikiwa na nani na nini itakuwa bei ya umeme huo kwa mtumiaji.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* unajengwa na Kampuni ya *Artumas Group Inc*. Kutoka Canada. Hatua zilizofikiwa ni kwamba majadiliano na mwekezaji yamekamilika na sasa Wizara inakamilisha kulifikisha suala hili kwenye Baraza la Mawaziri kupata ridhaa ya Serikali ya utekelezaji wa mradi huo. Matarajio ni kuwa wananchi wa Mji wa Mtwara watapata umeme wa uhakika kutokana na gesi ya *Mnazi Bay* katika muda si mrefu baada ya kusaini mikataba, na sehemu zingine za mikoa ya Lindi na Mtwara zitapata umeme huo baada ya mradi kukamilika katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kueleza katika maelezo yangu ya msingi wilaya zote za Mkoa wa Mtwara na Lindi ukiondoa Kilwa Masoko ambayo itapata umeme chini ya mradi wa *Way Leave Village Electrifiction* katika mradi wa Songosongo zitafaidika na mradi huu. Wilaya ya Liwale itapatiwa umeme kwenye awamu ya kwanza ya mpango utakaotumia fedha za mfuko wa *ORET*. Awamu hii inashughulikia MW 24 ambaapo wilaya tajwa itanufaika na mpango huo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, kampuni ya *ARTUMAS* wataingia mkataba wa *Franchiese* kwa muda wa miaka ishirini kwa ajili ya kuendesha mfumo wote wa umeme kuanzia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme kwa wateja katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika kipindi hicho *ARTUMAS* watakodi miundombinu ya *TANESCO* na kulipa ada kila mwaka kama watakavyokubaliana katika majadiliano. Hatua zitachukuliwa kuhakikisha kuwa bei ya uemem wa mradi inakuwa sawa na ile inayolipwa na wateja wengine nchini wanaopata umeme kutoka gridi ya Taifa.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mzuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua kwa vile sasa kati ya Nachingwea na Liwale ni kilometa 136 na hakuna nguzo za umeme, Je, mradi utakapotaka kukamilika ni lini sasa nguzo za umeme zitaanza kupelekwa Nachingwea ili zianze kusambazwa hadi Liwale kilometa 136 kutoka Nachingwea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikisha na kumthibitishia kwamba mradi huo wenyewe ndio ulitaka kuweka nguzo kuhakikisha kwamba umeme unasambazwa ipasavyo.

Na. 153

**Kiapo cha Utii wa Katiba ya Nchi kwa Wabunge**

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa kila Mbunge anayechaguliwa au kuteuliwa kwa njia halali zilizoainishwa na Katiba au Sheria husika hulazimika kula kiapo cha utii kwa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kuwapo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Je, Mbunge aliyekwisha kula kiapo cha utii wa katiba anapotamka katika kikao rasmi cha Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwa haitambui Serikali ya Zanzibar haendi kinyume na kiapo chake?

(b) Je, Mbunge wa namna hiyo, ana haki ya kuendelea kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

(c) Je, Mbunge anayetoa kauli kinyume na ibara yoyote ya Katiba anatakiwa kuchukuliwa hatua gani za kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijamjibu Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed Mbunge wa Donge lenye sehemu (a) (b) na ( c) kwa ujumla kama ifuatavyo. Ni kweli kuwa Mbunge anakula kiapo cha utii anapaswa kutekeleza wajibu wake Bungeni, kwenye Jimbo lake la Uchaguzi, na popote nchi kwa kuzingatia Katiba ya nchi. Masuala yote rasmi yanayoendelea Bunge lako Tukufu utawaliwana Sheria, Kanuni, na kanuni zilizotungwa na Bunge hili na pamoja na busara zako Mheshimiwa Spika.

*Mheshimiwa Spika, fungu la tano la sheria ya The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act No. 3* ya mwaka 1888 inawapa kinga Wabunge kutokushtakiwa Mahakamani wanapokuwa wametoa matamko kwenye mijadala ya Bunge. Hata hivyo fungu la 12 (1) la sheria hiyo hiyo inaipata Bunge kwa mujibu wa Sheria na *Standing Order* za Bunge, nguvu na mamlaka za kuchunguza na kutamka kuwa Mbunge amekiuka Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge na kutoa adhabu inayostahili.

Ningemshauri Mheshimiwa Mbunge, endapo anaamini matamshi ya Mbunge yoyote kuto kuitambua Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yamekwenda kinyume na kiapo cha Mbunge afanye utaratibu wa kuwasilisha hoja yake kwenye Kamati ya Bunge inayoshughulikia na Maadili ili uchuguzi uweze kufanyika na uamuzi uweze kutolewa.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yanaushauri mzuri wa Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hulka ya binadamu wakati mwingine kujisahau kama ilivyodhihirika humu Bungeni ambapo wewe mwenyewe umelazimika kutuweka sawa wakati mwingine kwa mavazi au kwa kauli, na kwa kuwa, imeshatokea mara kadhaa ambapo baadhi ya Wabunge kudharau mamlaka zilizchaguliwa kihalali na kwa mujibu wa Sheria. Serikali haioni kwamba wakati umefika kushauriana na uongozi wa Bunge ikawepo kanuni iliyowazi kama ile inayokataza kusema uongo humu ili ikalinda hadhi na mamlaka zilizochaguliwa kisheria na kwa mujibu wa katiba na vilevile kulinda hadhi na mamlaka ya Bunge hili?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni muhimu wote tukatambua na kulinda haki na mamlaka ya vyombo vinavyotambuliwa na katiba. Suala kubadilisha kanuni ninafahamu kwamba sasa hivi kuna Kamati ambayo inashughulikia. Kama pendekezo la Mheshimiwa Mbunge analiona lingefaa basi

lipelekwe katika Kamati ile inayoshughulikia kubadilisha kanuni, halafu tuone kama itafaa zibadilishwe, basi zitabadilishwa.

Na.154

**Pembejeo za Kilimo**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (K.n.y. MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI**) aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa pamba miaka yote hulima zao la pamba kwa ahadi nzuri za kupanda kwa bei ya zao hilo; na kwa kuwa mara nyingi mklima hujikuta amekopeshwa pembejeo kwa matatizo sana licha ya kuendelea kukopwa fedha na baadhi ya wanunuzi wa pamba:-

Je, Serikali ina mpango gain endelevu wa kuwasaidia wakulima wa pamba, kahawa, korosho na kadhalika. Kupatiwa pembejeo kwa muda muafaka na pia kuelezwa mwenendo wa masoko ya mazao hayo ili wanapofanya maamuzi ya wakulima yaweze kuwa na manufaa kwao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazao yote ya biashara yakiwemo mazao ya pamba, kahawa na korosho aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge bei zake zinatawaliwa na soko la dunia. Hata hivyo, Serikali inafanya kila linalowezekana kuhakikisha mkulima anapata bei nzuri kama vile kwa kufuta makato kwa ajili ya uendeshaji wa Bodi za mazao hayo. Aidha, kuhusu upatikanaji wa pembejeo kila moja ya mazao hayo linao utaratibu wake wa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa utaratibu waliokubaliana wadau wa zao husika.

Baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme (ASDP*) mwanzoni mwa mwaka huu 2006. Programu hiyo ya miaka saba itakayoanza kutekelezwa mwaka huu wa 2006/2007, imepangiwa kutumia shilingi Trilioni 2.5 na asilimia 75 ya fedha hizo zitatumika kugharimia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Mipango hiyo ya Wilaya itaandaliwa kwa kuibuliwa kwa utaratibu shirikishi wa wakulima vijijini kwa kuzingatia mahitaji yao halisi kwa ajili ya kuongeza tija mavuno na mapato ya wakulima zaidi ya maradufu. Sambamba na utekelezaji wa *ASDP*, Serikali inaendeleza mpango wake wa kutoa ruzuku kwenye mbolea, mbegu na madawa na kuimarisha usambazaji wake kwa lengo la kuwapatia unafuu wakulima wote nchini.

Wizara kupitia Bodi za Mazao imekuwa ikitoa taarifa za masoko kwa kutumia njia mbalimbali kama *radio*, magazeti, mikutano ya wadau na kwa kupitia vikundi au vyama vya wakulima. Hivi sasa wateja wa kampuni ya simu za *Vodacom* wanaweza kupata taarifa za bei za baadhi ya mazao makuu ya chakula katika masoko ya miji 20 kwa kutumia ujumbe usemao, MAZAO kupitia namba 155 na kupata ujumbe wa namna ya taarifa ya bei ya mazao inavyopatikana katika mojawapo ya miji hiyo. Miji hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Songea, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Shinyanga, Singida, Sumbawanga, Tanga, Tabora, Mtwara, Lindi, Musoma, Bukoba, Kogoma na Babati.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo;

Kwa kuwa, sehemu ya swali la msingi inazungumzia wakulima kukopwa na wanunuzi wa pamba, na kwa kuwa wapo wanunuzi wa pamba ambao wamewakopa wakulima katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, ambao hawajawalipa sasa hivi ikiwemo chama kikuu cha ushirika NYAZA cha Mwanza. Je, Serikali inatamka nini kuhusu hawa hususani NYAZA ina matamshi gani ya chama cha Ushirika cha NYAZA kuhusu kununua pamba wakati mnawakopa wakulima?

La pili, kwa kuwa wakulima wetu huwa hawajui bei ya pamba katika soko la dunia. Je, Serikali iko tayari kutamka bei ya pamba nyuzi ambayo ni sawa sawa na shilingi ngapi kwa bei ya pamba ya mbegu kwa tarehe ya leo ambako msimu umeshaanza jana, ili wakulima wajue na kufanya maamuzi wamuuzie nani na wauze kwa shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu wanunuzi ambao mpaka sasa hivi wanadaiwa na wakulima mbalimbali Serikali inafahamu hilo, na kwa kweli madai haya yanatokana na tofauti za bei ambazo katika kipindi cha msimu wa 2005/2006 kulikuwa na bei ambayo baadaye Serikali iliingilia kati na kuagiza kwamba ile tofauti wale wanunuzi waweze wakaifidia, baadhi ya wanunuzi wamekwisha kulipa na baadhi bado kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema. Serikali inaendelea kuwafuatilia watu hao na kusisitiza kwamba tushirikiane na Serikali kule wilayani kuhakikisha kuwafuatilia wanunuzi hawa waweze wakawalipa wakulima ambao bado wanawadai na ikizigatiwa kwamba fedha hizo ambazo zinadaiwa na wakulima hawa zilitokana na baadhi ya makato ambayo yalikuwa yameondelewa kutokana na majadiliano yaliyokuwa yamefanyika na Serikali katika kipindi kile.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu suala la bei, kama nilivyokuwa nimeeleza katika jibu la msingi kwamba bei za mazao haya ya biashara utawaliwa na bei ya soko la dunia, na ili kuepuka lile tatizo lililotupa kipindi kilichopita la kujaribu kuweka bei ya dira ambayo ilituletea matatizo kabla hatujajua bei yasoko la dunia ndio maana sasa hivi hatuwezi kutamka moja kwa moja kwamba bei sasa hivi ni kiasi gani mpaka hapo tutakapokuwa tumepata uhakika ya kwamba bei ya soko la dunia iko kiasi gani. Kwa hiyo nataka tu nimuhakikishe Mheshimiwa Mbunge tutakapokuwa tumefanya zoezi hilo

tutakuwa tayari kumfahamisha ili wakulima waweze wakajua kwa uhakika bei ya soko la dunia ina simama vipi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kazi moja ya Serikali ni kuhimiza na kuhamasisha wakulima kama wakulima wa pamba waongeze mazao yao na mojawapo ya hamasa ni kuhakikushia wakulima hawa watapata fedha ngapi baada ya kulima. Ni kwanini Serikali haitengi fedha ambayo angalau itafidia bei kama ikiteremka kutoka kiwango kile ambacho nafikiri kinaweza kikawahamisha wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi mojawapo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inawahamasisha wakulima ili waweze kuzalisha zaidi na hatimaye wajipatie kipato kikubwa zaidi.

Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba moja ya zoezi ambalo tunalifanya sasa hivi ni lile la kukubaliana kuondoa makato karibu yote ambayo yalikuwa yanapunguza pato la mkulima. Kwa hiyo, hii mojawapo tu inamhakikishia mkulima kwa mwaka huu angalau bei itakuwa juu zaidi kuliko kipindi kilichopita. Kwa hiyo, kumwongezea ari ya kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kutenga mfuko wa kufidia bei, nataka niseme kwamba Serikali inafanya maandalizi ya kuangalia uwezekano wa kuanzisha mifuko hiyo pamoja na mfuko wa kinga ya bima ambayo yote kwa pamoja ina lengo la kumsaidia mkulima katika kujipatia kipato zaidi.

**SPIKA:** Tunaendelea. Naona kwa lugha ya Waandishi ya Habari bado Wizara ya Miundombinu mnataka kuikaba koo. Mheshimiwa Anne Kilango, swali kwa Wizara ya Miundombinu? *(Kicheko)*

Na. 155

**Barabara za Same Mashariki**

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Same Mashariki takriban asilimia 60 wanaishi kwenye milima mirefu na kwa kuwa wananchi hao, wamekuwa wanatengeneza barabara zao wenyewe na msaada mwingine wanapata kutoka kwenye fedha za Halmashauri ya Wilaya.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzipandisha daraja barabara hizo zishughulikiwe na Mkoa kwa sababu barabara hizi ni nyingi sana na zinabeba maisha ya Watanzania walio wengi sana?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, majibu ya kuridhisha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Wilaya ya Same wanaoishi maeneo ya milimani ni maarufu kwa kujitengenezea barabara zao huko milimani kwa miaka mingi sana. Nami nawapongeza sana wananchi hawa kwa moyo wao huo wa kujitolea na kujitegemea. Aidha, Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Kilimanjaro na Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa pamoja zimeendelea kuhudumia barabara zilizoko chini ya miliki zao kwa kushirikiana na wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, suala la kupandishwa daraja kwa barabara hizi ni la kisheria na lina taratibu zake na vigezo vinavyotumika. Kwa hivi sasa Wizara yangu inaendelea na maandalizi ya sheria mpya ya barabara. Sheria hii itapitia tena barabara zote na kuziweka katika madaraja husika kulingana na vigezo vitakavyowekwa na sheria hiyo. Zipo barabara zitakazopanda au kushushwa madaraja. Matarajio ya Wizara yangu ni kuwa Sheria mpya ya Barabara itafikishwa Bungeni kwa mara ya kwanza mnamo mwezi Novemba, 2006. Katika mchakato huo, barabara za Wilaya ya Same zitafikiriwa ipasavyo kulingana na vigezo vitakavyowekwa kwa nchi nzima na uwezo wa Serikali kubeba gharama za barabara nyingi za hadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunashauri Mheshimiwa Mbunge kuendelea kuhamasisha wananchi ili wasaidiane na Serikali kuondoa kero hii ya barabara. *(Makofi)*

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba wakati ninapouliza maswali yangu mawili ya nyongeza, ninukuu mambo kidogo kutoka kwenye jedwali hili nilililoshika mkononi, ni jedwali la Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tarehe 20 Aprili, 2006 tulikutana kwenye Kikao cha Bodi ya Barabara Mkoani Kilimanjaro na Mheshimiwa Waziri alikuwepo. Kwa kuwa katika kikao hicho niliongelea jambo hili na Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe akakubali kwamba uchumi wa Same Mashariki uko ndani ya chupa kwa sababu ya barabara hizi kutoshughulikiwa. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe alimuamuru Mkuu wa Mkoa aunde Tume pamoja na *TANROADS* waende kuangalia barabara hizo na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alifanya kazi hiyo na amemshamletea mapendekezo kuhusu barabara hizi. Je, Serikali sasa inasema nini baada ya kupokea mapendekezo kama alivyotaka Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hizi za milimani zinategemea barabara yangu ya kutoka Mkomazi – Bendera – Kihurio – Ndungu – Maore – Kisiwani – Same na kwa kuwa barabara hii narudia tena ndio barabara pekee ya Mkoa wa Kilimanjaro ambayo haijawekwa lami na kwa kuwa Serikali katika kipindi hiki cha bajeti imeweka lami barabara nyingine ambazo hazikuwa wala barabara za Taifa je, Serikali inasema nini kuhusu barabara hii ya Taifa? *(Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona nimepitiliza muda wa kawaida wa maswali kwa sababu nafidia muda.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mkuu wa Mkoa na *TANROADS* kuunda Tume kuangalia barabara hizo, ripoti ya Tume hiyo imewasilishwa kwenye Kamati inayofanya mchakato wa kuangalia barabara gani zipandishwe na zipi zishushwe na majibu yake kama nilivyosema tutayaona mwezi Novemba, 2006. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri tuangalie kama barabara hizo zitapandishwa.

Kuhusu barabara ya Mkomazi – Same kwamba ndio barabara pekee katika Mkoa wa Kilimanjaro ambayo haijawekewa lami hiyo sio kweli. Kuna barabara kadhaa za Mkoa wa Kilimanjaro ambazo hazina lami lakini kitu cha muhimu ni kwamba uwekaji wa lami katika barabara zetu kwa kweli unategemea uwezo wa kifedha. *(Makofi)*

Tumesema kwamba mkakati wa Kitaifa ni kuweka lami barabara kuu kwanza halafu baadaye tunakwenda kwenye barabara za Mikoa kulingana na uwezo. Kwa hiyo, kitu kikubwa hapa ni uwezo na pindi uwezo utakapopatikana barabara za nchi hii zote zitawekwa lami lakini kwa muda huu tuendelee kuvumilia kwamba barabara nyingine zitaendelea kukarabatiwa kwa changarawe na udongo mradi tu ziwe zinapitika kwa kipindi chote. *(Makofi)*

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa barabara nyingi za milimani zina miamba mikubwa na inayohitaji pesa nyingi sana kupasua miamba hiyo na Halmashauri zetu za Wilaya hazina uwezo mkubwa kifedha wa kupasua miamba ukizingatia inahitaji kutumia baruti pamoja na teknolojia nyingine za kisasa zaidi.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa hivi Halmashauri za Wilaya ambazo zina barabara zilizoko milimani na zina miamba mikubwa hazipati fedha za kutosha ili kuweza kumudu kupasua miamba ile na je, wako tayari kuongeza nyongeza katika Mfuko wa Barabara kutoka 30% hadi 50% kutokana na ugumu na unyeti wa kazi yenyewe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara zetu nyingine ni za

milima, miamba lakini nyingine vile vile ziko kwenye mabonde ambapo ina mito mikubwa. Kwa hiyo, hali ya nchi kwa kweli inatofautiana kutoka mahali mpaka mahali.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine ambao wana matatizo ya miamba, kuna wengine wana matatizo ya mito, lakini hiyo haiwezi kufanya sasa Wizara ya Miundombinu ikaanza kutoa hela kwa ajili ya kushughulikia barabara ambazo ziko chini ya Halmashauri. Lakini pale ambapo uwezo unapatikana tumekuwa tukisaidia. Ningeshauri Mheshimiwa Mbunge angetoa mfano wa barabara hiyo anayosema ina miamba ili tujue Halmashauri hiyo husika imeshindwaje na imeomba msaada gani na Serikali ikashindwa labda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu fedha za mfuko za barabara kuongezwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kushughulikia barabara za miamba nadhani suala sio hilo ni kwamba mtandao wa barabara za Halmashauri ni mkubwa kilomita karibu 50,000 na kwa kweli kiasi cha 30% kimeonekana ni kidogo na Serikali inaangalia ifanyeje kuongeza *percent* hiyo inayokwenda kwenye Halmashauri. Hili Serikali inalifanyia kazi na pindi Wabunge watajulishwa.*(Makofi)*

Na. 156

**Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa Tanzania *(Meteorological Department)* ni moja kati ya taasisi za Muungano inayotegemewa zaidi na wakulima wengi nchini:-

(a) Je, Taasisi hiyo inawasaidia vipi wakulima ambao hukumbwa na mabadiliko mabaya na ya kushtukiza ya hali ya hewa ambayo huleta hasara kubwa?

(b) Je, uwiano wa vituo vinavyokusanya taarifa za mabadiliko ya hali ya hewa kati ya Tanzania Bara na Zanzibar unawakilisha mahitaji halisi ya Idara?

(c) Je, uwiano wa watendaji wakuu wa Idara hizo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya Hali ya Hewa ilianzishwa kuwa Wakala wa Serikali mwaka 1999 kutoka iliyokuwa Idara Kuu ya Hali ya Hewa. Mamlaka hii ni moja kati ya taasisi za Muungano ikiwa na lengo la kutoa pamoja na mambo mengine, taarifa muhimu zinazo wasaidia wakulima katika kupanga mipango yao ya kilimo. Taarifa hizi huwafikia wakulima kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo za radio, televisheni na magazeti. Mamlaka pia hutumia ofisi za Serikali zikiwemo za wakuu wa Wilaya na ofisi za kilimo za Wilaya. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hamed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuwasaidia wakulima kwa kutoa taarifa za hali ya hewa kupitia maafisa kilimo kwa nia ya kuwapa tahadhari kuhusu mabadiliko ya mwenendo wa hali ya hewa na hivyo kuwawezesha kuchukua hatua zinazofaa. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kujiandaa mapema kwa kilimo kama utabiri wa hali ya hewa utaonyesha kuwa mvua zitaanza mapema.

(ii) Aina ya mazao ya kupanda hasa mazao yanayovumilia ukame kama utabiri utaonyesha kuwa mvua zinazotegemewa kunyesha ziko chini ya wastani.

(iii) Kuchukuwa hatua za kutotumia vibaya chakula kilichopo pale utabiri utakapoonyesha kuwa hali inayotegemeWa ni ya ukame.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na sheria za Kimataifa kuhusu mtandao wa vituo vikuu (*synoptic stations*) vya hali ya hewa ni kwamba kunatakiwa kuwepo kwa kituo kimoja cha hali ya hewa kwa kila kilometa za mraba 250. Tanzania inazo kilometa 944,983 za mraba na kati ya hizo Tanzania Zanzibar ina kilometa 244 za mraba.

Mamlaka hivi sasa inavyo vituo vikuu vya hali ya hewa vipatavyo 27 ambapo vituo 25 viko Tanzania Bara na vituo viwili (2) viko Visiwani. Kutokana na tathmini hii ni dhahiri kuwa Tanzania Visiwani imekidhi mahitaji ya Kimataifa wakati Tanzania Bara ina upungufu mkubwa. Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa bado inaendelea kuongeza mtandao wa vituo vikuu vya hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe ambayo pia vitawekwa kwa upande wa Tanzania Visiwani. Kwa sasa tunayo mitambo miwili ya kutayarisha matangazo ya hali ya hewa (*weather studio*) mmoja umewekwa katika ofisi za Zanzibar na mwingine Dar es Salaam.

(c) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye hupatikana kwa njia ya ushindani unaokidhi vigezo vilivyowekwa kwa nafasi hiyo na waombaji wa nafasi hii hutoka pande zote mbili za muungano. Mamlaka hii ina Wakurugenzi wanne ambao wote wanatoka Tanzania Bara na Mameneja 29 ambao wanne kati ya hao wanatoka Visiwani na waliobaki wanatoka Tanzania Bara. Kama ilivyo kwa nafasi ya Mkurugenzi Mkuu nafasi za Wakurugenzi na Mameneja hupatikana kwa ushindani na waombaji hutoka pande zote mbili za Muungano.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Ninayo matangazo yafuatayo. Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo, anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 5 Julai, 2006 saa saba na robo mchana chumba na.219 jengo la utawala.

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa tano asubuhi ukumbi namba 133, ghorofa ya kwanza, jengo la utawala

Katibu wa *Tanzania Women Parliamentary Group*, Mheshimiwa Eliatta Switi, anapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanawake wanaokwenda kwenye maonyesho ya biashara Dar es Salaam kwamba mabasi ya Bunge yatakuwa tayari na yameegeshwa mbele ya jengo la ukumbi wa zamani wa Bunge. Spika anawatakia safari njema.

Nimeombwa hapa na naliona ni jambo halali tu, Wabunge kadhaa wanawakumbusha Waheshimiwa Mawaziri tunavyokwenda kwenye sekta kulikuwa na ahadi wakati wa michango kwenye Wizara za Fedha, Mipango na Ofisi za Waziri Mkuu zilizosema kwamba majibu yatapatikana kwenye sekta. Sasa tunaanza kilimo zipo ahadi zilizoachwa zinazohusu kilimo.

Kwa hiyo, ni kukumbusha tu itakapofika wakati huo kwa sababu hakuna muda wa Waheshimiwa wote kuchangia, yale yaliyosemwa wakati ule katika wiki mbili zilizotangulia inabidi pale ilipoguswa sekta tuna imani kwamba Waheshimiwa Mawaziri na wataalam waliandika hoja zile zipewe heshima ya kujibiwa wakati sekta husika inapojibu hoja. *(Makofi)*

Leo jioni nitamwachia Kiti Mheshimiwa Jenista Mhagama. Siyo kwamba nimechoka ni kwamba nimekuta ndani ya ofisi katika wiki hizi zote majalada mengi sana na mengine yanahusu maamuzi ambayo lazima yachukuliwe haraka. Kwa hiyo, leo nitatumia muda kukaa ofisini hadi jioni kuweza kufanya kazi hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista atakuwa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, alipata msiba, alifiwa na mdogo wake, Mheshimiwa Job Ndugai anaongoza ile Kamati ndogo ya Mambo ya Kanuni wako India. Kwa hiyo, wa kuruhusiwa kukaa hapa kwenye Kiti hiki

ni mimi na Mheshimiwa Jenista peke yake. Kwa hiyo, jioni ndio itakavyokuwa hivyo na kesho nitarejea.

Baada ya matangazo hayo, Katibu shughuli inayofuata. Endelea na *Order Paper. (Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007. Nawashukuru sana Mwenyekiti Mheshimiwa Gideon A. Cheyo na Waheshimiwa Wajumbe wengine wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kuipitisha Bajeti ya Wizara yangu na kuiunga mkono ipitishwe na Bunge hili Tukufu. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba zao za Bajeti na maelezo yao juu ya umuhimu wa kilimo katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mufindi Kaskazini, tunaungana na Watanzania wenzetu kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi huo mkubwa wa asilimia 80.28 ni matokeo ya imani na matumaini makubwa waliyonayo wananchi kwa Mheshimwa Rais Kikwete juu ya uwezo wake wa kuliongoza Taifa letu kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena kuwa Makamu wa Rais; na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kuchaguliwa kwao kunatokana na rekodi nzuri ya uongozi wao wakiwa katika madaraka hayo katika miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuchaguliwa tena na wananchi wa Jimbo lake la Uchaguzi la Monduli na kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na kupitishwa na Bunge hili kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu. Kuteuliwa kwake kunatokana na uwezo wake mkubwa na umahiri aliotuonyesha katika kutenda na kusimamia kazi, hususan katika ngazi ya Uwaziri wa Wizara mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, nachukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mbunge wa Urambo Mashariki kwa kuchaguliwa kwa

kura nyingi kuwa Mbunge na Spika wa Bunge letu Tukufu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza pia Waheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu Tukufu. Huo ni mchanganyiko mzuri wa kijinsia na pia wa umri wa kati na vijana katika uongozi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa wabunge wenzangu wote kwa ama kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bunge hili Tukufu. Kuchaguliwa na kuteuliwa kwao kunatokana na uwezo wao wa kuongoza na kuaminika kwa wananchi waliowachagua na Rais aliyewateua.

Katika Uchaguzi Mkuu uliopita, wananchi wamekipa tena Chama cha Mapinduzi (CCM) ridhaa ya kuongoza nchi hii kwa kuwachagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wabunge wengi kutoka Chama cha Mapinduzi. Huu ni ushahidi kuwa Sera za Chama Cha Mapinduzi zinakubalika na zinatekelezeka. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuzinadi sera hizo kwa umahiri mkubwa mpaka Chama chetu kikapata ushindi mkubwa. Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kuzitekeleza vizuri ili kuhakikisha Chama chetu CCM kinaendelea kuongoza Taifa hili kwa miaka mingi ijayo. Aidha, nawapongeza Naibu Mawaziri na Mawaziri wenzangu kwa kupewa madaraka hayo na Mheshimiwa Rais. Aidha nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Luteni Yusuf Makamba kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na hivi karibuni kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Kwa wote ndani ya Bunge hili, nawaomba kama usemavyo ule mstari wenye maneno matatu katika Kitabu cha Mungu cha Injili: "Tupendane Tushirikiane Tusaidiane". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wetu wa ngazi za juu wa Serikali ya Awamu ya Nne kwa kukipa kilimo msukumo mpya. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, wakati alipozindua Bunge hili Tukufu aliainisha maeneo ambayo yataleta mapinduzi katika Kilimo. Aidha, Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika tarehe 18 Januari, 2006 alitoa mwelekeo kuhusu jinsi anavyotaka kilimo kiwe na kutoa maelekezo na maagizo ambayo yametupa changamoto na mchango mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Katika Hotuba zake za mwisho wa mwezi, Mheshimiwa Rais amekuwa akifafanua masuala mbalimbali kuhusu kilimo, jambo ambalo limewapa hamasa kubwa wadau wa kilimo. Aidha, kufuatia ukame ulioyakumba maeneo mengi ya nchi yetu mwaka 2005/2006, Mheshimiwa Rais alitembelea sehemu mbalimbali za nchi yetu, ikiwa ni pamoja na maeneo ya biashara yakiwemo maghala na masoko ya vyakula ili kujionea hali ya upatikanaji na bei za vyakula. Katika ziara alizofanya, Mheshimiwa Rais alitoa maagizo na maelekezo yaliyowezesha vyakula kuagizwa kutoka nje kwa wingi na hivyo kupunguza kasi ya kupanda kwa bei. Tunamshukuru sana kwa uongozi wake wa karibu sana kwa Wizara yetu katika kipindi hicho ambapo nchi yetu ilikuwa ukingoni mwa janga la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, katika ziara ambazo amekuwa akifanya Mikoani, amekuwa akitenga muda wa kutosha kukagua na kuona shughuli za kilimo na kutoa maagizo mbalimbali kuhusu kilimo endelevu na

kinachozingatia ulinzi wa mazingira. Wizara yangu tayari imeanza kutekeleza maagizo hayo kwa kuandaa miongozo mbalimbali na mapendekezo yatakayowezesha kutungwa kwa Sheria ya Kilimo na kuhimiza Halmashauri zote nchini kutunga Sheria Ndogo za kuwafanya wadau wa kilimo kufanya shughuli zao katika namna ambayo inalinda mazingira, na inaleta mageuzi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa nyakati tofauti, ametembelea Wilaya mbalimbali nchini ili kujionea mwenyewe matatizo ya upungufu wa chakula yaliyokuwa yanawakabili wananchi na kuzungumza na wananchi na viongozi kuhusu namna ya kukabiliana na upungufu wa chakula uliokuwepo na siku za baadaye. Aidha, Waziri Mkuu amekuwa akitoa maelekezo mbalimbali ya kuendeleza kilimo ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa usimamiaji mzuri wa chakula cha njaa kuwafikia walengwa na kuokoa maisha ya waliokuwa wameishiwa kabisa chakula. Mheshimiwa Waziri Mkuu pia aliitisha mkutano wa wahisani ili kuwapa taarifa kuhusu hali ya nchi yetu kuwa ukingoni mwa janga la njaa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru nchi rafiki, mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, makampuni na watu binafsi kwa kuitikia wito wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kutoa misaada ya fedha, vyakula na mbegu kwa ajili ya wananchi walioathirika kutokana na ukame. Misaada yao tunaithamini sana na tutaendelea kuhitaji misaada yao hadi hali ya chakula nchini itakapokuwa nzuri. Nawashukuru sana Waheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa hatua walizochukua. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza sana viongozi wa Awamu ya Tatu tuliowapokea: Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa, Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Frederick Sumaye na Waziri wa Kilimo na Chakula Mstaafu Mheshimiwa Charles Keenja kwa sababu katika *Kihenge* cha Taifa (*Strategic Grain Reserve*) walituachia tani 112,000 na pia akiba ya kutosha ya fedha za kigeni tulizoagizia chakula tani 42,000 kutoka nje ili kuokoa maisha ya wananchi waliokuwa wanakabiliwa na janga la njaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni aliitisha mikutano ya wadau wa mazao ya korosho, tumbaku, kahawa na pamba. Katika mikutano hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo ambayo yametoa dira ya kuendeleza mazao hayo. Aidha, Waziri Mkuu aliziagiza Wilaya zote nchini kukipa kilimo umuhimu wa kwanza kutokana na fursa kiliyonayo katika kumwendeleza mkulima. Wizara yangu imekwishatoa mwongozo wa namna ya kuendeleza kilimo katika ngazi za Wilaya na Vijiji. Tunamshukuru sana Waziri Mkuu kwa kukipa msukumo kilimo na tunamuahidi kuwa tutatekeleza maagizo yake kwa kasi kubwa kwa lengo la kuongeza tija, mavuno na mapato ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa ushirikiano mkubwa wanaoipa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Kwa muda mfupi tangu kuundwa kwa Kamati hiyo, imetembelea Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuona utekelezaji wa mipango ya kilimo. Aidha, tarehe 31 Mei 2006, Kamati ilipokea na kuchambua kwa kina Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya Mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2006/2007. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo yamezingatiwa katika Mpango wa Wizara ambayo leo nauwasilisha katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, na Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Juma Halifa Ngasongwa, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mbalimbali yanayohusu kilimo. Wakati wa kujadili hotuba hizo, Waheshimiwa Wabunge wameonyesha jinsi wanavyokifahamu kilimo na wametoa ushauri wa usimamizi na utekelezaji wa maendeleo ya kilimo. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa ushauri wao utazingatiwa katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ukuaji wa Sekta ya kilimo umeendelea kuboreka. Katika mwaka 2004, kilimo kilikua kwa asilimia 5.8 ambapo mwaka 2005 kilikua kwa asilimia 5.2. Sekta ndogo ya mazao ilikua kwa asilimia 6.0 na asilimia 5.2 katika kipindi hicho. Hata hivyo, kasi hiyo ya ukuaji bado ni ndogo kukiwezesha kuchangia kikamilifu katika kuondoa umaskini na kutoa msukumo wa kutosha kuuwezesha uchumi wa Taifa kukua kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, ukuaji wa Sekta ya Kilimo katika miaka ya hivi karibuni umekuwa ukiathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa mfano, katika mwaka 2005/2006 maeneo mengi ya nchi yetu yalikumbwa na ukame. Kutokana na ukame huo, uzalishaji wa baadhi ya mazao ya chakula na biashara katika mwaka 2006/2007 utaathirika.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 80 ya kilimo cha Tanzania ni cha wakulima wadogo ambao hulima kati ya hekta 0.2 na hekta 2.0. Asilimia 70 ya wakulima hao hutumia jembe la mkono, asilimia 20 majembe ya kukokotwa na wanyamakazi na asilimia 10 tu hutumia matrekta. Mazao mengi huuzwa ghafi kwa bei ndogo katika masoko ya ndani na nje. Utumiaji wa mbolea za madini (*mineral fertilisers*) na mbegu bora ni mdogo mno. Aidha, ni asilimia 11.5 tu za eneo linalofaa zaidi (*high potential*) kwa kilimo cha umwagiliaji ndilo linalotumika. Hali hii imekifanya kilimo cha nchi hii kuendelea kuwa cha kujikimu.

Mheshimiwa Spika, Kilimo cha Tanzania kinakabiliwa na upotevu mkubwa wa mazao yakiwa mashambani na baada ya kuvunwa. Upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno unafikia wastani wa kati ya asilimia 30 na 40. Upotevu huo husababishwa na visumbufu vya mimea na mazao hususan, panya, kwelea kwelea, viwavijeshi, nzige na magonjwa ya mimea. Aidha, upotevu huo unachangiwa na kutozingatiwa kwa kanuni bora za utunzaji wa mazao na ukosefu wa miundombinu bora ya kuyaandaa, kuyasafirisha na kuyahifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi ya kilimo nchini kuna upotevu mkubwa wa udongo wenye rutuba unaosababishwa na uharibifu wa mazingira. Udongo huo huchukuliwa na maji ya mvua nyakati za mvua na upepo nyakati za ukame. Hali ni mabaya zaidi kwenye Mikoa yenye mifugo mingi na yenye vipindi virefu vya ukame, ikiwemo Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Shinyanga, Mwanza, Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kuwa na rasilimali nyingi za ardhi nzuri, maji mengi na nishati ya jua ya kutosha. Rasilimali hizo zikitumika kikamilifu, zinaweza kuongeza sana mavuno ya mazao ya kilimo. Inakisiwa tunazo hekta milioni 44 zinazofaa

kwa kilimo lakini zinalimwa milioni 10.8 tu, sawa na asilimia 24.5. Aidha, kuna hekta zipatazo 2,300,000 zinazofaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini kwa sasa ni hekta 264,388 za eneo lilanofaa kwa kilimo hicho limeendelezwa. Maji mengi ambayo yangeweza kutumika katika uzalishaji mashambani huachwa kuelekea kwenye mito, maziwa na bahari na pengine kusababisha mafuriko ambayo huleta maafa na uharibifu wa mashamba, miundombinu ya kiuchumi na mali nyingine.

Mheshimiwa Spika, Ushirika ni chombo muhimu cha kupambana na umaskini kwa njia ya kuunganisha uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kwa kukusanya nguvu zao kwenye Vyama vya Ushirika, ambavyo vinaweza kutoa mchango mkubwa katika kuendeleza kilimo na kazi nyingine za kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Vyama vya Ushirika vinakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo:-

- Ubadhirifu wa fedha na mali za wanachama;
- Uongozi usio wajibika kwa wanachama;
- Uwezo mdogo wa *COASCO* kukagua mahesabu ya vyama vya ushirika; na
- Elimu duni ya wanachama kuhusu ushirika na haki na wajibu wao kama wanachama.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya kuvisadia vyama vya ushirika kukabiliana na matatizo hayo, Serikali, kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Ushirika ya 2002 na Sheria ya Ushirika ya 2003, imeandaa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini ambayo lengo lake kuu ni kuwa na Vyama vya Ushirika vinavyoundwa kutokana na mahitaji ya wanachama na kusimamiwa na wanachama wenyewe. Programu hii itatekelezwa katika kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2005 hadi 2015. Awamu ya kwanza imeanza kutekelezwa mwaka 2005 na itakamilika mwaka 2010. Programu hiyo imeweka mkazo katika kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wanachama wake ya kiuchumi na kijamii kwa wakati.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi za uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika zinazotekelezwa na Wizara pamoja na wadau wa ushirika zinaonyesha matokeo mazuri. Mafanikio hayo yanatokana na kuanzishwa kwa vyama vipya na kuongezeka kwa wanachama wapya kwenye vyama vilivyopo. Idadi ya vyama vya ushirika wa aina mbalimbali vimeongezeka kutoka vyama 5,730 mwaka 2005 hadi vyama 5,832 mwaka 2006. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo imetokana na vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)* kuongezeka kutoka vyama 1,875 mwaka 2005 hadi vyama 2,028 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 katika SURA YA TATU inasema: “Kilimo cha kisasa ndio msingi wa uchumi wa kisasa”. Imefafanuliwa bayana katika ibara ya 30 kuwa: “Kilimo ndio msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika modenaizesheni ya uchumi wa Tanzania. Kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa”. Ibara ya 31 kifungu cha (a) hadi (p) imeainisha hatua za kuchukua kukifanya kilimo kikue kwa kasi kubwa zaidi. Kuhusu Ushirika Ilani hiyo katika Ibara ya 50(b) inasema: “Ushirika ndio njia kuu ya uwezeshaji kwa wananchi walio wengi. Ushirika ni njia ya kukusanya nguvu”. Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne imezingatia

maelekezo hayo katika mipango yake na imeanza kuyatekeleza katika Bajeti ya mwaka huu 2006/2007 kwa kufanya mambo makubwa manne yafuatayo:-

- La Kwanza: Kuongeza ruzuku ya mbolea na mbegu mara tatu kutoka Shilingi Bilioni 7.0 mwaka jana hadi Shilingi Bilioni 21 mwaka huu, na wingi wa mbolea ya ruzuku maradufu kutoka tani 63,000 mwaka jana hadi tani 129,000 mwaka huu;

- La Pili: Kuanza utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme* (*ASDP*) ya miaka saba (2006/2000 – 2012/2013) itakayogharimu Shilingi Trilioni 2.5 inayolenga kuongeza tija, mavuno na mapato ya wakulima Vijijini zaidi ya maradufu. Ufafanuzi wa *ASDP* nitautoa katika maelezo ya mpango wa mwaka 2006/2007;

- La Tatu: Kupitia *ASDP* kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kutoka hekta 264,388 za sasa hadi hekta 1,000,000 ifikapo 2010. Miradi ya Umwagiliaji ya Wilaya imekisiwa kugharimu Shilingi trilion 1.493 na ya kitaifa Shilingi bilion 474; na

- La Nne: Kuanza utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika ambayo imepangiwa katika Bajeti hii Shilingi bilioni 4.7.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbolea za madini nchini ni wastani wa kilo nane za virutubisho kwa hekta kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa kilo 60 kwa hekta unaopendekezwa na wataalam ili kurejesha kiwango hicho kinachotumiwa na mimea kila mwaka. Matokeo ya matumizi hayo madogo uzalishaji wa mzao unaondoa virutubisho katika udongo kwa wingi kuliko vinavyorejeshwa.

Kwa mfano, tathmini iliyofanywa na watalam wa kimataifa inaonyesha kwamba Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zinaondoa virutubisho kwenye ardhi kuliko inavyovirejesha Nchi nyingine duniani hutumia viwango vikubwa vya mbolea kwa hekta kwa mwaka: kwa mfano, India kilo 103, Marekani hutumia kilo 105, Ufaransa kilo 225, China kilo 275, Uingereza kilo 288, Uholanzi kilo 578, Afrika Kusini kilo 63, Malawi kilo 27 na Misri inayoongoza katika Afrika kilo 437. Wastani wa matumizi ya mbolea katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara (*Sub-Sahara Africa)* ni kilo 8 kwa hekta. Hata hivyo, matumizi ya mbolea nchini yameanza kupanda kutokana na kuanza tena utaratibu wa kutoa ruzuku kwenye mbolea mwaka 2003/2004. Kutokana na hatua hizo, utumiaji wa mbolea umepanda kutoka tani 70,540 mwaka 2000/2001 hadi tani 121,000 mwaka 2005/2006, sawa na ongezeko la asilimia 41.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapinduzi ya kijani (*Green Revolution*), lengo lililopitishwa na Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni kuongeza matumizi ya mbolea hadi:

- Tani 700,000 ifikapo mwaka 2009/2010 ili kufikia virutubisho vya wastani wa kilo 50 kwa hekta; na
- Tani milioni 1.4 mwaka 2014/2015 ili kufikia virutubisho vya wastani wa kilogramu 100 kwa hekta ifikapo mwaka 2015.

Uamuzi huu ambao kama inavyobidi utaendana na utumiaji wa mbegu bora ni wa kuiingiza nchi yetu katika Mapinduzi ya Kijani (*Green Revolution*) na kuiaga kabisa njaa kama walivyofanya wenzetu wa India, Pakistan na China kwa kutumia mkakati kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa mahitaji ya mbegu bora nchini ni zaidi ya tani 120,000 kwa mwaka. Matumizi ya mbegu bora yalifikia tani 12,830 mwaka 2004/2005, sawa na asilimia 10.7 ya mahitaji. Utumiaji wa mbegu bora ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo hususan zikitumiwa pamoja na mbolea. Serikali imeanzisha Wakala wa Mbegu wa Taifa (*National Seed Agency*) utakaozalisha mbegu kutosheleza mahitaji, ambao ulizinduliwa rasmi tarehe 23 Juni, 2006.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji. Upatikanaji na matumizi endelevu ya maji katika kilimo ni muhimu ili kuhakikisha wakulima wanapata tija kubwa sanjari na matumizi ya mbolea na mbegu bora. Kwa kuzingatia hilo, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(National Irrigation Master Plan (2002).* Katika mwaka 2005/2006, Wizara ililenga kuongeza eneo la uzalishaji kwa kutumia Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani kwa jumla ya hekta 18,000 ili kufikia jumla ya hekta 268,000. Hadi mwezi Mei 2006, skimu 63 zenye jumla ya hekta 14,396 zilikuwa zimekamilika na kufanya jumla ya eneo lililoendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji kufikia hekta 264,388.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula katika mwaka wa 2004/2005 ulikuwa tani milioni 9.79 zikiwemo tani milioni 5.40 za nafaka na tani milioni 4.39 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula yalikuwa tani milioni 9.55. Takwimu hizo zilionyesha kwamba Taifa lingejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 103. Hata hivyo, bei kubwa za vyakula zilizotokana na upungufu mkubwa wa chakula katika nchi jirani hususan Malawi na Zambia, ziliwashawishi baadhi ya wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya chakula nchini kuuza mazao hayo kwa wingi katika nchi hizo. Takwimu zinaonyesha kwamba, kati ya Julai 2005 na Machi 2006 jumla ya tani 158,392 za mazao ya chakula ziliuzwa nje ya nchi: zikiwemo tani 140,094 za mahindi, tani 10,848 za mchele; na tani 7,450 za maharage. Sambamba na hali hiyo, mvua za vuli ambazo kwa kawaida huanza kunyesha mwezi Septemba zilichelewa kuanza na zilinyesha kwa mtawanyiko mbaya na usiokidhi mahitaji ya kilimo. Aidha, mvua ndefu za mwaka ambazo kwa kawaida huanza kunyesha katikati ya mwezi wa Novemba, nazo zilichelewa kuanza kwa takriban miezi miwili. Kutokana na hali hiyo, nchi ilikumbwa na upungufu wa chakula katika mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini za kina za hali ya chakula zilizofanywa mwezi wa Agosti na Septemba na Novemba, 2005 zilionyesha kwamba wakulima wapatao 613,405 walipata mavuno ya mazao ya chakula chini ya asilimia 30 ya mahitaji yao na walihitaji jumla ya tani 21,499 za chakula kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Novemba, 2005 ili kuwafikisha kwenye mavuno ya mvua za vuli. Kutokana na kutonyesha vizuri kwa mvua za vuli, Serikali na wadau wa Usalama wa Chakula walifanya tathmini nyingine mwishoni mwa mwezi wa Januari na mwanzoni mwa mwezi Februari, 2006. Matokeo ya tathmini hizo yalionyesha kwamba watu 3,764,843 walikuwa na upungufu wa chakula na kati yao watu 564,723 hawakuwa na uwezo wa kujinunulia chakula hata cha bei nafuu.

Tathmini hiyo ilionyesha kwamba jumla ya tani 99,676 za chakula zilihitajika kwa ajili ya watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoliarifu Bunge lako Tukufu, katika hotuba yake, Serikali ilitoa tani 122,638 za mahindi na kati yake tani 15,537 zilitolewa bure na tani 107,101 ziliuzwa kwa bei nafuu ya Shilingi 50 kwa kilo. Aidha, ili kuhakikisha kuwa wananchi hawafi kwa njaa, Serikali iliagiza tani 42,000 za mahindi kutoka nchi za nje kwa gharama ya Shilingi bilioni 13.69. Mahindi hayo, yameingia nchini na yanaendelea kusambazwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilitoa msamaha wa kodi ya forodha kwenye mahindi kutoka nje ili kuwahamasisha wafanyabiashara kuagiza mahindi. Hadi tarehe 30 Aprili, 2006, jumla ya tani 134,575.8 za mahindi zimeingizwa nchini kwa utaratibu huo. Serikali ilipunguza ushuru wa forodha kwenye mchele unaoagizwa kutoka nje ya nchi kutoka asilimia 75 hadi asilimia 25 ili kuwahamasisha wafanyabiashara kuagiza mchele kutoka nje. Hadi tarehe 30 Aprili, 2006, jumla ya tani 27,388 za mchele ziliingizwa nchini chini ya utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Februari, 2006, Serikali iliomba msaada wa tani 100,000 za chakula kutoka kwa nchi na mashirika wahisani. Baadhi ya wahisani waliitikia wito huo na kutoa msaada wa fedha za kununulia chakula kupitia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani. Hadi tarehe 20 Juni 2006, jumla ya tani 19,913 za chakula zilikuwa zimepatikana. Kati ya hizo, tani 8,317 zimekwishawasili nchini na ugawaji umeanza katika Mikoa ya Shinyanga, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro. Nchi zilizotoa msaada huo ni Saudi Arabia US$ 2,000,000, Canada US$ 1,929,824 na Uturuki US$ 200,000, Jamhuri ya Czech US$ 128,821, Australia US$ 1,094,890, Uholanzi na Sweden US$ 3,200,000. Wengine walikuwa watu binafsi marafiki wa *WFP US$* 82,118. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wote hao waliotusaidia. Nawashukuru pia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Watendaji wa Serikali, wananchi na wafanyabiashara walioshiriki katika kufanikisha zoezi la usambazaji wa chakula nchini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini katika msimu wa kilimo wa 2005/2006. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonyesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 10.73 zikiwemo tani milioni 5.19 za mazao ya nafaka na tani milioni 5.54 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2006/2007 yamekisiwa kufikia tani milioni 9.73. Kwa hiyo, inatarajiwa kuwa Taifa litajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 110. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tathmini hiyo imeonyesha kwamba Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Mara na Kigoma itajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada na haitakuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula. Mikoa ya Tanga, Mbeya, Lindi, Kagera, Morogoro, Iringa na Manyara itakuwa na ziada lakini itakuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula. Mikoa ya Pwani, Kilimanjaro, Tabora na Arusha itajitosheleza kwa chakula lakini itakuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula. Mikoa ya Shinyanga, Dodoma, Singida, Mwanza na Dar es Salaam itakuwa na upungufu wa chakula kwa viwango tofauti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya tathmini hiyo, Taifa kwa ujumla litajitosheleza kwa chakula. Hata hivyo, yatakuwepo maeneo yatakayokuwa na upungufu wa chakula. Hivyo, changamoto kubwa ni namna ya kusambaza chakula kutoka maeneo yenye ziada ya chakula kwenda kwenye maeneo yenye upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- Imeagiza tani 30,000 kutoka nje ya nchi ili kuwezesha SGR kuwa na akiba ya kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza;

- Imepanga kununua tani 80,000 za mahindi na mtama kutoka katika Mikoayenye ziada ya chakula;
- Kuwahimiza wananchi waliopata mavuno mazuri ya chakula katika msimu wa 2005/2006 kuhakikisha wanajiwekea akiba ya chakula ya kutosheleza angalau mahitaji ya kaya hadi kufikia mavuno ya msimu wa 2006/2007. Wananchi wanashauriwa kuuza ziada tu;

- Kuwahimiza wafanyabiashara kununua chakula kutoka kwenye maeneo yenye ziada na kukiuza kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula kwanza kabla ya kufikiria kukiuza nje ya nchi;

- Kuwahimiza wananchi wanaotegemea mifugo kwa ajili ya kipato chao, kuuza baadhi ya mifugo wakati huu ambapo ina hali nzuri na bei ziko juu ili wajinunulie na kuhifadhi chakula cha kutosha mahitaji yao hadi msimu ujao;

- Kuwahamasisha wananchi wengine wanaotegemea kipato kutokana na shughuli zingine ambazo si za kilimo cha mazao ya chakula kununua chakula cha kutosha mahitaji yao wakati wa kipindi cha mavuno ambapo bei za vyakula zinakuwa nafuu; na

- Kufanya tathmini ya kina kwa kushirikian na Halmashauri za Wilaya na wadau wengine katika maeneo yenye upungufu wa chakula mwezi Julai 2006. Lengo ni kubaini kaya zenye upungufu wa chakula na hatua za kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) ya Aprili, 2006 kuhusu matarajio ya uzalishaji wa mazao ya chakula Duniani inaonyesha kwamba nchi nyingi za Kusini mwa Afrika zikiwemo: Malawi, Zambia, Zimbabwe, Botswana, Namibia na Msumbiji zilipata mvua za kutosha na zinatarajia kupata mavuno mazuri ya nafaka. Nchi za Afrika ya Kusini na Angola zinatarajiwa kupata mavuno pungufu ikilinganishwa na mwaka 2005. Uzalishaji wa mahindi katika nchi ya Afrika ya Kusini unatarajiwa kushuka kutokana na kushuka kwa bei ya zao hilo na kuwepo kwa akiba kubwa ya mahindi ya miaka ya nyuma. Afrika ya Kusini ina akiba ya mahindi ya tani milioni 4.5. Uzalishaji katika nchi ya Angola umeathirika kutokana na kipindi kirefu cha ukame katika maeneo ya Kusini Magharibi ambayo ni maarufu kwa kuzalisha nafaka. Nchi za Kenya, Somalia na Djibouti pamoja na kupata mvua nzuri katika baadhi ya maeneo, zitaendelea kuwa na upungufu wa chakula katika mwaka 2006/2007 kutokana na athari za ukame wa muda mrefu. Nchi ya Uganda itakuwa na hali nzuri ya chakula isipokuwa maeneo ya Kaskazini mwa nchi hiyo. Upandaji wa

mazao ya chakula katika nchi za Burundi na Rwanda ulichelewa kuanza kutokana na kuchelewa kuanza mvua kunyesha. Hali hiyo inaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula. Pamoja na mvua nzuri kunyesha katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (*DRC*), hali ya chakula inaweza kuendelea kuwa mbaya kwa sababu ya vita za wenyewe kwa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upungufu wa chakula katika nchi jirani unaweza kuathiri upatikanaji wa chakula nchini kutokana na biashara za vyakula mipakani. Biashara ya vyakula hufanyika sana katika mipaka ya Tanzania na Kenya, Malawi, Zambia, Rwanda Burundi na Kongo. Kutokana na hali nzuri ya chakula katika nchi za Malawi na Zambia, hali ya chakula katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaweza isiathirike sana. Hata hivyo, upatikanaji wa chakula katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Mara unaweza kuathirika kutokana na biashara ya mipakani hasa katika mpaka wa Tanzania na Kenya. Hivyo Wizara yangu itashirikiana na Mikoahusika kuhamasisha wananchi kuhifadhi chakula cha kutosheleza mahitaji ya kaya zao ya mwaka mzima. Aidha, Serikali itawahamasisha wafanyabiashara kupeleka kwanza vyakula kwenye Mikoayenye upungufu kabla ya kuuza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazao makuu ya biashara ambayo huzalishwa nchini ni pamoja na; pamba, korosho, kahawa, chai, sukari, tumbaku, pareto na mkonge. Uzalishaji wa mazao hayo umeonyesha kupanda isipokuwa mazao ya kahawa na chai ambayo uzalishaji wake uliathiriwa na ukame. Kati ya mazao hayo, zao la pamba liliongoza kwa kuliingizia Taifa fedha za kigeni likifuatiwa na tumbaku, kahawa, korosho, chai, sukari, mkonge na pareto. Uzalishaji wa mazao ya biashara nchini katika mwaka 2005/2006 kwa kulinganisha na mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na kuyumba kwa bei za mazao ya asili ya biashara katika soko la Dunia, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imeanza kuhimiza kilimo cha mazao yenye thamani kubwa na soko la uhakika kama vile; vanilla, paprika, maua, pilipili, iliki, mananasi, mapesheni, vitunguu, *Jatropha* na *Artemizia*. Suala la kuongeza tija na uzalishaji kwa kuzingatia ubora vinapewa umuhimu mkubwa kwa kuwa mazao yenye ubora wa juu yana bei nzuri na uhakika wa soko. Ili kuinua tija na kuzalisha mazao yenye ubora unaotakiwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi, Wizara imeandaa mpango wa kuwapatia wakulima mbegu na vipando bora na mafunzo kuhusu uzalishaji wa mazao hayo. Mbinu itakayotumika kuendeleza mazao hayo ni pamoja na kilimo cha mkataba (*Contract Farming*) ambacho kinawahakikishia wakulima pembejeo na soko la mazao watakayozalisha na kuwapatia mafunzo ya kanuni bora za uzalishaji na matumizi sahihi ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 727,120,000 kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali hususan kodi za ukaguzi wa mazao. Hadi kufikia tarehe 20 Juni 2006, kiasi cha Shilingi 798,362,279.11 sawa na asilimia 109.8 ya makadirio zilikusanywa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006 Wizara yangu ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 134.89. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 71.4 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 63.49 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za

miradi ya maendeleo, Shilingi bilioni 7.44 zilikuwa fedha za ndani na Shilingi bilioni 56.05 zilikuwa fedha za nje. Hadi tarehe 25 Juni 2006, Wizara ilipokea Shilingi 68,130,959,591.42 za matumizi ya kawaida, ambazo ni sawa na asilimia 95.4 ya kiasi kilichoidhinishwa. Hadi tarehe 25 Juni 2006 matumizi ya kawaida yalifikia Shilingi 68,125,775,586.61 sawa na asilimia 99.99 ya kiasi kilichotolewa.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 15 Juni 2006, Shilingi 7,440,000,000 fedha za ndani zilikuwa zimetumika, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, Shilingi 22,661,521,445.28 fedha za nje, sawa na asilimia 40 ya fedha za nje zimetumika kugharamia miradi. Matumizi haya madogo yanatokana na kutokuanza kutekelezwa kwa miradi ya *DASIP* (Shilingi 4,000,000,000) na Programu ya Kuendeleza Huduma za Kilimo yaani *Agricultural Services Support Programme (ASSP*) Shilingi 27,919,600,000 ambazo sasa zitaanza kutekelezwa mwaka 2006/2007. Aidha, Programu ya ASSP sasa imejumuishwa ndani ya Mfuko wa Pamoja wa *ASDP* (*ASDP Basket Fund*). Utekelezaji kupitia Idara za Wizara ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango. Mambo muhimu yaliyotekelezwa na Idara ya Sera na Mipango ni yafuatayo:-

Kukamilisha maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* kwa kuzingatia Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa 2005

Mheshimiwa Spika, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2006, Wizara yangu ikishirikiana na Wizara nyingine za Sekta ya Kilimo na kwa kuzingatia Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa 2005 na maelekezo ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara, imekamilisha kuandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programe ASDP*) ya miaka saba (2006/2007-2012/2013) ambayo ilianza kuandaliwa mwaka wa 2002. Kwa hiyo, Programu hii kama ilivyo sasa ni ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005. Aidha, Idara iliratibu maandalizi na uzinduzi wa Mradi wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo Wilayani yaani *District Agricultural Sector Investment Project (DASIP)* na kuratibu Mipango na Bajeti ya Wizara.

Kuhusu ubinafsishaji wa Mashamba na Mashirika ya Kilimo. Katika kipindi cha mwaka wa 2005/2006, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine ilibinafsisha mashamba ya mpunga ya Mbarali na Kapunga na ya ngano ya West Kilimanjaro.Kuhusu kurekebisha na kuhuisha sheria. Katika mwaka wa 2005/2006, Wizara imeendelea kurekebisha na kuhuisha sheria kwa lengo la kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo. Kazi kubwa zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa mapendekezo ya mfumo wa sheria ya Mbolea na Kanuni za sheria za mbegu, Haki Miliki za Uzalishaji wa Mbegu na Mimea Mipya na kufanya mapitio ya Sheria ya Afya ya Mimea na ile ya Taasisi ya *TPRI*. *(Makofi)*

Idara ya Utafiti, katika mwaka 2005/2006, utafiti wa mazao ya kilimo uliendelea kwa lengo la kupata mbegu zenye sifa za kutoa mavuno mengi kwa eneo, kuvumilia magonjwa, ukame, na kukomaa mapema. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni utoaji wa mbegu bora za ufuta (Lindi 02), ngano (Riziki C1) na maharage (Selian 05). Aidha,

vituo vya utafiti vilizalisha mbegu za mama *(breeder seed)* za mazao ya mpunga (tani 7.9), mahindi (tani 8.2), maharage (tani 63), viazi mviringo (tani 40,000), pamba (tani 8), muhogo (vipando 2,684,000), viazi vitamu-vipando (894,800), pareto (vipando 21,961) na korosho (miche 31,500 na vikonyo 55,960). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wanafunzi 559 walijiunga na mafunzo ya muda mrefu ngazi ya stashahada ya kilimo kwa kulipiwa na Serikali. Aidha, wanafunzi wengine 345 walisomea astashahada ya kilimo kwa utaratibu wa kujigharamia. Aidha, Wanafunzi 240 wa stashahada ya kilimo na 263 wa astashahada ya kilimo walihitimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ilikamilisha skimu 63 zenye hekta 14,396 na kuongeza eneo la umwagiliaji kuwa hekta 264,388. Kazi za ugani mwaka jana ni pamoja na mafunzo kwa wakulima katika mashamba darasa darasa katika wilaya 20, aidha vipindi 52 vya redio vya mkulima wa kisasa vilitangazwa na machapisho nane ya majarida yalitolewa kwa wakulima na sekta binafsi ilishirikishwa katika utoaji wa huduma za ugani.

Husishi ya Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji *(PIDP)* (hekta 2,804); Miradi inayogharimiwa na Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula (hekta 1,250) na Mipango ya Wilaya ya Maendeleo ya Kilimo (*DADPs* (hekta 4,377). Aidha, Wizara kwa kupitia Kanda za Umwagiliaji imeendeleza skimu 18 zenye eneo la hekta 5,227 na kujenga mabwawa 6 yenye uwezo wa kumwagilia hekta 738. Skimu nyingine 29 zenye jumla ya hekta 3,604 ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iliendelea kuhimiza na kusimamia uanzishaji wa mashamba ya mfano katika maeneo yanayozunguka Ziwa Viktoria kwa lengo la kutengeneza ukanda wa kijani wa mazao ya kilimo (*Green Belt*). Mashamba ya mfano yanayosimamiwa na vikundi 10 yenye jumla ya hekta 36 yalianzishwa.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Matumizi Bora ya Ardhikatika mwaka 2005/2006, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo ili kuchangia katika juhudi za Taifa za kuongeza uzalishaji wa kilimo na kukabiliana na madhara yatokanayo na mmomonyoko wa udongo mashambani ambao huchangia katika tatizo la uharibifu wa mazingira. Kazi muhimu zilizotekelezwa ni pamoja na kupima mashamba, kutoa ushauri wa kilimo mseto na matuta, kuchora ramani, kuanzisha mashamba ya mfano ya mbinu za kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kutoa mafunzo kwa wataalam.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Zana Bora za Kilimo. kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2005/06 ni pamoja na kuendeleza kilimo cha zana bora za kilimo kwa kutekeleza kazi zifuatazo: kutoa ushauri wa kitaalam, kuhamasisha wafanyabiashara na vikundi vya wakulima kunzisha vituo vya zana za kilimo, kuwapatia mafunzo wataalam wa zana za kilimo. Aidha, jumla ya vituo 30 vya maksai vilifanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kueneza mbinu ya Shamba Darasa (*Farmer Field Schools-FFS)* katika Halmashauri za Wilaya 20, kutayarisha na kutangaza vipindi vya redio vya Ukulima wa Kisasa, kuandaa na kusambaza machapisho na majarida kwa wakulima na kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ugani. Kazi nyingine zilihusu utoaji wa mafunzo ya rejea kwa wataalam wa huduma za ugani na kusimamia viwango vya utoaji wa huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na wakulima ilipambana na milipuko ya visumbufu mbalimbali vya mimea na mazao ikiwa ni pamoja na kwelea kwelea, nzige, viwavijeshi, panya na magonjwa mbalimbali ya mimea. Wizara iliendelea kuhamasisha wakulima kutumia mbinu ya Udhibiti Husishi *(IPM).* Aidha*,* Wizara ilifanya ukaguzi wa mazao yanayoingia nchini na yanayotoka nje ya nchi, ili kudhibiti uingizaji wa viuatilifu. Kazi nyingine muhimu ilikuwa ni kuendelea na juhudi za kudhibiti magugu maji katika Ziwa Viktoria, kudhibiti magonjwa ya mnyauko fusari wa mibuni na mnyauko wa migomba mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 kazi muhimu zilizotekelezwa ni pamoja na kuzalisha kwa wingi vipando na mbegu bora za mazao ya muhogo, soya, mahindi lishe, miche ya matunda, viungo na kuhamasisha kilimo cha mkataba katika mazao ya mboga na matunda na viungo. Aidha, Wizara iliwahamasisha wakulima wa mboga, matunda na maua kuweka mfumo wa kitaasisi utakaowawezesha kuwa na mipango ya pamoja ya uzalishaji, usindikaji na masoko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara iliendelea na utekelezaji wa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project-PADEP),* Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Programme Support)* na Programu Maalumu ya Usalama wa Chakula (*Special Program for Food Security).* Miradi hiyo ilitoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa malengo ya Wizara katika kuimarisha huduma za ugani, uzalishaji wa mbegu kwa kuwatumia wakulima, uundaji na usimamizi wa vikundi vya wakulima, kuwawezesha wakulima kupata mikopo na kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalam wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuwahamasisha wafanyabiashara wa pembejeo, hususan mbolea na viuatilifu kuagiza na kuingiza nchini pembejeo hizo kulingana na mahitaji ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, kama mbolea ingepatikana kwa wakati na kwa bei nafuu matumizi ya mbolea nchini yangeweza kufikia tani 385,000. Hadi kufikia mwezi Juni 2006, jumla ya tani 241,753 za mbolea ikijumuisha mbolea za ruzuku zilipatikana. Mbolea hizo ni pamoja na *DAP* (tani 18,152); *UREA* (tani 118,976); CAN (tani 28,134); *TSP* (tani 13,283); NPK 20:10:10 (tani 9,077); *NPK* 25:5:5 (tani 5,980); *NPK* 10:18:24 (tani 48,740); *SA* (tani 7,585) na *MRP* (tani 150). Kati ya hizo, jumla ya tani 121,000 za mbolea zilinunuliwa na wakulima kati ya hizo, mbolea iliyouzwa chini ya utaratibu wa ruzuku ilikuwa tani 51,629.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia jumla ya tani 10,477 za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta. Kati ya hizo, tani 1,452 zilizalishwa na Mashamba ya Serikali ya Mbegu za Msingi *(Foundantion Seed Farms),* makampuni binafsi yalizalisha tani 3,528 hapa nchini na tani 5,220 ziliagizwa kutoka nje. Aidha, Wizara iliendelea kudhibiti ubora wa mbegu zinazozalishwa na kuingizwa nchini kupitia Taasisi ya Serikali ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(Tanzania Official Seed Certification Institute (TOSCI).*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wwa Pembejeo. Katika mwaka wa 2005/2006, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulipewa shillingi 2,921,426,610 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo na zana za kilimo, wakulima binafsi, vikundi vya wakulima (*SACCOS*) na Mifuko ya Pembejeo ya Halmashauri mbali mbali kwa ajili ya kununua na kusambaza pembejeo za kilimo na mifugo, zana za kilimo, kukarabati matrekta mabovu na kununua matrekta mapya. Mikopo ilitozwa riba ya asilimia 8 ikilinganishwa na wastani wa riba ya asilimia 15 inayotozwa na mabenki. Kuanzia Julai 2005 hadi tarehe 10 Mei, 2006 jumla ya fedha zilizotumika kwa kutoa mikopo ni Shilingi 5,745,510,720.00. Kiasi hicho, kinajumuisha marejesho ya mikopo ya miaka iliyopita. Hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa dhidi ya wadaiwa sugu ili kuhimiza urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Idara Ya Usalama Wa Chakula. Kazi muhimu zilizotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2005/2006 ni pamoja na kuboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu na taarifa za chakula nchini ambapo, mafunzo ya ufuatiliaji wa hali ya mazao mashambani na hali ya chakula yalitolewa kwa wataalam wa ugani katika Halmashauri za Wilaya na Miji katika Mikoa yote. Kazi nyingine zilihusu ukusanyaji wa takwimu na taarifa ya hali ya mvua na mazao mashambani na kufanya tathmini za uzalishaji wa mazao ya chakula na mwenendo wa hali ya chakula nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya chakula na Usindikaji katika mwaka 2005/2006, Wizara iliendesha kampeni ya ukadiriaji na hifadhi ya chakula cha kutosha mahitaji ya kaya katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Morogoro, Ruvuma, Pwani, Kagera, Kigoma, Mtwara, Lindi na Tanga. Aidha, teknolojia za hifadhi, usindikaji na elimu ya lishe kwa mazao ya mtama, muhogo, viazi, mboga na matunda ilitolewa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa (Sgr). Katika mwaka 2005/2006, Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilianza na akiba ya tani 112,712.4 za mahindi na pia ilinunua tani 1,773.8 za mahindi zenye thamani ya Shilingi milioni 316.7. Hii ni sawa na asilimia 4.0 ya lengo la kununua tani 44,000. Lengo halikufikiwa kutokana na ukame ulioikumba sehemu kubwa ya nchi. Kutokana na upungufu huo, Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa ilinunua tani 81,156.9 kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa na tani 42,000 kutoka nje ya nchi ili kutosheleza mahitaji ya wananchi waliokumbwa na upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maendeleo ya Ushirika. Katika mwaka 2005/2006, kazi muhimu iliyofanyika ilihusu utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na

Modenaizesheni ya Ushirika nchini (*Cooperative Reform and Modernization Program (CRMP*) ambayo ilianza kutekelezwa rasmi mwezi Januari, 2005. Lengo kuu la Programu hiyo ni kuwawezesha wanachama kuibua Ushirika unaoendeshwa kibiashara, wenye nguvu za kiuchumi na uwezo wa kuhimili ushindani katika soko huru. Programu hii ni sehemu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* na imelenga kutekeleza malengo ya MKUKUTA kupitia sekta ndogo ya Ushirika. Programu hiyo imewezesha kuimarisha uongozi wa vyama vya ushirika kwa kusimamia chaguzi za viongozi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi na Vyama Vikuu 2,074 kati ya vyama 2,551 vyenye sifa ya kufanya uchaguzi katika Mikoatisa ya Tanzania Bara. Aidha, Maafisa Ushirika 200 wa Mikoa na Wilaya wamepewa semina maalum ili kuwawezesha kusimamia vizuri uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuimarisha uongozi, mafanikio katika Ushirika yamejitokeza kwenye ongezeko la vyama vya ushirika na wanachama. Kwa mfano, idadi ya *SACCOS* na wanachama wa vyama hivyo imekuwa ikiongezeka kwa kasi. Idadi ya wanachama iliongezeka kutoka 254,651 mwezi Mei, 2005 hadi 291,368 mwezi Mei, 2006. Aidha, Mikopo iliyokuwa imetolewa na *SACCOS* hadi Mei, 2005 imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 54.1 hadi Shilingi bilioni 65.7 mwezi Mei 2006. Mikopo hiyo hutolewa kwa ajili ya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, biashara, ujenzi wa nyumba, elimu na tiba.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi katika mwaka 2005/2006, Wizara iliendelea kutekeleza zoezi la kuwapandisha watumishi cheo, kurekebisha ajira za watumishi kwa kuwaajiri katika masharti sahihi na kuwathibitisha kazini pamoja na kuajiri watumishi wapya. Watumishi waliopandishwa cheo ni 260 na walioajiriwa ni 131. Kazi nyingine zilihusu kutoa mafunzo ya mabadiliko yanayoendelea katika utumishi wa umma, namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* umeanza hatua kwa hatua kwa kuzingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Programu (*ASDP Framework and Process Document*). Tangu mwaka 2002/2003, fedha zimekuwa zinapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani *(DADPs)* kama sehemu ya utekelezaji wa *ASDP*.

Wakati huo huo maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo yalikuwa yanaendelea na yamekamilika mwanzoni mwa 2006. Wizara za Sekta ya Kilimo, ambazo ni Kilimo Chakula na Ushirika, Maendeleo ya Mifugo, Viwanda Biashara na Masoko na Tawala za Mikoana Serikali za Mitaa, zimeweka utaratibu wa kugharamia utekelezaji wa Mpango huu kupitia Kapu la Mfuko wa *ASDP* (*ASDP Basket Fund)*.

Mheshimiwa Spika, Programu hii imekadiriwa kugharimu Shilingi trilioni 2 na bilioni 500 katika kipindi cha miaka saba kuanzia mwaka 2006/2007. Programu hii ni ya aina yake ambayo itatekelezwa katika Mikoana Wilaya zote pamoja na Wizara nne za Sekta ya Kilimo kwenye ngazi ya Taifa. Aidha, zaidi ya asilimia 75 ya utekelezaji wa Programu utakuwa kwenye ngazi ya Wilaya na katika Wilaya hizo, zaidi ya asilimia 75

ya matumizi yatalenga kwenye miradi ya kilimo cha umwagiliaji. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Programu imetengewa Shilingi bilioni 45.67 ambazo kati yake Shilingi bilioni 33.17 ni za wahisani na Shilingi bilioni 12.5 ni za Serikali.

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya *ASDP* ni yafuatayo:-

- Kuongeza tija, mavuno na mapato ya wakulima zaidi ya maradufu;

- Kuwawezesha wakulima kupata mafunzo na teknolojia za kilimo;

- Kuwa na uhakika wa masoko na miundombinu ambavyo pia huchangia kuongeza tija, mapato na faida katika kilimo;

- Kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) miongoni mwa wakulima na wafugaji;

- Kuongeza kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 264,388 za sasa hadi hekta 1,000,000 ifikapo 2010; na

- Kuvutia uwekezaji katika sekta binafsi kwa kuboresha Sheria, Sera na Kanuni.

Mheshimiwa Spika, gharama za Programu katika ngazi ya Wilaya na Taifa kwa miaka saba zitakuwa kama ifuatavyo: Gharama za Utekelezaji katika Ngazi ya Wilaya na Vijiji – Jumla ni Shilingi bilioni 1,876 sawa na asilimia 75 ya Bajeti ya programu:-

- Uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji maji mashambani Shilingi bilioni 1,493 sawa na asilimia 80 ya fedha zitakazopelekwa Wilayani.

- Miradi ya Kuendeleza Kilimo Shilingi bilioni 135.795 sawa na asilimia 7.24 ya fedha zitakazopelekwa Wilayani.

- Uboreshaji wa Huduma za Kilimo Shilingi bilioni 189.63 sawa na asilimia 10.11 ya fedha zitakazopelekwa Wilayani.

- Kujenga Uwezo wa Utekelezaji wa Mipango kwa Watendaji na Wakulima na Kuboresha Mifumo ya Utendaji Shilingi bilioni 29.342 sawa na asilimia 2 ya fedha zitakazopelekwa Wilayani.

- Kuendesha mafunzo ya wakulima na wafugaji na watumishi katika ngazi ya Wilaya Shilingi bilioni 15.794 sawa na asilimia 0.84 ya fedha zitakazopelekwa Wilayani.

Gharama za Utekelezaji katika Ngazi ya Taifa – Jumla ni Shilingi bilioni 615.9 sawa na asilimia 25 ya bajeti ya Programu.

- Kuboresha huduma za ugani na utafiti Shilingi bilioni 104.21 sawa na asilimia 16.92 ya fedha zitakazobaki ngazi ya Taifa;

• Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji Shilingi bilioni 474 sawa na asilimia 76.97 ya fedha zitakazobaki ngazi ya Taifa;

• Kuendeleza masoko na sekta binafsi Shilingi bilioni 11.4 sawa na asilimia 1.84 ya fedha zitakazobaki ngazi ya Taifa;

• Uhakika wa Upatikanaji wa Chakula Shilingi bilioni 5.3 sawa na asilimia 0.86 ya fedha zitakazobaki ngazi ya Taifa; na

• Kuratibu, kufuatilia na kutathmini shughuli za Programu Shilingi bilioni 17.9 sawa na asilimia 2.91 ya fedha zitakazobaki ngazi ya Taifa.

Maelezo ya kina ya makadirio ya gharama ya Programu kwa kipindi cha miaka saba yameonyeshwa kwenye.

Mheshimiwa Spika, Wizara za Sekta ya Kilimo zimeboresha Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na kuutuma kwenye Wilaya zote. Utaratibu wa kuwajengea uwezo wataalam wa Halmashauri za Wilaya wa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya umeandaliwa na mafunzo hayo yatatolewa katika mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Miongozo mingine inayohusu namna ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, uimarishaji wa masoko, ushirikishwaji wa sekta binafsi na uhakika wa upatikanaji wa chakula itatayarishwa katika mwaka 2006/2007. Aidha, Waheshimiwa wabunge wote watafanyiwa semina maalum ya kuwaelielimisha zaidi juu ya *ASDP*.

Mheshimiwa Spika, Programu hii ndiyo itakayotafsiri kwa vitendo utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Strategy (ASDS*) pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) katika Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Katika mwaka wa kwanza, Programu imeweka mkazo mkubwa katika kujenga uwezo wa Wilaya kutayarisha na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans- DADPs*) pamoja na kujenga uwezo wa watendaji katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Vijiji ili kuwahudumia wakulima kwa ufanisi zaidi. Maeneo mengine yanayosisitizwa ni kuboresha huduma za ugani, utafiti na mafunzo ya kilimo ambayo ni majukumu muhimu ya Wizara husika za Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, pamoja na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Shilingi bilioni 15.3 zimetengwa kwa ajili ya miradi inayoendelea ambayo pia inachangia katika kutekeleza programu hii, kama ifuatavyo:-

• Mradi Shirikishi wa Kuendeleza Kilimo na Uwezeshaji *(PADEP)* kwa ushiriki wa Benki ya Dunia unatekelezwa katika Mikoa14 na Wilaya 31, Shilingi bilioni 9.5;

- Mradi wa Kuimarisha Kilimo *(ASPS)* kwa ushiriki wa *DANIDA* katika Mikoa ya Iringa na Mbeya, Shilingi bilioni 2.3; na

- Mradi wa Kuimarisha Uwekezaji Wilayani *(DASIP)* unaotekelezwa kwa ushiriki wa *ADB* katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera na Kigoma, Shilingi bilioni 3.5. Aidha, maandalizi ya aina hii yanaendelea kwa Mikoa ya Tabora, Rukwa, Singida, Dodoma na Wilaya mbili za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni hatua muhimu ya kutekeleza dhana ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*decentralization by devolution*). Aidha, ni changamoto kubwa kwa Wilaya kuibua Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* kwa kutumia mbinu shirikishi pamoja na kuwajibika kwa usimamizi wa fedha. Ni muhimu sana viongozi na watendaji katika Mikoana Wilaya kuelewa vizuri mantiki ya Programu hii. Fedha za kutoka Kapu la Mfuko wa *ASDP (ASDP Basket Fund)* zitapatikana kwa kuibua Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na si vinginevyo.

Kwa hiyo, ni muhimu sana kwa kila Wilaya kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ulioibuliwa kwa utaratibu shirikishi kutoka miongoni mwa wakulima Vijijini. Serikali inao wajibu wa kuhakikisha uibuaji wa Mipango hiyo unafanyika. Hivyo, Wizara itakuwa macho kufuatilia na kuzisaidia Halmashauri kufanikisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, ili kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Programu kwa ufanisi, uwezo wa watendaji wa Wizara za Sekta ya Kilimo kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa utajengwa katika kuandaa mipango, kutekeleza na kuandaa taarifa za utekelezaji. Aidha, Wizara za Sekta ya Kilimo zitatayarisha mfumo ambao utatumika kukusanya takwimu na kuandaa taarifa za utekelezaji na matokeo ya Programu kulingana na malengo yaliyowekwa. Vilevile, Mfumo wa utoaji taarifa unaotumiwa na Serikali za Mitaa utaboreshwa ili kuwa na mfumo mmoja utakaokubalika kutoa taarifa za utekelezaji wa Programu kuanzia ngazi ya Vijiji hadi Taifa.

Mheshimiwa Spika, Programu itajenga uwezo wa watendaji wa Mikoaili isaidie kutoa utaalamu kwa Wilaya katika maeneo ya uandaaji wa mipango, ufuatiliaji, usimamizi, tathmini ya matokeo na uandaaji wa taarifa za utekelezaji. Aidha, vigezo vitakavyotumika kupima ubora wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani vitawekwa. Mapitio ya utekelezaji yatakuwa yanafanyika kila baada ya muda maalum ili kuifanyia marekebisho Programu pindi itakapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Januari 2006, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika alisisitiza wajibu wa Wizara katika kutekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 ambapo alitoa maagizo na maelekezo yafuatayo:-

- Kutayarisha mkakati na mipango itakayowezesha kubadilisha kilimo kuwa cha kisasa, chenye tija na kitakacho waletea wananchi maendeleo;

- Kuhakikisha wakulima wanapata na kutumia zana bora, pembejeo za kilimo hususan mbolea, mbegu bora na madawa ya kudhibiti visumbufu. Aidha, aliagiza kuwa na wakulima wenye ujuzi (*skilled farmers*) na kuhakikisha upatikanani wa masoko ya uhakika;
- Kuhakikisha kuwa wakati wote wananchi hawafi kwa njaa; na

- Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia kila chanzo cha maji kinachowezekana – mito, maziwa, mabwawa, visima na maji ya mvua.

Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambao utaanza mwaka 2006/2007 ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchanguzi Mkuu wa Mwaka 2005, na maagizo ya Mheshimiwa Rais. Aidha, maagizo mengine yamezingatiwa katika bajeti hii kama ifuatavyo:-

(b) Kuhakikisha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Ruzuku ya mbolea, mbegu na madawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mbolea katika kuendeleza kilimo, ruzuku ya mbolea imeongezwa kutoka Shilingi bilioni 7.5 mwaka 2005/2006, hadi Shilingi bilioni 21. Lengo kuu la Serikali katika kutoa ruzuku ya mbolea ni kuhakikisha kuwa matumizi ya mbolea yanaongezeka ili kuongeza tija, mavuno na mapato ya wakulima. Inakadiriwa kwamba upatikanaji wa mbolea yenye ruzuku utaongezeka mara dufu kutoka tani 63,000 mwaka 2005/2006 hadi tani 129,000 mwaka 2006/2007. Aidha, tani 3,000 za mbegu bora na madawa ya korosho yatapatiwa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa kutoa ruzuku ya mbolea umekumbwa na matatizo mengi ya kiutekelezaji ambayo inabidi yapatiwe ufumbuzi wa haraka. Matatizo haya yanatokana na usimamizi dhaifu, uteuzi wa waagizaji na mawakala wa mbolea wasio na uwezo na wasio waaminifu na kutokuwepo kwa utaratibu wa wazi wa kutenganisha mbolea yenye ruzuku na isiyo na ruzuku. Katika mwaka 2006/07, hatua madhubuti zitachukuliwa kudhibiti hali hii kama ifuatavyo:-

- Kuweka vigezo vya wazi na imara vya kuteua wasambazaji na mawakala wa mbolea;
- Kuwataka mawakala kusaini mikataba na Halmashauri husika;

- Kila Kijiji kutoa orodha ya wakulima kwa wakala wa mbolea *(stockist)* ambayo ndiyo itakayotumika kuwauzia wakulima mbolea yenye ruzuku;

- Kutangaza bei za mbolea kwenye ngazi za Mikoa, Wilaya na maduka ya mawakala;

- Kutumia mifuko maalum kwa mbolea ya ruzuku; na

- Kuimarisha kamati za Mikoana Wilaya katika kusimamia na kufuatilia upatikanaji wa mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na watendaji wote kwenye ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya wanatakiwa kutoa kipaumbele cha pekee katika kusimamia mbolea ya ruzuku ili kuhakikisha hakuna hata mfuko mmoja wa mbolea utakaopotea. Kuhakikisha Upatikanaji na Utumiaji wa Mbegu Bora.

Mheshimiwa Spika, Wizara itahakikisha matumizi ya mbegu bora za mazao muhimu yanayozalishwa nchini yanaongezeka kutoka wastani wa tani 10,500 za sasa hadi tani 30,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2010 kwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kuhakikisha Wakala wa Serikali wa Mbegu za Mazao *(Agricultural Seed Agency)* unatekeleza mpango mzuri wa uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora;

- Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji na uagizaji wa mbegu bora;

- Kuhamasisha wakulima kujizalishia mbegu za ubora unaotambulika *(Quality Declared Seed)*; na
- Kuimarisha uwezo wa Taasisi ya Ukaguzi na Udhibiti wa Ubora wa Mbegu *(TOSCI)* wa kusimamia Sheria na Kanuni za udhibiti wa ubora wa mbegu ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu zenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Juni, 2006 kulifanyika mkutano maalumu wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu mbolea (*Africa Fertilizer Summit – African Union Special Summit of the Heads of State and Government*) huko Abuja, Nigeria. Mimi nilipata heshima kubwa na ya pekee kumwakilisha Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika mkutano huu, ambao ulikuwa na mafanikio makubwa kwa kukubaliana nchi wanachama kutekeleza yafuatayo:-

- Kuanzisha mawakala wa pembejeo za kilimo (*agro-dealers/rural stockists*) Vijijini ifikapo Juni 2007;

- Kuanzisha dhamana ya Kitaifa kwa mikopo ya pembejeo za kilimo (*National Agricultural Input Credit Guarantee Facilities*);

- Kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wasio na uwezo (*smart subsidies for the poor and vulnerable*);

- Kuanzisha mtandao wa kikanda wa kununua na kusambaza mbolea, usio na vikwazo vya kibiashara na kuhimiza uzalishaji wa mbolea kitaifa na kikanda; na

- Kuanzisha mfumo wa kugharimia maendeleo ya utumiaji wa mbolea Afrika (*Africa Fertilizer Development Financing Mechanism*).

Mheshimiwa Spika, aidha, mkutano huu ulitoa Tamko la Abuja kuhusu Mapinduzi ya Kijani ya Afrika (*Abuja Declaration on the Africa Green Revolution*) ambalo pamoja na mambo mengine, linasisitiza umuhimu wa mbolea za madini na mbegu bora katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Tamko hilo linaelekeza kuongeza

matumizi ya mbolea hizo kutoka wastani wa sasa wa kilo 8 za virutubisho kwa hekta hadi angalau kilo 50 kwa hekta ifikapo mwaka 2015. Iwapo Tanzania itazingatia agizo hilo, inatarajiwa kwamba matumizi ya mbolea nchini yataongezeka kutoka tani 121,000 za sasa hadi tani milioni 1.4 mwaka 2015. Mkutano umezitaka Serikali za Afrika kuchukua hatua madhubuti za kuongeza upatikanaji wa mbolea kwa wakulima. Kaulimbiu ya Mkutano huu ni Rutubisha Udongo, Lisha Bara la Afrika *(Nourish the Soil Feed the Continent)*. Nasi Kaulimbiu yetu tumeamua itakuawa: Rutubisha Udongo Kulisha Taifa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kuongeza bajeti ya ruzuku ya mbolea ni hatua muhimu ya Kutekeleza Tamko la Abuja. Aidha, Serikali inategemea kuanza mazungumzo na waagizaji wa mbolea na wahisani kwa lengo la kuanzisha akiba maalum ya mbolea nchini (*National Fertilizer Buffer Stock*) ili kuhakikisha kuwa kuna mbolea ya kutosha nchini wakati wote na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kupanua Kilimo cha Umwagiliaji. Maji ni pembejeo muhimu sana katika kilimo bora na endelevu. Kwa hiyo, lengo la Wizara yangu ni kufanya Kilimo cha umwagiliaji kuwa ni kitovu cha Kilimo bora nchini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji itasimamia kikamilifu matumizi bora ya maji katika kilimo ili kuhakikisha kuwa watumiaji wote wanajua kuwa maji ni rasilimali muhimu na inatumika kwa njia endelevu ili isiathiri upatikanaji wake.

Lengo la Wizara ni kuendeleza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 264,388 za sasa hadi hekta 1,000,000 ifikapo mwaka wa 2010. Nchi yetu ina eneo la hekta zipatazo milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya hizo, hekta milioni 2.3 zina uwezo mkubwa wa Kilimo cha umwagiliaji *(high irrigation potential)*; hekta milioni 4.8 uwezo wa kati wa kuendelezwa *(medium potential)* na hekta milioni 22.3 uwezo mdogo wa kuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinatuonyesha kuwa nchi yetu ina fursa kubwa ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ambayo hatujaitumia ipasavyo. Kilimo cha umwagiliaji kimekuwa kikikua kwa kasi ndogo kutokana na miradi ya umwagiliaji kuhitaji uchunguzi wa kina ili kuhakikisha ni endelevu na haina athari kwa mazingira na pia inahitaji fedha nyingi ambazo haziwezi kupatikana kwa wakati mmoja. Mikakati ya kutekeleza kilimo cha umwagiliaji imeainishwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambayo utekelezaji wake unaanza mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazotekelezwa na Wizara katika mwaka 2006/2007, ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ni kama ifuatavyo:-

- Usimamizi wa uimarishaji wa miundombinu iliyojengwa katika maeneo ya umwagiliaji: Wizara yangu itahakikisha kwamba maeneo yote yenye miundombinu ya umwagiliaji yanawekewa utaratibu mzuri wa usimamiaji. Kazi hii itafanywa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

- Ujenzi wa Skimu na Mabwawa: skimu 14 za asili zenye eneo la hekta 4,200 zitakarabatiwa. Aidha, mabwawa manne yatakayowezesha hekta 750 kumwagiliwa

yatajengwa katika maeneo yenye ukame. Sambamba na kazi hizo, Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na usanifu wa skimu 63 katika Mabonde ya Mito Wami na Kilombero Mkoani Morogoro ambayo yana maji ya uhakika na rutuba ya kuwezesha hekta 315,000 kuendelezwa.

Aidha, michoro kwa ajili ya kuendeleza maeneo kame ya Mikoa ya Singida, Dodoma, Tabora, Shinyanga na Manyara itatayarishwa kama sehemu ya maandalizi ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika maeneo hayo. Vilevile, michoro hiyo itasaidia kuharakisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji mara fedha zitakapopatikana kutoka vyanzo mbalimbali tunavyoendelea kuvifanyia kazi.

- Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula (*Japan Food Aid Counterpart Fund*). Mfuko huu ambao umeanzishwa kutokana na mapato ya mauzo ya chakula cha msaada kinachotolewa na Serikali ya Japan, unatumika kugharamia miradi midogo midogo inayolenga zaidi katika kuongeza upatikanaji wa chakula nchini. Katika mwaka 2006/2007 skimu nane za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 3,540 zitagharamiwa na Mfuko huu. Skimu hizo ni Uraroni, Rombo (hekta 1,250); Lundo, Mbinga, (hekta 400); Makangaga, Lindi Vijijini (hekta 100); *Mang'ola Prison Farm,* Karatu (hekta 450); Kitere, Mtwara Vijijini (hekta 120); Ulyanyama, Sikonge (hekta 500); Butiama, Musoma Vijijini (hekta 320) na Mbebe, Ileje (hekta 400). Pamoja na kutekeleza miradi hiyo, Wizara kupitia Ofisi zake za Kanda za Umwagiliaji itaendelea kuzisaidia Halmashauri za Wilaya kuandaa maandiko ya kitaalam ya kuombea fedha kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya kutoka kwenye Kapu la Mfuko wa *ASDP (ASDP Basket Fund)*.

- Kujenga Uwezo wa Wataalamu na Wakulima Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji: ili kuwezesha miundo mbinu ya skimu na mabwawa kuwa endelevu, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itasimamia skimu zote za umwagiliaji maji mashambani na mabwawa ili kuhakikisha kwamba malengo ya tija na uzalishaji yaliyowekwa katika skimu hizo yanafikiwa. Utekelezaji utahusisha kutoa mafunzo ya matumizi bora ya maji kwa wakulima na mafunzo kuhusu uendeshaji na usimamizi wa skimu za umwagiliaji maji kwa wafanyakazi wa Halmashauri. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa wakulima yatakayowawezesha kutumia teknolojia za kisasa za uvunaji wa maji ya mvua hususan ujenzi wa matangi ya ardhini ya kuvuna maji (*underground water tanks*), umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip Irrigation*), utumiaji wa maji yaliyoko chini ya ardhi, pampu za miguu na zinazotumia nishati za mafuta au umeme.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Huduma za Kilimo. Bado kuna matatizo mengi yanayokabili huduma za ugani Vijijini. Huduma za ugani ambazo zimehamishiwa kwenye Serikali za Mitaa tangu mwaka 1998 zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalam, vitendea kazi pamoja na usimamizi. Kwa mfano, tathmini iliyofanywa na Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI imebaini kwamba takriban wataalam wa ugani 12,000 wanahitajika nchini lakini waliopo ni 3,833 tu.

Aidha, kuna kero kubwa ya maslahi ya watumishi hasa ya kuchelewa kupandishwa cheo. Katika kuimarisha huduma za ugani, Wizara itaendelea kushirikiana

na Wizara ya TAMISEMI kuangalia upya watumishi wa ugani waliopo pamoja na vitendea kazi kwenye Halmashauri zote kwa lengo la kutambua mahitaji halisi ya watumishi hao pamoja na vitendea kazi wanavyohitaji ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kazi hii ilikuwa ifanyike mwaka 2005/2006 lakini haikuwezekana kutokana na kuchelewa kukamilisha Programu ambayo ndiyo ingegharamia zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wakulima wanapata mafunzo juu ya mbinu za kilimo bora, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kutumia mbinu shirikishi katika kuibua, kupanga na kutekeleza miradi yao ya maendeleo katika Sekta ya kilimo. Utaratibu huu siyo mgeni hapa nchini kwa kuwa umeshatumika katika maeneo mengi hususan katika Mkoa wa Singida, na katika maeneo yanayotekeleza miradi ya kitaifa inayosimamiwa na Wizara. Maeneo hayo yapo katika baadhi ya Wilaya za Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Singida, Manyara, Iringa, Morogoro, Mtwara, Lindi, Tabora, Tanga. Maeneo mengine ni Shinyanga, Kagera na Mwanza. Katika matumizi ya mbinu shirikishi, mkazo utawekwa katika kutumia mbinu ya shamba darasa ambayo imeonyesha mafanikio makubwa katika kuwapatia wakulima mbinu za kilimo bora cha mazao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara imepanga kuimarisha shughuli za uwezeshaji wa wakulima *(farmers empowerment*) ili kuwajengea uwezo wa kushiriki katika kuibua matatizo yanayowakabili na kuandaa mipango ya kuyatatua. Kazi hii itatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP*) ambao unawataka wakulima kujiunga katika vikundi ili kuwapatia mafunzo ya mbinu bora za kilimo na uendeshaji wa vikundi. Aidha, chini ya Programu hiyo, vitaanzishwa Vituo vya Raslimali za Wakulima katika kata *(Ward Agricultural Resource Centers-WARCs)* katika Halmashauri za Wilaya. Vituo hivyo vitawezesha wakulima katika Kata kupata mafunzo ya kilimo bora kwa vitendo kupitia wataalam wa Kata. *(Makofi)*

Katika kuimarisha ujasirimali kwa wakulima, sekta binafsi itahusishwa zaidi katika kutoa huduma hiyo. Lengo ni kuwawezesha wakulima kuanzisha mitandao ya vikundi katika kila ngazi ya utawala (*Farmer forums and farmer group networks*) kwa kutumia uzoefu wa Mtandao wa kitaifa wa Vikundi vya Wakulima yaani MVIWATA.

Mheshimiwa Spika, Kupanua Matumizi ya Zana Bora za Kilimo. Ili kuendeleza matumizi ya zana bora zinazokokotwa na wanyamakazi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendelea kukamilisha ukarabati wa vituo 25 vya wanyamakazi kwenye Mikoa ya Mara, Mwanza, Tabora, Shinyanga, Dodoma, Singida, Morogoro, Manyara, Arusha, Iringa, Mbeya na Rukwa na kuvipatia zana timilifu ili viweze kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima juu ya matumizi ya zana bora. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)* na Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini *(CAMARTEC)* itahakiki ubora wa zana za kilimo ili kuhakikisha wakulima wanapata zana zenye ubora unaokidhi mahitaji ya mazingira ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Kilimo. Ili kuimarisha huduma za utafiti, Wizara itatekeleza mikakati ifuatayo:-

• Itaanzisha Mifuko ya Utafiti ya Kanda *(Zonal Agricultural Research and Development Funds (ZARDEFs)* ambayo itagharamia shughuli za utafiti na ugani kulingana na mahitaji ya wadau. Aidha, shughuli za utafiti zitakazogharamiwa zitakuwa zikichaguliwa kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia mahitaji ya wadau.

• Itaeneza dhana ya usimamizi wa utafiti kulingana na mahitaji ya wateja *(Client Oriented Research Development and Management Approach- CORDEMA)* ili kuhakikisha mahitaji ya wadau hususan wakulima yanazingatiwa katika utoaji wa huduma za utafiti.

• Vituo vya Utafiti wa Kilimo vitaendelea kutoa huduma za utafiti wa mazao, udongo, kilimo mseto, kilimo uhandisi *(agricultural engeneering)* na utafiti wa mifumo ya Kilimo na masuala ya uchumi na sayansi ya jamii na mifumo ya uzalishaji wa mazao *(Farming Systems Research and Socio-Economics).* Kama sehemu ya utekelezaji wa lengo hili, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya aina za mbegu bora za mazao ya jamii ya nafaka, mikunde, na mbegu za mafuta pamoja na mazao ya mizizi ambayo yana tija, uwezo wa kustahimili ukame, visumbufu vya mimea na yanayokidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa na soko la ndani na nje. Aidha, Vituo vya Utafiti vitaendelea kuzalisha na kutunza mbegu mama *(breeders' seeds)* kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wazalishaji wa mbegu bora nchini.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaimarisha huduma ya utabiri wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea na mazao ili kuhakikisha udhibiti unafanyika kabla ya mazao ya wakulima hayajashambuliwa. Ili kuongeza ufanisi katika udhibiti, Wizara itatoa mafunzo kwa wakulima na kupanua matumizi ya mbinu shirikishi katika utabiri wa visumbufu hususan viwavijeshi. Mafunzo hayo yatatolewa katika Mikoa ya Kigoma, Singida, Mtwara, Lindi, Morogoro, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera ambako milipuko ya visumbufu hotokea mara kwa mara kuliko maeneo mengine nchini. Aidha, Wizara itaendelea na shughuli za udhibiti wa gugumaji katika Ziwa Viktoria, ugonjwa mnyauko wa migomba *(Banana bacterial wilt),* batobato kali ya muhogo katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na mashambulizi ya inzi wa matunda katika maeneo yanayozalisha matunda kwa wingi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Kilimo kwa Wataalam na Wakulima. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wataalam wa Wizara, maafisa ugani na wakulima. Mafunzo hayo yatatolewa kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo vya Uyole, Igurusi, Tumbi, Naliendele, Ukiliguru, Ilonga, na Chuo cha Taifa cha Sukari, Kidatu. Lengo ni kuwapatia mafunzo ya Stashahada wanafunzi 650 kupitia Vyuo hivyo. Kati ya hao, wanafunzi 300 watakuwa wapya na wanafunzi 350 watakuwa maafisa ugani wanaojiendeleza. Aidha, kupitia Vyuo hivyo na Vyuo vya Mafunzo ya Wakulima vya *Kilimanjaro Agricultural Training Centre – KATC*, Mkindo, Morogoro; Inyala, Mbeya; Bihawana, Dodoma na Ichenga, Iringa. Wizara itatoa mafunzo kwa wakulima wapatao 1,800. Mafunzo hayo yanalenga kuwa na wakulima wataalam ambao watakuwa na uwezo wa kuwafundisha wakulima wenzao baada ya kuhitimu mafunzo. *(Makofi)*

Kazi nyingine itakayofanyika ni kuandaa na kuwapatia wakulima na wataalam wa ugani vitabu na vitini kuhusu mbinu za kilimo bora cha mazao ya chakula na ya biashara.

Aidha, vipindi vya redio na televisheni vitaandaliwa na kutangazwa ili kuwapatia wakulima, watalaam na jamii kwa ujumla taarifa muhimu na elimu juu ya mbinu bora za uzalishaji.
Mheshimiwa Spika, ili kusambaza elimu ya matumizi ya zana bora za wanyamakazi, Wizara itashirikiana na Halmashauri kutoa mafunzo kwa Maofisa Zana Wafundishaji 250 kwenye Halmashauri za Wilaya ili watoe mafunzo kwa wakulima. Aidha, jumla ya vikundi 200 vyenye jumla ya wakulima 3,000 katika Wilaya 20 nchini vitaanzishwa na kupatiwa mafunzo ya matumizi ya wanyamakazi. Kila kikundi kitapatiwa mafunzo kwa vitendo kwa kutumia mbinu ya shamba darasa ili kutoa fursa kwa wakulima wengi zaidi kuona na kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usindikaji wa mazao ya kilimo. Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya nafaka, mikunde, muhogo, viazi, mboga na matunda ili kuwajengea uwezo wakulima kuongeza thamani ya mazao wanayoyazalisha. Mafunzo hayo yatatolewa kupitia vikundi vya wakulima na wataalam wa Halmashauri. Wizara itatoa mafunzo juu ya utayarishaji na matumizi mbalimbali ya mazao ya mtama, muhogo, mboga na matunda. Ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa soko na matumizi ya zao la muhogo, Wizara itahamasisha wasindikaji wa mazao ya nafaka kuchanganya unga wa muhogo na unga wa nafaka. Aidha, Wizara itakusanya taarifa kuhusu viwanda vya usindikaji wa mazao ya chakula na maeneo ya uzalishaji, kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi ya kilimo. Mmomonyoko wa udongo ni tatizo kubwa nchini kutokana na wakulima wengi kutozingatia Kilimo cha kuhifadhi udongo.

Katika mwaka 2006/2007, Wizara itashirikiana na Wizara za Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Maendeleo ya Mifugo na TAMISEMI na wadau wengine wa ardhi kuandaa Mpango Kabambe wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo (*Agricultural Land Use Masterplan)* ambao utakuwa msingi wa upangaji na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo. Mpango huo utaainisha majukumu ya kila mdau katika ngazi zote: Taifa, Mkoa, Wilaya, Vijiji hadi mtu binafsi. Aidha, Wizara itashiriki kwenye mchakato wa kuandaa muswada wa sheria itakayotuwezesha kutenga na kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itakamilisha maandalizi ya kanuni za matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara pia itafanya yafuatayo:-

- Kutengeneza mfumo wa takwimu na utoaji taarifa za ardhi ya kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa za *remote sensing* na *Geographical Information System* (*GIS)* ambazo zinarahisisha ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa kwa usahihi zaidi;
- Kundaa mipango ya matumzi bora ya ardhi ya kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya;

- Kueneza teknolojia za asili za matumizi bora ya ardhi ambazo zimeonyesha kuwa endelevu katika kilimo; na

- Kusimamia upimaji wa mashamba ya wakulima, kutambua na kupima maeneo mapya yanayofaa kwa kilimo kwa ajili ya wawekezaji wadogo, wakati na wakubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Kilimo, jumla ya wakulima 4,000 watapatiwa mafunzo juu ya mbinu za Kilimo hifadhi. Mafunzo hayo yatahusu matumizi ya zana za kilimo hifadhi na matumizi ya mazao funika *(cover crops)*. Wizara itawapatia mafunzo maafisa ugani wakufunzi 64 kutoka Halmashauri za Wilaya 18 juu ya udhibiti wa mmomonyoko wa udongo, kilimo hifadhi na kilimo mseto. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya Wizara itaanzisha mashamba maalum ya mafunzo kwa wakulima juu ya udhibiti wa mmomonyoko wa udongo katika maeneo yaliyoathiriwa sana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, Mazao ya Chakula na Biashara. Wizara itahakikisha kuwa uzalishaji wa mazao makuu ya chakula hususan mahindi, muhogo, mpunga, mtama, mikunde, migomba na mbegu za mafuta unaongezeka kwa wastani wa asilimia 30 ifikapo 2010. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kuwahimiza wakulima kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao yao ili wapate bei nzuri na uhakika wa masoko ndani na nje ya nchi. Serikali itahakikisha wanunuzi wa mazao wanazingatia viwango vya vipimo katika biashara ya chakula kwa mujibu wa sheria na kanuni. Aidha, Wizara itawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi au vyama vya ushirika ili wapate bei nzuri;
- Kupanua eneo la uzalishaji wa mazao kwa kuwa bado kuna maeneo makubwa yanayofaa kwa uzalishaji ambayo hadi sasa hayatumiki. Ili kufanikisha lengo hilo, Wizara itahimiza matumizi sahihi ya zana bora za Kilimo;

- Kuhakikisha pembejeo muhimu kama vile mbolea na mbegu bora za kutosha zinapatikana na kwa wakati hasa kwa zao la mahindi;

- Kuimarisha huduma za ugani na utafiti ili kuhakikisha wakulima wanapata teknolojia bora za uzalishaji wa mazao;

- Kusimamia utelezaji wa Sheria na Kanuni za uzalishaji na biashara za mazao ya chakula. Ili kutekeleza lengo hilo, Wizara itaimarisha uwezo wa Vituo vyake vya huduma ya udhibiti wa visumbufu na itashirikiana na Halmashauri za Wilaya kusimamia sheria na kanuni za uzalishaji wa mazao ya Kilimo; na

- Kuhakikisha malengo ya uzalishaji wa mazao ya chakula yanafikiwa. Wizara itashirikiana na Halmashauri kuweka utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa malengo utakaowahusisha viongozi wote kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri hadi Vijiji. *(Makofi)*

Kuanzia tarehe 12 hadi 18 Mei 2005, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitisha vikao vya wadau wa mazao ya korosho, pamba, tumbaku na kahawa. Mikutano hii ilihudhuriwa na Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Wakuu wa Wilaya, Makatibu wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wenyeviti Watendaji wa Halmashauri, Wenyeviti wa Bodi za Mazao, Wenyeviti wa Vyama vya Ushirika, wanunuzi na wasindikaji wa mazao pamoja na wasambazaji wa pembejeo. Mikutano hii ilitoa nafasi kwa wadau kujadili hali ya uzalishaji wa mazao haya, changamoto zilizopo na hatua za kuchukua ili tuweze kuongeza tija na ubora wa mazao haya. Baadhi ya masuala muhimu yaliyoamuliwa ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao haya ni pamoja na:-

- Kuhakikisha wakulima wanalipwa bei nzuri na kwa wakati;

- Kuhakikisha kuwa pembejeo za kutosha zinapatikana kwa wakati unaotakiwa na kwa bei nafuu;

- Kuimarisha na kuboresha huduma za ugani na utafiti;

- Kupanua maeneo ya uzalishaji;

- Kusimamia Sheria na Kanuni za uzalishaji wa mazao ya biashara;

- Kuongeza wingi na ubora wa miundombinu; na

- Viongozi wote wa Taifa, Mikoana Wilaya kuelekeza nguvu zao katika kuongeza uzalishaji.

Aidha, mikutano hiyo ilitoa malengo ya uzalishaji wa mazao haya ifikapo 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uamuzi wa Serikali wa kufuta makato yote ya Bodi za Mazao na kulipa gharama za kuendesha Bodi hizo kuanzia Julai 2006 ni hatua muhimu ya kuboresha bei ya mkulima kwa mazao haya. Aidha, inasisitizwa kuwa yasiwepo makato mengine yoyote katika bei za mazao kwa wakulima bila idhini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya ukame ulioyakabili maeneo mengi yanayozalisha zao la pamba katika msimu wa kilimo wa 2005/2006, uzalishaji wa pamba katika msimu wa 2006/2007 unatarajiwa kushuka na kufikia tani 200,000 ikilinganishwa na tani 344,210 zilizozalishwa katika msimu wa 2004/2005. Ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini, Wizara itahamasisha wadau wa zao la pamba kuimarisha huduma za usambazaji na upatikanaji wa viuatilifu vya zao la pamba, itaimarisha huduma za utafiti katika zao la pamba na kuhakikisha matokeo ya utafiti yanaenezwa kwa wakulima, itawahamasisha wakulima kutumia kwa wingi samadi na mbolea za viwandani na wakulima watahamasishwa kuzingatia kanuni za kilimo bora cha pamba. Wakulima watawezeshwa kulima mashamba zaidi ya mfano katika maeneo mbalimbali yanayolima pamba ili kuhamasisha wakulima kutumia teknolojia za kisasa katika kilimo cha pamba. Aidha, usimamizi wa shughuli za zao la pamba utaimarishwa katika ngazi zote kwa

kuwashirikisha watendaji wa Serikali za Mitaa na Sekta binafsi ili kuongeza ubora na usafi wa pamba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuimarika kwa usimamizi wa shughuli za kuendeleza zao la korosho, uzalishaji wa zao hilo unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 27.23 kutoka tani 90,385 zilizozalishwa katika msimu wa 2005/2006 hadi tani 115,000 msimu wa 2006/2007. Ili kufikia lengo hilo, hatua zimechukuliwa za kuhakikisha madawa ya korosho yanapatikana kwa wingi zaidi na kwa wakati. Aidha, ili kuongeza tija, Serikali itawahamasisha wakulima kung'oa mikorosho ya zamani na kupanda mikorosho mipya inayokomaa mapema na yenye mavuno mengi zaidi. Hatua zitachukuliwa za kuhakikisha kwamba miche bora ya korosho inazalishwa kwa wingi na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, wakulima wataongezewa uwezo wa kudhibiti wadudu na magonjwa ya korosho kwa kutoa ruzuku kwenye pembejeo za udhibiti, hususan madawa na mabomba ya kupulizia madawa. *(Makofi)*

Huduma za ugani zitaimarishwa ili kuwafundisha wakulima mbinu na kanuni za uzalishaji wa korosho bora. Wauzaji nje wa korosho iliyobanguliwa watapewa vivutio na kuhamasishwa kutafuta masoko ya korosho yenye uhakika hususan katika nchi za Marekani, Ulaya na Asia zikiwemo China na Japani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 13 kutoka tani 30,000 zilizozalishwa katika msimu wa kilimo wa 2005/2006 hadi tani 34,000 msimu wa kilimo wa 2006/2007. Mikakati ya kufikia uzalishaji huo ni pamoja na kuweka utaratibu wa kupeleka mbolea ya ruzuku katika maeneo yanayolima chai na kuanzisha kilimo cha chai katika maeneo mapya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaboresha huduma za ugani kwa wakulima wa chai ili waweze kuongeza tija na uzalishaji. Wakulima watahamasishwa kuimarisha vyama vyao vya akiba na mikopo (*SACCOS*) ili wapate mikopo ya pembejeo kutoka Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zao la tumbaku msimu wa 2006/2007, unatarajiwa kuongezeka kutoka 56,500 hadi tani 65,000. Mikakati ya kufikia lengo hilo ni pamoja na kuongeza kiasi cha mbolea yenye ruzuku inayopelekwa katika maeneo yanayolima tumbaku na kurekebisha kasoro zilizopo katika utaratibu wa kutoa mikopo ya mbolea. Aidha, Bodi ya Tumbaku itasimamia kikamilifu upandaji wa miti zaidi ya milioni nane kwa ajili ya kuni za kukaushia tumbaku na hifadhi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa sukari msimu 2006/2007, unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 263,317 za mwaka 2005/2006 hadi tani 312,000. Mikakati ya kufikia kiasi hicho cha uzalishaji ni pamoja na kuongeza eneo linalomwagiliwa katika mashamba ya kiwanda cha Kagera, kupanua mashamba ya miwa ya viwanda vya Mtibwa na *TPC* katika maeneo ya Dakawa na Kahe. Aidha, kampuni ya ILLOVO inayomiliki kiwanda cha sukari cha Kilombero itaanza kutekeleza awamu ya pili ya kupanua uwezo (*capacity expansion*) wa kiwanda hicho. Vilevile, jitihada za kutafuta wawekezaji watakaojenga kiwanda kingine cha sukari katika eneo la Ruipa Wilayani Kilombero zitaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa utafiti wa miwa katika kuendeleza sekta ndogo ya sukari, Serikali itaendelea kuwahamasisha wadau wa sekta hiyo nchini waendelee kuchangia maendeleo ya Taasisi ya Utafiti wa Miwa ya Sukari (*Sugarcane Research Institute*) iliyoko Kibaha Mkoani Pwani, kwa lengo la kuiongezea uwezo wa kutafiti, kuzalisha na kusambaza aina bora za miwa inayostahimili visumbufu na ukame na kutoa sukari nyingi. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ndogo ya sukari katika kukijengea uwezo na kukiimarisha Chuo cha Taifa cha Sukari (*National Sugar Institute* ) kilichoko Kilombero ili kiweze kutoa mafunzo yanayotoa majibu kwa matatizo yanayowakabili wazalishaji wa miwa na sukari hapa nchini kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, uzalishaji wa pareto unatarajia kushuka na kuwa tani 1,500 ikilinganishwa na tani 2,500 zilizozalishwa katika mwaka wa 2005/2006. Upungufu huo wa uzalishaji unatokana na mkakati wa ufufuaji wa zao la pareto unaohusisha kuwahamasisha wakulima kung'oa pareto ya zamani yenye tija ndogo ya wastani wa kilo 250 kwa hekta na kupanda miche bora iliyo tija kubwa sawa na kilo 500 kwa hekta.

Kutokana na juhudi hizo, inatarajiwa kuwa uzalishaji wa pareto utaongezeka kwa kasi katila msimu wa 2007/2008 kukatona na miche hiyo mipya inayopandwa sasa kuanza uzalishaji. Aidha, pareto hiyo itaongeza ubora kutoka asilimia kati ya 0.8 na 1.1 hadi asilimi 1.3; maboresho hayo yataongeza pato la mkulima kwa zaidi ya asilimia 150.

Hali hiyo pia itakifanya kiwanda kusindika pareto inayokubalika katika soko la dunia na hivyo kuliongezea taifa fedha za kigeni. Mkakati mwingine ni kutafuta mbegu za pareto zilizobora na kusambaza kwa wakulima kwa ajili ya kutengeneza vitalu vya miche bora ya pareto itakayopandwa upya.

Aidha, Bodi ya Pareto itaimarisha ushirikiano na wawekezaji binafsi katika zao la pareto na kituo cha ufatifi cha Uyole kilichoko Mbeya katika kutafiti na kuzalisha miche ya pareto yenye sumu nyingi itakayosambazwa kwa wakulima wenye uzoefu ili wazalishe miche bora kwa mikataba. Aidha, uhakika wa bei na soko kwa mkulima utaimarika kwa kuanzisha kilimo cha pareto kwa mkataba (*contract farming*).

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani 34,334 zilizozalishwa mwaka wa 2005/2006 na kufikia tani 55,000 mwaka wa 2006/2007, Wizara itazihamasisha Halmashauri za Wilaya kupitia Mipango ya Kilimo Wilaya kuzalisha miche bora ya kahawa iliyotolewa na TaCRI na kuisambaza kwa wakulima kwa haraka zaidi. Aidha, wizara itawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na vyama vya ushirika ili iwe rahisi kuwapatia mafunzo ya uzalishaji wa miche ya kahawa bora, mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha kahawa, kupanua eneo la kilimo cha kahawa kwenye maeneo ambayo bado kuna uwezekano.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mkonge unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 11 kutoka tani27,000 zilizozalishwa katika msimu wa kilimo wa 2005/2006 hadi tani 30,000 msimu wa kilimo wa 2006/2007. Mikakati ya kufikia uzalishaji huo ni pamoja na

kupanua maeneo yanayozalisha mkonge, kuhusisha wakulima wadogo chini ya utaratibu wa kilimo cha mkonge. Aidha, Wizara kupitia bodi ya mkonge itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa zao la mkonge kupanua wigo wa matumzi ya zao la mkonge hususan katika uzalishaji wa nishati, mbolea, madawa, vinywaji na makaratasi.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Mazao Mengine.Wizara itaweka msukumo katika uzalishaji wa mazao ambayo yanastahimili ukame hususan muhogo, mazao yenye viinilishe kwa wingi na mazao yanayotumika kutengeneza nishati na ya kutengeneza madawa ya binadamu hususan ugonjwa wa Malaria. Mazao mengine ni ya viungo, mboga na matunda kwa ajili ya soko la ndani na nje. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaweka kipaumbele katika mazao yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uzalishaji wa muhogo na upatikanaji wa soko la uhakika, Wizara itaandaa na kutekeleza mpango wa kuendeleza zao la muhogo nchini. Mpango huo utakapoanza kutekelezwa utawezesha muhogo utakaozalishwa kusindikwa ili kupata bidhaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya binadamu, wanyama na viwanda. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Idara ya Magereza kuzalisha vipando bora vya muhogo kwa wingi ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa vipando vya zao hilo. Chini ya utaratibu huo, jumla ya vipando bora milioni 10 vitazalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, watahimizwa kujiunga na utaratibu wa kilimo cha mkataba kati yao na wenye viwanda vya kusindika mazao katika Mikoa ya Pwani, Mtwara, Lindi, Morogoro, Dar es Salaam na Tanga. Utaratibu huo unalenga kukifanya kilimo cha zao hilo kuwa cha kibiashara na hivyo kuondokana na dhana potofu kwamba muhogo ni zao la njaa tu.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha lishe na kupunguza utapiamlo wa utomwili *(protein)* nchini, Wizara itahimiza wakulima kuzalisha mazao yenye viwango vikubwa vya utomwili, hususan mazao ya aina ya soya na mahindi lishe (*Quality Protein Maize*) nchini. Wizara itaendelea kuhimiza wakulima kuzalisha mbegu bora za mazao hayo za daraja la kuazimiwa ili kuongeza upatikanaji.

Mhesimiwa Spika, Kilimo Nishati na Mazao Mapya. bei ya mafuta ya petroli na diseli inaendelea kupanda kwenye soko la Dunia kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mafuta na hofu ya kupungua kwa uzalishaji wa mafuta hayo. Dalili zilizopo zinaonyesha kuwa bei ya mafuta itaendelea kupanda, hivyo kuongeza matumizi ya fedha za kigeni kwa nchi yetu. Baadhi ya nchi duniani zimechukua hatua za kupunguza tatizo la kutegemea mafuta kutoka nje kwa kuanzisha kilimo nishati *(farming for energy).*

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na Wizara za Nishati na Madini na Viwanda Biashara na Masoko kuhimiza kilimo nishati hapa nchini. Taarifa kutoka nchi kama Brazil ambazo zilianza kilimo nishati mapema zinaonyesha kuwa kilimo hicho kina fursa kubwa ya kumuongezea mkulima mapato kutokana na mazao yanayozalishwa kuwa na bei nzuri na soko la uhakika. Mazao kama sukari, mbono (*Jatropha carcus*), muhogo, nyonyo na michikichi ni chanzo kikubwa cha nishati ya mafuta na kwa kuwa yanastawi vizuri katika nchi yetu, kuna fursa kubwa kwa nchi yetu kunufaika na kilimo nishati. Wizara yangu itaanza kufanya utafiti na kuzalisha mbegu na vipando vya kutosha vya

mazao hayo kwa ajili ya kuvisambaza kwa wakulima. Hatua nyingine itakayochukuliwa ni kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, Mazao ya Mboga, Matunda na Maua.ili kuhakikisha kilimo cha mazao mboga, matunda na maua, Wizara itawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi au ushirika na kuingia katika utaratibu wa kilimo cha mkataba. Chini ya utaratibu huo, wakulima watapata uhakika wa kupata mbegu, pembejeo bora na uhakika wa masoko ndani na nje ya nchi. Aidha, kama sehemu ya kuendeleza usindikaji wa mazao hayo, Wizara itawahamasisha wawekezaji katika viwanda vya usindikaji wa mboga na matunda kuingia mikataba maalum na wazalishaji wa mazao hayo. Aidha, Wizara itazifanyia tathmini sheria zinazosimamia upatikanaji wa pembejeo za mazao ya mboga na maua kwa lengo la kuziboresha ili kuhakikisha wakulima wa pembejeo hizo wanapata pembejeo hizo kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, usalama wa Chakula na Hifadhi ya Mazao. Wizara itatekeleza mpango wa kuzijengea uwezo Halmashauri kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula kupitia DADPs. Wizara itatoa mafunzo kwa timu za wawezeshaji wa Halmashauri ili ziwasaidie wakulima kuibua miradi inayolenga kuboresha usalama wa chakula. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kuratibu hali ya uzalishaji wa mazao na chakula nchini. Ili kutekeleza lengo hilo, Wizara itatoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia za *Geographical Information System (GIS)* na *Geographical Positioning System (GPS)* kwa wataalam waliopo Wizarani na katika Halmashauri ili kupata takwimu sahihi. Aidha, Wizara itapanua mtandao wa vituo vya kupima kiasi cha mvua kutoka vituo 500 vya sasa hadi vituo 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa chakula, Wizara itaendelea kufanya savei mbalimbali za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula ili kubaini hali ya chakula nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini za kina katika maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula. Sambamba na hayo, Wizara itaratibu utayarishaji wa Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uhakika wa chakula katika ngazi ya kaya, Wizara itaendelea kusambaza teknolojia mbalimbali za kupunguza upotevu wa mazao ya chakula baada ya mavuno kwa kutoa mafunzo ya ujenzi wa vihenge bora kwa mafundi mchundo, wakulima na wataalam wa Halmashauri na mafunzo ya hifadhi bora ya mazao ya nafaka na mikunde kwa wataalam wa Halmashauri. Aidha, ili kueneza teknolojia hizo, Wizara itafanya maonyesho ya usindikaji na matumizi ya mazao ya chakula katika maonyesho mbalimbali ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wataalam wa Halmashauri na wakulima kuhusu utayarishaji na matumizi ya mazao ambayo yana virutubisho muhimu katika kusaidia kuongeza kinga ya mwili katika kupambana na UKIMWI na kuongeza muda wa kuishi kwa matumaini. Mazao hayo ni kama vile; ulezi, mahindi yenye protini nyingi, uwele, soya, muhogo, magimbi, njugu mawe, maharage, dengu, njegere, mawese, alizeti, ufuta, karanga, nazi, na mboga na matunda. Mazao mengine ni viungo kama vitunguu swaumu, tangawizi, iliki, kotimiri na vitunguu maji.

Wakulima wanashauriwa kuzalisha na kula vyakula vya mazao hayo kwa kuwa vina faida kubwa mwilini.

Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)* itaanza mwaka 2006/2007 bila akiba ya chakula. Ili kuijenga upya akiba ya chakula, katika mwaka 2006/2007, Wizara imepanga kununua jumla ya tani tani 80,000 za mahindi na mtama. Aidha, tani 30,000 za mahindi zitaagizwa kutoka nchi za nje na hivyo kufanya akiba yote kufikia jumla ya tani 110,000.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo. Wizara inatekeleza miradi na programu za Kitaifa kama sehemu ya utekelezaji wa *ASDP* (Kiambatisho Na. 6). Miradi au programu hizo ni:-

(i) Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agriculture Sector Investment Project- DASIP):* Mradi huo ulizinduliwa mwezi Aprili, 2006 na utatekelezwa kupitia Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga. Katika mwaka 2006/2007, mradi umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuunda timu za wawezeshaji za Wilaya na kata na kuzipatia mafunzo ili kuzijengea uwezo wa kuwafundisha wakulima kuibua, kuandaa na kutekeleza miradi ya Kilimo. Aidha, timu hizo, zitawajibika kufuatilia utekelezaji wa miradi na usimamizi wa matumizi ya fedha;

- Kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya katika maeneo ya Mradi wa kuandaa Mipango ya Wilaya ya Maendeleo ya Kilimo inayozingatia mahitaji ya wakulima;

- Kutoa mafunzo kwa wakulima yatakayowawezesha kuanzisha na kusimamia asasi za akiba na mikopo *(SACCOS).*

(ii) Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project - PADEP*): Mradi huu unatekelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Lindi, Arusha, Singida, Iringa, Manyara, Kilimanjaro, Tabora na Mtwara na Zanzibar Mikoa ya Mjini Magharibi, Kusini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba. Katika mwaka 2006/2007, Mradi umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- Kuendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi ya jamii na vikundi na kuimarisha uwezo wa Wilaya katika kusimamia shughuli za maendeleo ya Kilimo na Ushirika.
- Kuwezesha jamii kubuni na kutekeleza miradi kwa kutumia mbinu shirikishi na kuwapatia wakulima elimu kuhusu kanuni bora za kilimo na ufugaji;

- Kukamilisha ukarabati wa maabara za udongo na kuzipatia vifaa vya maabara; na

- Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji katika ngazi ya Wilaya na Kata ili kuwaongezea uwezo wa kuwezesha jamii na vikundi vya wakulima kuibua matatizo yanayowakabili na kuandaa miradi ya kakabiliana nayo.

(iii) Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Programme Support (ASPS):* Sehemu kubwa ya programu inatekelezwa katika Mikoa ya Mbeya na Iringa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani katika Mikoahiyo. Katika ngazi ya Wizara, programu itaendelea kusaidia kujenga uwezo wa wizara katika uhuishaji na usimamizi wa sera na kufundisha wakulima uzalishaji wa mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji na Mikopo Katika Kilimo. Kama sehemu ya kuwavutia wawekezaji na kuongeza upatikanaji wa mikopo katika Kilimo, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Biashara la Taifa, Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara *(Businsess Enviroment Strengthening in Tanzania (BEST),* Wizara za Miundombinu, Ardhi na Makazi na Mipango Uchumi na Uwezeshaji itatekeleza mikakati ifuatayo:-

- Kuainisha maeneo ya mashamba ya kati na makubwa kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji katika kilimo cha kibiashara;

- Kuhamasisha taasisi za fedha kukubali mashamba yaliyopimwa kutumika kama dhamana ya kupatia mikopo;

- Kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuwekeza katika Sekta ya Kilimo;
- Kuhamasisha wakulima kujiunga katika Kilimo cha mkataba kwa lengo la kuwapatia wakulima huduma za ugani, pembejeo pamoja na masoko ya uhakika;

- Kutunga Sheria ya kulinda ardhi ya Kilimo;

- Kuandaa ramani inayoonyesha uwezekano wa maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa mazao kulingana na hali ya hewa, udongo na miinuko ya ardhi;

- Kuandaa Sera ya Umwagiliaji itakayowavutia wawekezaji kuwekeza katika Kilimo cha umwagiliaji;

- Kuhamasisha wakulima kutumia huduma za mikopo zitolewazo na *Private Agricultural Sector Support (PASS)* chini ya Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo; na

- Kuimarisha *SACCOS* kuwa njia mojawapo ya kutoa mikopo kwa wananchi hususan wakulima.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, utaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya kununua na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Mikopo hiyo itatolewa kupitia taasisi za fedha hususan benki na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania *(SCCULT).*

Ili kuboresha utoaji wa huduma za mikopo, katika mwaka 2006/2007, Mfuko umeingia mkataba na Taasisi inayoitwa Dunduliza ambayo inahudumia *SACCOS* katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Ruvuma na Mara pamoja na Benki ya Biashara na

Uchumi ya Mkoa wa Kilimanjaro. Katika mwaka 2006/2007, Mfuko umepanga kutoa mikopo yenye jumla ya Shilingi bilioni 3.5. Aidha, Mfuko utaendelea kukusanya madeni pamoja na kuuza dhamana za wadaiwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini. Lengo la Programu hiyo ni kufufua, kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini. Ili kufanikisha utekelezaji wa Programu hiyo, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kuandaa na kusambaza miongozo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ili kuviwezesha Vyama kujiendesha kibiashara na kwa kuzingatia sheria na taratibu za Vyama vya Ushirika na maslahi ya wanachama wake;

- Kuziwezesha Halmashauri za Wilaya kutoa mafunzo kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika ili kuwawezesha kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003;

- Kutoa elimu ya uhamasishaji, ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika kwa Maafisa Ushirika katika ngazi za Mikoana Wilaya ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kama sehemu ya utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika;

- Kuimarisha *SACCOS* kwa kuziwezesha kubadili mifumo ya uendeshaji, uandaaji wa mipango ya biashara, kuajiri watendaji wenye sifa, kuimarisha uwezo wa utunzaji na usalama wa fedha za wanachama;

- Kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika kujadiliana na benki za biashara ili kupata mikopo;

- Kushirikiana na wadau wengine, hususan taasisi za Serikali kuwahamasisha wananchi kujiunga na kuanzisha Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kuufanya Ushirika ushamiri kama chombo cha kumkomboa mwananchi kutoka kwenye umasikini; na
- Kuhamasisha wadau wa ushirika kuunda Baraza la Ushauri wa Ushirika Tanzania *(Tanzania Cooperative Advisory Council).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Wizara itaendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kubinafsisha mali ambazo hazijabinafsishwa. Mali hizo ni mashamba ya Kahawa ya Mbozi, kiwanda cha chai cha Dabaga, Mashamba ya ngano ya *West Kilimanjaro (Foster* na Kanamondo), mashamba ya mahindi ya Mbozi na Namtumbo, mali za *NMC* zilizoko Mwanza, viwanda vya matunda vya Tangold vilivyoko Tanga na Dar es Salaam na ghala lililopo kiwanja Na. 192 Barabara ya Nyerere, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Sekta ya kilimo ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya

sasa. Wizara itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mbolea utakaoweka utaratibu wa kusimamia uagizaji, utengenezaji, usambazaji na matumizi endelevu ya mbolea nchini. Aidha, Wizara itaendelea na mchakato wa kurazinisha Bodi za Mazao (*Rationalisation of Crop Boards)*. Mchakato huo utakamilika kwa kurekebisha Sheria zilizounda Bodi za Mazao. Marekebisho hayo yatawezesha Bodi kutekeleza majukumu yake ya usimamizi (*regulatory roles*) kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya sasa au malengo ya kutungwa kwa sheria hizo. Aidha, Wizara itaendelea na mchakato wa kuandaa muswada wa Sheria ya Kilimo itakayotambua, kulinda na kuendeleza maeneo ya kilimo nchini. Mswada wa sheria hiyo unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwaka 2006/2007. Sheria itakayotungwa itasaidia katika kusimamia shughuli za kilimo kwenye maeneo yatakayopimwa na kuainishwa kwa kilimo. Sheria italenga katika kutofautisha matumizi mbalimbali ya ardhi kwenye maeneo ya kilimo na kuweka utaratibu wa kusimamia matumizi endelevu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kutoa huduma kwa wadau wa Sekta ya kilimo. Ili kutekeleza lengo hilo, Wizara itatekeleza mikakati ifuatayo:-

- Kuajiri watumishi 276 ili kuongeza nguvu kazi katika utoaji wa huduma;

- Kutekeleza mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Rushwa pamoja na kuzingatia maadili katika Utumishi wa Umma. Wataalam watapatiwa mafunzo ya namna ya kutekeleza mikakati hiyo;

- Kutoa mafunzo kwa watumishi 100 ili kukidhi mahitaji ya Miundo yao ya Utumishi (*Schemes of Service*) ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi;

- Kuwapandisha vyeo watumishi 904 katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia sera ya menejiment ya ajira katika utumishi wa umma;

- Kuelimisha na kuhamasisha watumishi kuzingatia masuala ya jinsia katika upangaji na utekelezaji wa majukumu yao; na

- Kuelimisha watumishi mbinu za kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Watumishi watapatiwa elimu ya lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kufanya utafiti wa kutoa teknolojia zinazoweza kupunguza harubu katika uzalishaji na pia itafanya utafiti wa kuzalisha mazao vyenye lishe bora kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, hususan Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi na waheshimwa

Wabunge waliochangia Hotuba za Waziri Mkuu, Mawaziri wa Fedha, Mipango Uchumi na Uwezeshaji kwa michango yenu mliyoitoa kuhusu masuala tunayopaswa kuyazingatia ili kilimo kikue kwa kasi zaidi na hivyo kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuondoa umaskini. Tutazingatia maoni na ushauri wenu katika utekelezaji wa mipango ya Wizara, hususan katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Programu hiyo, ndiyo itakayotafsiri kwa vitendo utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Strategy (ASDS*) pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) miongoni mwa wakazi wa Vijijini.

Aidha, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo inatekeleza dhana ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*decentralization by devolution*) ili washiriki kikamilifu katika kuibua matatizo yanayowakabili, kupanga mipango ya kukabiliana nayo, kushiriki katika utekelezaji wa mipango hiyo na kufanya tathmini ya mafanikio ya utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija, mavuno na mapato kwa wakulima, ipo haja ya kuhakikisha wakulima wanaongeza matumizi ya pembejeo bora za kilimo hususan mbolea, mbegu bora na madawa ya kilimo. Ili kuwa na uhakika wa uzalishaji, hususan wa mazao ya chakula ni muhimu kuongeza maeneo ya kilimo cha umwagiliaji endelevu.

Kwa hiyo, Mpango wa Wizara wa mwaka huu ni hatua kubwa ya mwanzo katika kuielekeza nchi yetu katika *Mapinduzi ya Kijani (Green Revolution).* Viongozi na watendaji wote kwenye ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya wanatakiwa kutoa kipaumbele cha pekee katika kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ikiwa ni pamoja na kusimamia usambazaji wa mbolea yenye ruzuku ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyotamkwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu Mwaka 2005, Ushirika una nafasi muhimu sana ya kuleta mapinduzi katika kilimo kwa sababu Ushirika ndio njia kuu ya uwezeshaji kwa wananchi walio wengi kukusanya nguvu zao ili kujiletea maendeleo kwa haraka zaidi.

Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi hususan wakulima, kuanzisha na kujiunga na vyama vya ushirika na kuhakikisha wanachagua viongozi waadilifu na wanaowajibika ipasavyo kwa wanachama wao.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Viongozi wenzangu wa Wizara hii: Naibu Mawaziri Mheshimiwa Hezekiah V. N. Chibulunje na Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Katibu Mkuu Bwana Peniel M. Lyimo na Naibu Katibu Mkuu Bwana Mohamed S. Muya na kwa niaba yangu mimi mwenyewe napenda kuchukua nafasi hii kutoa

shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kututeua na kutukabidhi madaraka ya kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo marefu kuhusu maendeleo na matatizo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, naomba nichukue nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza Kilimo. *(Makofi)*

Kwanza napenda kuzishukuru nchi za China, Canada, Denmark, Finland, India, Ireland, Israel, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Norway, Saudia, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *BADEA, UNDP, FAO, JICA, DFID, EU, UNICEF, UNIDO, WFP, IFAD, CIMMYT, CFC, ICRISAT, ASARECA, USAID, GTZ, IITA, DLCO-EA, IRLCO-CSA* na Sasakawa *Global 2000.* Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunayaihitaji ili tuweze kuendeleza Kilimo nchini. Napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa wafanyakazi wenzangu nikianza na Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Hezekiah V. N. Chibulunje na Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, kwa msaada na ushauri wao katika kutayarisha Bajeti hii. Aidha, Katibu Mkuu Peniel M. Lyimo, Naibu Katibu Mkuu Mohamed S. Muya, Wakuu wa Idara na Wafanyakazi wa Wizara yangu pamoja na wale wa taasisi zilizo chini ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Ndugu wakulima ahsanteni sana. Naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 123,093,381,600 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2006/2007.

Kati ya fedha hizo, Shilingi 77,280,932,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 45,812,449,600 ni kwa ajili ya shughuli za Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo, Shilingi 8,353,994,000, sawa na asilimia 18.24 ni fedha za ndani na Shilingi 37,458,455,600, sawa na asilimia 81.76, ni fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Kutoa Hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimekwisha pokea majina ya wachangiaji 30 Katibu amefanya chambuzi, saba hawajaongea katika hoja yoyote kwa hiyo hao ndiyo nitawapa kipaumbele nao ni:-

Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo , Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi na Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda hao saba. Orodha ya waliokwisha changia mara moja ni ndefu mno sitaisoma lakini mtaona katika orodha tutakayochapisha tahadhari kwa hao waliokwisha changia mara mbili kwa hiyo matumaini ya kuchangia hoja hii pamoja na kuwa ni siku mbili kwa uzoefu wetu kwa sababu pengine watafikiwa lakini niwataje: Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, na Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, nafasi yenu ni finyu, kwa hiyo tutaanza na hawa ambao hawajachangia saba, halafu tutakwenda kwa wale waliochangia mara moja tu tangu umeanza mkutano wetu huu ambao ni 20.

La pili, Waheshimiwa Wabunge kuna baadhi yetu mmekuwa mkishangaa kwamba kabla hatujaingia Kamati ya Matumizi nasimama kuwahoji na baadhi yenu mmekwenda mbali zaidi mkadhani nakosea kila jambo ninalolifanya hapa najitahidi kujianda vizuri sana, sasa katika hatua ile ninapowahoji kabda hatujaingia katika Kamati ya Matumizi ni utaratibu wa Kibunge Spika hawezi kuondoka tu akaenda kuvua joho inabidi Spika aseme sasa tunaingia katika hatua tofauti na kwa hiyo nawahoji na hoja yangu ndiyo maana sisemi mpitishe makadirio katika hatua hiyo nawahoji ili tuingie katika Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo msijione kwamba nawafunga kwamba nimesema wanaoafiki waseme ndiyo ni kwamba tunakubali hoja ya Waziri, hoja ya Waziri tunaikubali mwisho lakini siwezi kuondoka hapa bila hoja yoyote nikageuka tu niaenda itakuwa ni jambo la ajabu sana. Kwa hiyo ninapowahoji mara ya kwanza nawahoji tuingie katika hatua ya Kamati ya matumizi. Ahsante sana.

Msemaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Monica N. Mbega.

**MHE. JOHN M. CHEYO:-** Maelekezo ya Spika.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa John M. Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:-** Kwa kuwa inavyoonekana kuna *speech* mbili zinazotolewa na Mawaziri, kuna hii ambayo imeandikwa na imechapwa na ile ambayo imesomwa na Mawaziri na kuna *difference* kubwa sana sasa sisi tunapojadili tufuate zaidi ipi? Maneno yaliyomo humu au maneno ambayo yatakuwa kwenye *Hansard*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Masuala ya Bunge, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:-** Mheshimiwa alichosema ni sawasawa inapaswa kuwa mbili, moja hii inayowekwa pale ambayo inaweza kuwa ndefu sana lakini anakuwa na *summary* muda aliopewa ni dakika 30 tu kwa hiyo anafanya *summary* ya hiki lakini ndiyo maana kinawekwa mezani asubuhi ili waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili waichukue hii na ile *summary* yake.

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu ulioanzishwa kama miaka mitatu iliyopita tulipoanza kuweka hii mezani, zamani ilikuwa haiwekwi hivi tulipoanza kuweka kwa makusudi hayohayo ili kuokoa muda lakini Waziri anaweza mengi sana ya kusema ambayo hayawezi kusemwa yote kwa nusu saa ndiyo maana anaweka hii mezani ili waweze kuchangia. *(Makofi)*
Kwa hiyo wachangiaji wanaweza kusoma yote mawili.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante kwa ufafanuzi huo sasa namwita Mheshimiwa Tatu Ntimizi.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:-** Muongozo wa Spika.
**SPIKA:** Muongozo wa Spika.

**MHE. TATU M. NTIMIZI: -** Mheshimiwa Spika, nafikiri Mwenyekiti wa Kamati wa Wizara hii hajawasilisha na Kambi ya Upinzani kabla ya mchangiaji hajaanza. Sijui kama ni ndivyo?

**SPIKA:** Ndiyo namuita Mwenyekiti wa Kamati kwanza atafutiwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo.

**MHE. GIDEON ASIMULIKE CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI: -** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka uliopita pamoja na maoni ya Kamati juu ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia ndani ya Bunge lako Tukufu naomba kabla sijaanza kutekeleza Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge toleo la 2004 nitumie nafasi hii kutoa pongezi na shukrani chache.

Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ally Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Pili, napenda nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili tukufu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa

kukusaidia kuliongoza Bunge letu tukufu, mimi na waheshimiwa Wabunge wenzangu tuna imani kubwa na uwezo wenu wa kuongoza kwa kiwango na kasi mpya.

Tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliuwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri wote kwa kuteuliwa kushika nyadhifa walizonazo, wote wameanza kazi zao vizuri nawatakia mafanikio mema, tuko pamoja.

Nne, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi au kuteuliwa na Rais kuingia katika Bunge hili tukufu wote nawatakieni uwakilishi mwema.

Mwisho napenda kutoa shukrani maalum kwa wananchi wa Jimbo la Ileje kwa imani na heshima waliyonipa kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na pili nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa kunipa heshima ya kuwa Mwenyekiti wao na kwa ushirikiano wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na shukrani hizo napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi ambao ndiyo waliochambua na kutoa maoni na mapendekezo kuhusu bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, wajumbe hao ni :-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo – Mwenyekiti;
Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe - Makamu Mwenyekiti;
Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah - Mjumbe;
Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir - Mjumbe;
Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan - Mjumbe;
Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha - Mjumbe;
Mheshimiwa Salim H. Khamis - Mjumbe;
Mheshimiwa Castor R. Ligallama - Mjumbe;
Mheshimiwa Joyce N. Machimu - Mjumbe;
Mheshimiwa Manju S. O. Msambya - Mjumbe;
Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye - Mjumbe;
Mheshimiwa Said Juma Nkumba- Mjumbe;
Mheshimiwa Juma Said Omar - Mjumbe;
Mheshimiwa Shally J. Raymond - Mjumbe;
Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti - Mjumbe;
Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu - Mjumbe;
Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda - Mjumbe;
Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla - Mjumbe; na
Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe - Mjumbe.

Wajumbe wa Kamati hii tumefarijika sana kwa uteuzi wa Mheshimiwa Kidawa Hamad Salehe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu kuwa Katibu wa Idara ya Oganaizesheni ya Chama Cha Mapinduzi, tunampongeza sana.

Aidha tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa mwaka 2005/2006. Kamati yangu ilitoa ushauri mbalimbali kwa Wizara katika maeneo kadhaa, nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuyafanyia kazi maeneo hayo na hatua za utekelezaji zilizochukuliwa zimeonekana. Kamati imeridhishwa na hatua hizo, aidha katika maeneo ambayo yameonekana kuhitaji juhudi na kuboreshwa zaidi Kamati yangu imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio na Matatizo katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006. Kwanza mafanikio Kamati yangu ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha uliopita.

Baadhi ya Mafanikio ni pamoja na kwanza mikopo ya Pembajeo mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 5,745,510,720/= ilitolewa kwa wakulima kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembajeo. Kadhalika Wizara imeweza kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za mazao ili kuongeza uzalishaji na kukabiliana na tatizo la njaa.

Pili, tani 14,955 za chakula cha bure zigawiwe kwa wananchi 564,723 hali kadhalika tani 105,318 za mahindi ya bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo moja zitolewe kwa wananchi waliokuwa na upungufu wa chakula ambao hawakuwa na uwezo wa kununua kwa bei soko.

Tatu, jumla ya hekta ya 14,396 za eneo la umwagiliaji zimeongezeka na kufanya jumla ya eneo lote linalotumia kilimo cha umwagiliaji kufikia hekta 264,388. Aidha, Skimu nyingine 29 zenye jumla ya hekta 3604 ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Nne, Serikali kwa kushirikiana na wakulima imefanikiwa kupambana na milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao kama vile kweleakwelea nzige, viwavijeshi pamoja na magonjwa ya mimea. Hali kadhalika Wizara imefanikiwa kukarabati vyuo na vituo vya tafiti mbalimbali za kilimo.

Tano, program kabambe ya mageuzi ya modernisation ya Ushirika nchini yaani *Cooperative Reform and Modernisation Program* ilianza kutekelezwa ili kuwawezesha wanachama kuibua ushirika unaondeshwa kibiashara wenye nguvu za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Changamoto. Pamoja na mafanikio hayo Kamati yangu pia ilifahamishwa changamoto kadhaa zinazoikabili Wizara, changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, baadhi ya malengo ya Wizar yalishindwa kufikiwa kutokana na ukame ulioikumba nchi ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa mazao na kupunguza ukuaji wa sekta ya kilimo kutoka asilimia 5.8 kwa mwaka 2004 hadi asilimia 5.2 kwa mwaka 2005.

Pili, Halmashauri za Wilaya zilishindwa kuandaa mipango ya kuendeleza kilimo kutokana na kukosa watalaam wa kutosha.

Tatu, ubovu wa Miundombinu hususan barabara za vijijini unaathiri usambazaji wa pembejeo, upatikanaji wa masoko ya mazao, uwekaji na kusababisha gharama kubwa za uzalishaji.

Nne, Idara ya Ushirika kuwa na upungufu wa watumishi na hivyo kuchelewesha au kukwamisha utekelezaji wa shughuli za ushirika.

Tano, wananchi wengi hawajajiunga na vyama vya ushirika, aidha elimu ya umuhimu wa kujiunga na vyama vya ushirika bado ni ndogo.

Sita, maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini bado hayatumiki ipasavyo na hivyo kufanya kilimo kiwe cha kutegemea mvua zaidi. Takwimu za sasa zinaonyesha ni asilimia 8 tu ya wakulima ndiyo wanatumia kilimo cha umwagiliaji maji.

Saba, kiwango cha usindikaji wa mazao yetu bado ni kidogo sana hali hii husababisha mazao mengi yauzwe yakiwa ghafi na hivyo kuyapunguzia ubora na thamani na hatimaye kupata bei ndogo katika soko. Kadhalika, mazao mengine kwa mfano matuna na mboga huharibika kabla hayajauzwa.

Nane, fedha zinazotengwa kwa ajili ya hifadhi ya Chakula cha Taifa *SGR* ni kidogo na hazitoshelezi kuhimili ushindani wa soko, fedha hizo pia huchelewa kutoka hali ambayo husababisha ununuzi ufanyike kwa bei ya juu kwa msimu wa mavuno unakuwa umepita.

Tisa, kuwepo kwa huduma duni za ugani na ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalam wa ugani kunapunguza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaipongeza Wizara na Serikali kwa jumla kwa jinsi walivyoshughulikia tatizo la njaa iliyoikumba sehemu kubwa ya nchi yetu katika msimu wa mwaka 2005/2006.

Mojawapo ya hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kuondoa ushuru kwa waagizaji wa chakula kutoka nchi za nje ili hatimaye wananchi walio wengi wamudu kununua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo nzuri, bei za vyakula katika masoko mengi nchini hazikuzingatia azma hiyo ya Serikali. Wananchi waliendelea kuuziwa chakula kwa bei kubwa sana. Ili kutatua tatizo hili, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kwa karibu zaidi uuzaji wa chakula hicho.

Mheshimiwa Spika, ili kuepukana na tatizo la upungufu wa chakula, Kamati yangu inaishauri Serikali ijielekeze kwa nguvu zake zote katika kutekeleza Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji kama alivyoeleza hivi punde Mheshimiwa Waziri. Aidha, msisitizo uwekwe kwenye ujenzi wa mabwawa, uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya umwagiliaji pamoja na ufufuaji wa mifereji ya asili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Kilimo cha Umwagiliaji kisiwe cha kutawanyisha fedha kila mahali, bali msisitizo zaidi uwekwe kwenye maeneo ambayo yataleta tija. Hii haimaanishi kwamba sehemu nyingine za Tanzania zisiwe na Kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada hizi, Serikali kwa kushirikiana na wananchi iimarishe na kurejesha utamaduni wa hifadhi nzuri za chakula kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kijijini. Lengo ni kuwa na akiba ya chakula katika ngazi ya Taifa na Kaya wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba yaainishwe maeneo (*agro-ecological zone*) ambayo yanafaa kwa kila zao ili kuwawezesha wananchi kulima mazao ambayo yanastawi katika maeneo husika na kuepuka kulima mazao ambayo hayastawi katika maeneo fulani.

Hali kadhalika wananchi hasa wa maeneo kame, wahamasishwe kulima mazao yanayostahimili ukame kama mihogo, viazi, mtama, uwele na mazao jamii ya kunde kama mbaazi, choroko na kadhalika. Hata kama mazao hayo hayana bei nzuri katika soko, walime kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa katika hotuba ya Bajeti ya Ofisi yake kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imeweka kilimo kuwa agenda namba mbili na hivyo kuwa na matarajio ya kujitosheleza kwa chakula ifikapo mwaka 2010. Kama ilivyowekwa bayana, kuwa Viongozi wote wa ngazi ya Mkoa na Wilaya watahusika moja kwa moja katika kutekeleza azma hiyo na watapimwa, Kamati yangu inashauri na kutoa wito kwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri zetu na sisi Waheshimiwa Wabunge tujue kwamba sisi ndio wahamasishaji wakuu katika kuhakikisha kuwa lengo hili la Serikali linafikiwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli usiopingika kuwa Vyama vya Ushirika ni nyenzo zinazoweza kuwakwamua wakulima wetu na kuwawezesha kuondokana na umaskini na kipato. Hata hivyo, Vyama vingi vya Ushirika Nchini vinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa mitaji pamoja na riba kubwa inayotozwa kwenye mikopo inayotolewa na mabenki. Kwa mfano, hivi sasa Vyama vya Ushirika vinadaiwa na Taasisi mbalimbali za fedha jumla ya Shilingi bilioni 23.8

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaishauri Serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wadau wengine kuangalia uwezekano wa kufuta deni hili ambalo historia yake ni ndefu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapa wakulima nguvu ya pamoja na kuwa na sauti kuhusu bei za mazao yao, ni muhimu kuendelea kuimarisha huduma za ushirika. Shughuli za Ushirika ndani ya Wizara ziendelee kupewa uzito unaostahili. Serikali kupitia Wizara ihamasishe wananchi wajiunge na Vyama vya Ushirika. Msisitizo zaidi uwekwe kwenye Vyama vya Msingi kama Sheria inavyotamka na kwa kuzingatia Programu Kabambe ya Mageuzi na *Modernisation* ya Ushirika Nchini.

Aidha, Serikali kwa ujumla wake iendelee kusimamia na kudhibiti mwenendo wa soko huru kwa mazao ya kilimo. Serikali pia isambaze kwa lugha rahisi elimu kuhusu sera na Sheria ya Vyama vya Ushirika ili wananchi washiriki ipasavyo katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo *(ASDP),* Kamati inaipongeza Wizara kwa kubuni Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo inayolenga kuiwezesha nchi yetu kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 110 kuanzia mwaka huu 2006. Hata hivyo, utekelezaji wa programu hi unategemea sana uwezo wa Halmashauri zetu kinyenzo na kitaalam ambao hivi sasa ni mdogo sana. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya wakati wa kutekeleza programu hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mifano mizuri ya mafanikio ya wakulima wadogo na Chai, Miwa, Mikonge na kadhalika, ipo haja ya kuendeleza kilimo cha wakulima wadogo kwa mazao ya biashara kwa utaratibu wa Mkataba kati ya wakulima wadogo na ama wakulima wakubwa na Viwanda vya kusindika mazao husika. Utaratibu huu unganifu katika uzalishaji utawahakikishia wakulima wadogo soko, bei nzuri na ubora wa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mazao Makuu ya Biashara kama vile Pamba, Kahawa, Korosho, Tumbaku, Mkonge, Pareto, Chai, Miwa na kadhalika, yapewe msukumo wa pekee ili kuyaongezea uzalishaji wa tija. Mfano wa zao la Pamba, tuongeze uzalishaji kutoka kilo 300 kwa ekari moja hadi kilo 100 kwa ekari. Hali kadhalika, masoko kwa mazao hayo yatafutwe ndani na nje ya nchi. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua ya kuwakutanisha Wadau wa Mazao hayo na kupeana kazi.

Aidha, ili kumwongezea mkulima pato litokanalo na mazao yake, Kamati inaona iko haja kwa Serikali kupunguza na kuondoa makato na kodi nyingi kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa huduma za ugani kwa wakulima Vijijini ni moja ya changamoto zinazosababisha nchi yetu kukumbwa na tatizo la njaa mara kwa

mara. Aidha, uchache wa wataalam wa Sekta ya Kilimo Vijijini pia unachangia wakulima kutotumia mbinu za kisasa katika kilimo. Hali hii inatokana na ukweli kwamba watalaam wengi wa ugani wanaishia maofisini, hawaendi mashambani kutokana na kukosa nyenzo na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili Halmashauri ziwezeshwe kuwa na wataalam wa ugani wa kutosha. Aidha, watalaam hao wapatiwe nyenzo za kutendea kazi, mafunzo, waongezewe maslahi na wawajibishwe kwa kupewa hadidu za rejea ili kuhakikisha ufanisi katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati yangu inashauri kuwa ni vyema Maafisa Ugani wapangiwe maeneo ya kazi kulingana na taaluma walizosomea. Kama ni Mtaalam wa Kahawa apelekwe kwenye maeneo yanayolimwa Kahawa. Kwenye maeneo ya Mkonge, Chai, Pamba na mazao mengine kadhalika upangaji wa Maafisa Ugani uendane na Taaluma zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ihamasishe uanzishaji wa mashamba darasa kwa ajili ya kuwaelimisha wakulima juu ya mbinu za kisasa za kilimo kwa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuanzisha Mfuko wa Pembejeo. Mfuko huu unalenga kuwakwamua na kuwawezesha wakulima walio wengi kumudu kununua pembejeo hizo na hivyo kuongeza uzalishaji wa tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali isimamie kwa karibu Makampuni na watu binafsi waliopewa dhamana ya kusambaza pembejeo ili wasiwauzie wananchi kwa bei ya juu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupunguza urasimu ili mikopo ya pembejeo iwafikie wakulima kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara, kuhakikisha kuwa pembejeo zinawahishwa kwa wakulima angalau miezi mitatu au minne kabla ya msimu wa kilimo. Hali kadhalika, Vyama vya Ushirika vipewe uwezo wa kusambaza pembejeo hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na taarifa sahihi za Miradi ya Kilimo na Bajeti ya Kilimo kila mwaka, Kamati inaishauri Wizara iainishe miradi na fedha zilizotengwa kwa Wizara yenyewe kwa upande mmoja na miradi na fedha zilizotengwa kwa Mamlaka/Taasisi nyingine kwa upande mwingine. Mamlaka hizo ni pamoja na Serikali za Mitaa, Taasisi za Kilimo na kadhalika. Lengo hapa ni kupata picha kamili ya fungu la fedha katika Sekta ya Kilimo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, karibu Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia katika majadiliano ya Hoja ya Bajeti ya Serikali na ile ya Waziri Mkuu wamezungumzia Sekta ya Kilimo. Hii inadhihirisha umuhimu wa Sekta ya Kilimo

katika Uchumi na Maendeleo ya Taifa letu. Kilimo ndicho kiwanda mama cha Uchumi wa Taifa letu na ni mwajiri mkuu wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ili wakulima wawe na uhakika na maeneo yao ya kilimo, ni muhimu zoezi la kutambua, kupima na kuwamilikisha mashamba yao Vijijini liendelee kwa nguvu na kasi mpya. Zoezi hili likikamilika, wakulima hawatakuwa na hofu ya kuhama au kuhamishwa, watatumia hatimiliki zao kama dhamana ya kupata mitaji kutoka vyombo vya fedha. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali iendelee kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya zoezi hili. TAMISEMI iratibu zoezi hili kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati yangu inashauri kuwa, msisitizo uwekwe katika kumilikisha mashamba kwa vijana. Hatua hii itavutia vijana wengi zaidi kushiriki katika kilimo na hivyo kukiona kilimo kuwa ni kazi kama kazi nyingine. Halikadhalika, Serikali iangalie uwezekano wa kuyatumia mashamba ambayo yamebinafsishwa ili vijana wapate ajira.

Sambamba na zoezi hilo, Serikali pia iharakishe kujenga miundombinu na kupeleka huduma muhimu kama maji na Zahanati kwenye maeneo ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, Programu za Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo Wilayani *(DADPs)* zinalenga kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* katika ngazi za Vijiji na Wilaya. Kwa mantiki hiyo, mafanikio ya *(DADPS)* ndiyo yatakayopelekea programu nzima ya Sekta ya Kilimo ifanikiwe. Ili programu hizo ziweze kutekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi ili waibue miradi yao. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ihusishe pia uboreshaji wa miundombinu hususan barabara Vijijini katika programu za *DADPs*.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji *(RUBADA)* ikitumiwa na kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake, itatoa mchango na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Kilimo. Hata hivyo, inaonekana Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto na vikwazo vingi sana hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hii, Kamati inaishauri Wizara kukutana na Mamlaka hii ili kubaini changamoto hizo na namna ya kuzikabili ili hatimaye kuipa mamlaka uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu inaunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwa heshima kubwa, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kupitisha kiasi cha fedha kinachoombwa katika Fungu 43 na nataja tarakimu ambazo zimetolewa na Wizara ya Fedha ni Sh.121,593,381,600/=. Kati ya fedha hizo, Sh.75,780,932,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 45,812,449,600/= ni

kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Fedha za ndani ni Sh. 8,353,994,000/= na fedha za nje ni Sh.37,458,455,600/=.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Wizara hii ni kidogo sana na hakitoshelezi kutekeleza majukumu yote ya Wizara hasa katika kipindi hiki kinachotajwa kuwa cha Mapinduzi ya Kilimo. Aidha, kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Wizara ya Kilimo, pamoja na fedha zilizotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo katika mafungu ya Wizara ya TAMISEMI, Maendeleo ya Mifugo, Maliasili na Utalii, Miundombinu na Wizara ya Viwanda na Biashara ni asilimia 5.6 tu ya Bajeti yote ya Serikali.

Kamati yangu inaona kuwa, kasi ya kufikia Azimio la Dar es Salaam linalozitaka nchi Wanachama wa *SADC* kutenga angalau asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali kwa Sekta ya Kilimo ifikapo mwaka 2008 bado hairidhishi. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua thabiti kutenga fedha zaidi kwa matumizi ya Wizara na Sekta ya Kilimo kwa ujumla katika Bajeti zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutumi nafasi kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika - Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Mheshimiwa Christopher Chiza, kwa ushirikano wao mzuri.

Pia, nawapongeza wataalam wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mohammed Mmuya, kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii.

Aidha, natoa shukrani kwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango yao na ushirikiano mkubwa walionipa mimi na Makamu wangu, Mheshimiwa Kidawa Salehe katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi na Ofisi yako hasa Katibu wa Bunge - Ndugu Damian Foka na wasaidizi wake, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Frank Mbumi, Ndugu Daniel Eliufoo na Bi Maria Mwakasege kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imekuwa ni miongoni mwa Bajeti za mwanzo kujadiliwa, napenda kuwatakia kila la kheri Waheshimiwa Mawaziri wote na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili Bajeti za Wizara zitakazofuata.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii . Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Toleo la 2004, Ibara ya 43(5) (b)(c) na 81 (1), napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwako wewe na Naibu wako, kwa kazi nzuri na kubwa ya kuongoza Bunge hili.

Nakishukuru Chama changu cha *CUF* kwa kuniteua mimi kuwa mgombea kwa tiketi ya Chama hicho katika Jimbo la Chambani na hatimaye wananchi kunipa baraka zao kuwawakilisha humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wapigakura wangu wa Jimbo la Chambani, kwa imani waliyoendelea kukipa Chama changu na mimi binafsi kwa kura nyingi. Mimi naahidi kuwa nitafanya kazi kama walivyoniagiza.

Mheshimiwa Spika, wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni tarehe 30 Desemba, 2005 na ile ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa tarehe 6 Aprili, 2006 wakati akifunga Mkutano wa Tatu wa Bunge, walizungumzia sana Sekta ya Kilimo. Ni wazi hii ndiyo ilikuwa tamko rasmi la dira ya Serikali ya Rais wa Nne wa nchi yetu kuhusiana na sekta hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, wengi wetu tuliomo humu ndani, ama ni wakulima au tunatoka katika familia za wakulima. Ni wazi kuwa tunajua nini maana ya kilimo kwa kutambua matatizo yake, mahitaji yake na kuelewa masharti ya kilimo bora na cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Marais wote waliopita wamekuwa wakiongelea suala la mapinduzi ya kilimo. Neno mapinduzi ya kilimo limekuwa kauli mbiu ya kila mwanasiasa wa nchi hii anapohitaji kura za wananchi wetu ambao karibu wote maisha yao yana mahusiano ya karibu na sekta hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wa kujiuliza nini tatizo. Ni mapinduzi gani haya yanayofanyika kwa zaidi ya miaka 45 bila ya mafanikio yake kuonekana. Kila siku tunaongelea matatizo tu.

Mheshimiwa Spika, kukubali kushindwa ni uungwana na siyo kushindwa kisiasa. Wenzetu wa CCM ni lazima wakubali kuwa sekta hii imewashinda.

Mheshimiwa Spika, wakati tukitambua umuhimu wa sera ya ujamaa na kujitegemea ambazo Kiongozi wetu wa kwanza Mwalimu Nyerere alisimama kidete kuzilinda na kuzitetea ingawa muda mwingi alijikuta akiwa yuko peke yake, ni muhimu

kukubali makosa yaliyofanyika katika utekelezaji wa sera hizo. Mojawapo ya makosa hayo ni kuzuia maendeleo ya kilimo kikubwa cha kibiashara kufanywa na watu ama Makampuni binafsi. Hili lilikuwa kosa kubwa na kwa bahati mbaya ndilo limekuwa mzizi wa matatizo ya aibu kama kukosa chakula tunayokumbana nayo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika kilimo unahitaji mtaji wa kutosha na mtaji wa kutosha ni lazima Serikali ikubali kuunganisha nguvu zake na wawekezaji binafsi wa ndani na nje. Taarifa ya mwaka 2004 kuwa uwekezaji wa mitaji kutoka nje inaonyesha Sekta ya Kilimo imewekezwa kwa asilimia 6.7 tu. Ni moja wa ushuhuda wa jinsi gani, sio tu Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilifanya hapo kale lakini bado inaendelea kufanya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sekta Binafsi katika kilimo itakuwa ni ya manufaa makubwa sana iwapo itatekelezwa kikamilifu na kwa uadilifu. Kuwepo kwa Sekta Binafsi kutaendelea kuboresha ushindani kiuzalishaji, ubora wa bidhaa zetu za kilimo na kuleta ajira ya uhakika kwa Watanzania wote bila kujali wanaishi maeneo ya Vijijini au Mjini. Ni wazi hili litasaidia kupunguza hatari inayonyemelea Taifa letu kutokana na hili Jeshi la wasio na kazi katika Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC* kuwa kilimo kitapewa asilimia 10 ya Bajeti ya nchi wanachama. Ahadi hii haikuwa tu kwa kuwaridhisha wananchama wenzetu katika kundi hili, lakini vilevile kwa kutambua kwamba kihitoria kilimo ni Mtanzania na Mtanzania ni kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kutenga asilimia 3.2 ya matumizi yake kwa Sekta ya Kilimo, ambayo ni chini ya ile ya mwaka jana ya 3.9 na huku mfumuko wa bei unazidi kupaa zaidi ya asilimia tano na Shilingi inazidi kuserereka, ni kutoonyesha heshima kwa Watanzania zaidi ya asilimia 60 wanaotegemea Sekta hii. Cha ajabu ni kuwa ndugu zetu hawa ambao tunashindwa kuwapa heshima stahili, ndio wanaochanga asilimia 45.6 katika Pato la Taifa. Serikali inapaswa kutoa maelezo ya kina, ni kwa nini tumeshindwa kutimiza ahadi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Sekta hii umekuwa unapiga *mark time* tangu tupate uhuru wetu. Ni wazi kuwa katika nchi yenye takriban ekari milioni 44 safi kwa kilimo bora, yenye mito mikubwa kama Rufiji, Ruvuma, Kilombero, Pangani na Kagera yenye urefu wa takriban kilomita 2,800, hali ya hewa nzuri kwa kilimo kwa mwaka mzima, watu wapatao milioni 30 wenye nguvu na uwezo wa kulima hata katika mazingira magumu yaliyoje, mapinduzi ya kilimo yanahitaji miaka mitatu tu na siyo zaidi ya miaka 45 kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya karibuni, kumekuwa na mipango mbalimbali tuliyoambiwa inalenga kuinua kilimo chetu. Miradi hiyo ni kama ile ya umwagiliaji ambao lengo ni kuwezesha angalau hekta 405,400 kati ya hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kuendelezwa hadi ifikapo mwaka 2017. Hii ina maana kuwa ziendelezwe zaidi ya hekta 30,000 kila mwaka. Mnamo mwaka 2004, Serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo ilifanya Semina kwa Wabunge ndani ya Ukumbi wa Bunge na

kueleza mpango huo ulioitwa kabambe. Aidha, Serikali ilieleza kuwa itatekeleza mpango huo kwa kutumia fedha za *STABEX.*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 Serikali imepanga kuendeleza ekari 10,000 tu licha ya ahadi yake ya mwaka 2004/2005 ya kuendeleza angalau hekta 30 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo na elimu ndio kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Nne kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni juzi, ni kwanini basi Shilingi bilioni 10.5 tunazoambiwa zipelekwe Mikoani kwa ajili ya wajasiriamali zisiingizwe katika kilimo cha umwagiliaji maji, kitakachoongeza ajira, chakula kwa matumizi ya ndani na kuuza nje na baadaye pesa hizo kurudishwa kwa ajili ya miradi mingine?

Mheshimiwa Spika, lakini cha zaidi ni kuwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla wanapaswa kujua maendeleo ya mpango huo hadi hivi sasa. Watanzania wana haki ya kujua fedha kiasi cha Shilingi bilioni 40 za *STABEX* tulizoambiwa zitatumika katika mpango huo zimetumikaje. Hili linapaswa kufanyika kabla ya kurukia hili la Shilingi trilioni mbili za *ASDP*.

Mheshimiwa Spika, hii ni Awamu ya Pili ya Mpango wa *Agricultural Sector Development Programme (ASDP),* Mpango wa miaka saba utakaogharimu Shilingi trilioni mbili. Kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita, asilimia 75 ya fedha hizo zinakwenda katika Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara ya Kilimo imeonyesha wasiwasi wake juu ya ufanisi wa mpango huu pale ilipotilia mashaka uwezo wa Halmashauri kuhusu matumizi ya fedha na uandaaji wa mipango bora na usimamizi wa mipango ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Bunge lako lako Tukufu likapewa taarifa rasmi kuhusu mpango huo ikiwemo taarifa ya kiasi gani kimeshatumika hadi sasa, kimetumikaje, matatizo yote yanayoukumba mradi huu kuainishwa wazi na kuelezwa ni hatua gani zimechukuliwa na pale ambako kuna uzembe na ubadhirifu wa fedha za mradi huo mkubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia fedha ambazo Serikali imekuwa ikitoa kupitia Mfuko wa Pembejeo upande wa matrekta toka Bajeti ya mwaka 2003/2004 mpaka Bajeti ya mwaka 2005/2006 Bunge lilikwishaidhinisha kiasi cha Sh. 13,141,635,633/= kwa ajili ya matrekta mpya na matengenezo ya matrekta makongwe.

Mheshimiwa Spika, marejesho ya fedha hizo hadi sasa yanasikitisha. Ni wazi wakulima wengi Vijijini ambao ndio wanapaswa kuwa walengwa wakuu, hawajui utaratibu wa kukopa kutoka katika Mfuko huo wa Pembejeo. Matokeo yake, wajanja wachache wanajineemesha na Watanzania walio wengi wanaendelea kuathirika kana kwamba nchi hii siyo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke wazi hadi kwenye ngazi ya Vijiji jinsi mkulima anavyoweza kupata mkopo huo. Ni muhimu Serikali ikawasogezea huduma hiyo wakati msimu wa kulima unapowadia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungependa wananchi wafahamishwe ni matrekta mapya mangapi yalinunuliwa kwa mkopo huo? Nini hali ya umiliki wake? Ni matrekta mangapi ya zamani yalifanyiwa ukarabati na yamesaidiaje walengwa? Ni hekta ngapi zimefikiwa na malengo yalikuwa hekta ngapi? Fedha kiasi gani hadi sasa hazijarejeshwa? Walioshindwa kurejesha ni wangapi na akina nani na hatua gani zimechukuliwa dhidi yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma tuliiomba Serikali ianzishe Vituo vya Matrekta kwenye Kanda mbalimbali, wananchi wakodishwe matrekta hayo. Kama walivyoanzisha Mapadri wa Benedict Mtwara, lakini walikatishwa tamaa na Serikali kwa kuweka kodi kwenye ukodishaji huo wa matrekta yao. Juhudi za watu kama hawa, yaani Mapadri wa Benedict wa Mtwara na Lushoto ni lazima zitambuliwe kwa kuwaongezea pale wanaposhindwa na sio kuja na mipango ya kuvunja juhudi hizo. Watanzania wengine wengi wawezeshwe kuja na mipango kama hii katika kila Wilaya na tarafa za nchi yetu na ni lazima wapewe baraka za misamaha ya kodi mbalimbali wanazokumbana nazo. Hawa ndio wawekezaji wa kweli kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaleta hapa Bungeni kuhusu mpango wake wa kila Mkoa kulima zao moja la biashara na zao moja la chakula. Kwa sasa hatuelewi mpango huu umeishia wapi na kama bado upo, mafanikio yake ni yapi? Ni muhimu Serikali ikatoa taarifa ya Mipango ya aina hiyo ili tujue kama ni endelevu kiasi gani na au ni matatizo yapi yaliyotokana nayo ili iwe kigezo kwa mipango ijayo.

Mheshimiwa Spika, wakulima wadogo wadogo ndio wazalishaji wakuu wa mazao ya kilimo nchini. Lakini kipato chao kinapungua kila mwaka wakati mahitaji yao na gharama za uzalishaji zinaongezeka. Hii inatokana na mkulima wa aina hii kukosa mtu wa kusikiliza kilio chake. Kuendelea kutumia jembe la mkono, kutokutumia mbegu bora, kutotumia mbolea ya kutosha kwa muda muafaka na kutokupata ushauri wa kitaalamu, ni baadhi ya matatizo yanayowakumba ndugu zetu hawa kwa muda mrefu sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika dunia yetu hii ya vyakula halisi, yaani *organic foods*, ndugu zetu hawa ni hazina kubwa kwa Taifa letu. Badala ya kusisitiza ndugu zetu hawa kutumia mbolea za viwandani ambazo kuzipata ni mzigo mwingine kwao, wakati umefika Serikali ikachukua hatua madhubuti na za haraka kuboresha kilimo asilia ambacho ndicho kinategemewa na Watanzania walio wengi ili waweze kukuza kilimo chao na kuweza kuuza bidhaa zao katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Vietnam ambao nao wanategemea kilimo cha wakulima wadogo kama ilivyo hapa kwetu, wameweza kufanya mapinduzi makubwa ya kilimo kwa miaka michache iliyopita. Tunapendekeza Serikali yetu kutuma ujumbe

mahsusi wa wakulima wetu, wataalamu wetu, wanasiasa na hata wanafunzi wetu kusoma siri ya mafanikio yao ya hivi karibuni. Ni wazi tuna mengi ya kusoma zaidi kule, ingawa nchi yetu haina upungufu wa utaalamu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli miundombinu mibovu inachangia kwa kiasi kikubwa kuporomosha bei ya soko la mazao ya wakulima wetu hasa hawa wadogo wadogo. Tatizo la miundombinu ya kusafirisha bidhaa za kilimo katika nchi yetu ni moja ya mzigo mkubwa tunaowapata Watanzania wanaojitahidi kujilimia mazao yao wakitegemea kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wanapopiga kelele kuhusu uzembe wa Serikali yetu katika utekelezaji wa ahadi zake mbalimbali katika Sekta ya Miundombinu, hawaongelei kuwawezesha wao kufika katika maeneo yao tu, bali vilevile kumsaidia mkulima wa Tanzania kuondokana na ufukara usio na kifani. Wakati tunachangia kuhusu miundombinu yetu, suala lisihusishwe na kura za Watanzania tu, bali liangaliwe kwa upeo wa jukumu la Serikali yetu kuwapa moyo wananchi wake kwa juhudi wazifanyazo kujenga Taifa letu, kama vile wanavyojishughulisha kwa karibu na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kukubali kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge ni kusikia kilio cha Watanzania na sio kukubali kushindwa chagizo la Waheshimiwa Wabunge wetu ambao wengi wao huishia kuunga mkono hoja ya Serikali kwa asilimia mia kama ilivyokuwa hapo 2005. Ni dhahiri kuwa Serikali ya CCM, kwa miaka 45 iliyopita imeshindwa kuja na mbinu endelevu katika kuleta maendeleo ya kweli ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, huko zamani tuliwahi kuwa na hekta 450,000 za umwagiliaji maji, lakini kwa sasa zipo hekta 260,000 tu. Kwa miaka kadhaa, sasa wananchi wamekuwa wakiambiwa kuwa wakati umefika wa kuboresha kilimo cha umwagiliaji. Cha ajabu ni kwamba, hata wakati huu ambao tayari janga la ukame limeshatuathiri, bado hakuna dalili yoyote ya mpango makini wa kuboresha kilimo cha umwagiliaji nchini. Hata kwenye mabonde yetu makubwa kama Bonde la Rufiji, Bonde la Ruvuma, Bonde la Malagarasi na mengineyo mengi tu, bado hakuna dalili ya umakini wa kuyaendeleza.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu alituambia, kupanga ni kuchagua. Ni wazi somo hilo bado halijafika barabara kwa Serikali ya CCM. Kutumia mabilioni yote kwa kununua ndege iliyo na matatizo, kama taarifa za hivi karibuni tulizozipata kule Mwanza, kununulia *Radar* ya gharama kubwa ambayo haiendani na mahitaji hasa ya nchi yetu, Mifuko yetu ya jamii kuingia katika miradi yenye mushkeli kama ule wa *Quality Plaza* na kuacha kuwatengenezea barabara wananchi wa Kusini ambao ni wazalishaji wakubwa wa Korosho na Mihogo au kuacha kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani ambayo ingetuondosha kwenye ombaomba ya chakula, ni mfano wazi jinsi tusivyomtendea mema Mtanzania wa kawaida na mzee wetu Baba wa Taifa,

Marehemu Julius Kambarage Nyerere ambaye alijitahidi kwa uwezo wake wote kuwalinda Watanzania wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi wetu, uuzaji bidhaa zetu nje ya nchi yetu ni lazima uwe mkubwa kuliko ununuzi. Kwa hivi sasa Tanzania tunanunua zaidi kuliko tunavyouza japokuwa tuna bahati ya kuwa na mazao makubwa takriban tisa ya biashara ambayo yanahitajika sana katika Soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, takwimu za hadi Aprili, 2006 zinaonyesha kuwa tulinunua bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 4,012.4 na tuliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,919.8. Takwimu zinaendelea kuonyesha kuwa uzalishaji wa zao la Mkonge ulifikia tani 264,000 mwaka 1965 lakini baadaye uzalishaji ulishuka hadi tani 17,793 mwaka 2005. Hivyo hivyo, kwa Tumbaku kutoka tani 51,227 mwaka 1996 hadi kufikia tani 37,982 mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, hii ni mifano michache tu ya kuthibitisha jinsi gani Serikali yetu imeshindwa kuboresha Sekta ya Mazao ya Biashara kwa kiwango cha kuuza nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, korosho ni moja ya mazao muhimu ya nchi yetu ambayo hali ilionyesha wazi kuwa tumeshindwa kuyapa thamani inayotakiwa. Tanzania tuna viwanda 12 vya kubangulia korosho. Kama viwanda hivi vitakarabatiwa, kila kimoja kina uwezo wa kubangua tani 10,000 za korosho. Wakulima wanazalisha tani 120,000 kwa mwaka. Kutokana na mipango isiyo madhubuti, hivi sasa ni wastani wa asilimia tano tu ndio huuzwa zikiwa zimebanguliwa. Hii inatokea tukijua wazi thamani ya bidhaa hii iliyobanguliwa ni Sh. 6,600/= kwa kilo na ile iliyobanguliwa ni Sh.1,105/=.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wa kukubali kuwa mbinu za kubinafsisha viwanda hivyo zimeshindwa kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Mapungufu ya kisera ya kiutendaji katika mpango huo yamesababisha matatizo zaidi na zaidi. Kama tungeweza kusafirisha wastani wa tani 50,000 za korosho zilizobanguliwa, nchi yetu na wakulima wetu wangeweza kujiingizia wastani wa Shilingi bilioni 225, sawa na Dola za Kimarekani 225 kwa bei ya wastani wa Shilingi milioni tano na laki moja sawa na Dola za Kimarekani 5100 kwa tani au wastani wa Sh. 5,100/= sawa na Dola za Kimarekani 5.1 kwa kilo. Kwa kushindwa kuboresha viwanda vyetu, korosho isiyobanguliwa ingeingiza wastani wa Shilingi bilioni 42 tu, sawa na Dola za Kimarekani 42.5 ambayo ni sawa na Shilingi laki nane na nusu tu *(US$ 850)* kwa tani au Shilingi 850 *(US$ 0.85)* kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kushindwa kuviboresha viwanda vya kubangulia na kuongeza thamani ya korosho zetu, tunawanyima wakulima wetu haki ya kupata neema inayoendana na zao hili katika Soko la Dunia na kupoteza nafasi ya ajira kwa vijana wetu wapatao 60,000 endapo viwanda hivi 12 vingefanya kazi inayotakiwa. Kama hivi viwanda vitakuwa na *shift* mbili kama ilivyo kawaida, ajira zitaongezeka na kufikia watu 120,000. Hii ni katika zao moja tu la korosho.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba ni zao linalolimwa na idadi ya Watanzania hasa waliopo katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mara, Kagera, Pwani na Morogoro. Tunaweza kabisa kuondokana na umaskini katika familia na kuongeza Pato la Taifa kama kilimo cha Pamba kitaboreshwa. Ni ajabu kuwa katika nchi yetu ambapo Mikoa mingi inayozalisha pamba inazunguka raslimali ya Ziwa Victoria, tunakumbwa na tishio la kukosa mavuno ya uhakika kutokana na msimu mmoja tu wa upungufu wa mvua. Ni ajabu kuwa tunashindwa na wenzetu wa Sudan na Misri ambao sio tu wanaweza kuzalisha zao hili bila hofu ya ukame unaowazunguka, lakini pia wanazalisha pamba yenye thamani yenye ubora wa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Spika, zao la tumbaku ni zao kuu la biashara na wakulima wa Mkoa wa Tabora, Ruvuma. Ukweli ni kuwa wakulima wameendelea kulima zao hili japokuwa haliwapi faida kwa kigezo kuwa hilo ni zao ambalo waliachiwa na mababu zao. Suala la Muungano wa Wanunuzi wa Tumbaku Tanzania, yaani *ATTT* ambao pamoja na mengi mengine hutumika kubuni unjanja wa kumnyonya mkulima, ni suala la kuangaliwa kwa umakini na kukemewa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria ya Tumbaku ya Mwaka 2001 *(The Tobbaco Industry Act No. 2 /24 2001)* ilianza kutumika mwezi Julai, mwaka 2002; kwa kuwa Muungano wa Wanunuzi wa Tumbaku Tanzania *(ATTT)* ulianzishwa kwa malengo ambayo sasa yanapingana na Sheria ya nchi na mfumo wa biashara huria ambapo wanunuzi kupanga bei ni kinyume cha mfumo. Kwa hili, Kambi ya Upinzani katika Bunge lako Tukufu linataka majibu yaliyokamilika kuhusu yafuatayo:-

(a) *Option* zipi zinazoweza kutolewa kisheria kumlinda mkulima kutokana na unyanyasaji huo wa wazi hasa baada ya tarehe 01 Julai, 2002 ilipoanza kutumika sheria hiyo?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya uhalali wa ushiriki huo wa *ATTT* katika biashara ya tumbaku hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya malengo ya Muungano huo yanapingana na Sheria ya Tumbaku katika kifungu cha 5 (5)?

(c) Ni stahili zipi ambazo mkulima atakuwa nazo pale itakapodhihirika kuwa alilazimika kuendelea kubaki katika biashara au Mkataba wa mtu, au Kampuni ya ambayo haina uhalali au leseni ya kuwepo katika mlolongo mzima wa mawasiliano ya kibiashara hasa baada ya sheria ya tumbaku ya mwaka 2001 kuanza kutumika?

Mheshimiwa Spika, ni aibu kuona kuwa tatizo la zao la mahindi ambalo limekuwa likizalishwa kwa wingi katika Mkoa wa Nyanda za Juu Kusini na ambapo awali Mikoa hiyo ilijulikana kama *Big Four,* limekumbwa na balaa la kuanguka kwa sababu mbalimbali. Kwa hiyo, kwa sasa limepoteza umaarufu wake wa kuitwa *Big Four*. Ni ajabu kusikia kuna wananchi katika Mikoa hiyo wanakabiliwa na njaa. Ni wazi hapa kuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunapaswa kushughulikia na Serikali, ni namna tunavyoimarisha viwanda vya wenzetu huko Ughaibuni kwa kuwarahisishia

uwezo wa kununua mazao yetu kama mali ghafi. Nadharia ya uchumi inatuambia kuwa, Sekta ya Kilimo ikikua itatoa mwanya kwa Sekta nyingine kukua. Hivyo wakati tunafikiria kukuza Sekta ya Kilimo kufikia asilimia 10, ni muhimu vile vile kuboresha ukuaji wa Sekta ya Viwanda na hasa viwanda vidogo vidogo katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa kama tukifikia malengo haya hata kama asilimia saba tu, uzalishaji wa mazao ya kilimo Vijijini yataongezeka. Vile vile bila ya kuboresha miundombinu kama barabara ama viwanda vya usindikaji, mengi yataishia kuendelea kuoza na wakulima kuendelea kugubikwa na umaskini.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kuacha kusingizia Soko la Dunia, kumbe anayewanyonga wakulima wetu ni pamoja na Sera za Kodi zetu wenyewe. Mfano ni zao la karafuu ambalo katika Soko la Dunia bei yake ni Dola 3,500 kwa tani, wakati mkulima analipwa Dola 1,200 tu kwa tani sawa na asilimia 35.7 ya bei ya soko. Hili la kuuza bidhaa zetu zikiwa ghafi ni kuendeleza ukoloni mamboleo ambao tumekuwa tukiupigia kelele kwa miaka minne sasa.

Mheshimiwa Spika, japokuwa Serikali imeongeza ruzuku ya pembejeo kutoka Shilingi bilioni saba katika mwaka 2005 hadi Shilingi bilioni 21 mwaka huu 2006/07, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, sisi tuna wasi wasi kuwa ongezeko hilo huenda likamnufaisha zaidi mfanyabiashara kuliko mkulima mwenyewe. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu mbinu na mikakati itakayotumika katika kusambaza mbolea hii.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iangalie upya jinsi ya kufufua Kiwanda cha Mbolea, kwani hiyo itakuwa ni suluhisho na tatizo la kuchelewa kufika kwa wakulima kwa wakati na bei kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maafisa Ugani, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ifanye mabadiliko makubwa yafuatayo: Kwanza , wawajibike moja kwa moja kwa Wizara wanayoifanyia kazi iwe ya Kilimo, Ardhi, Mifugo, Maji na kadhalika ili mapungufu yawe ni rahisi kugundulika na kurekebishwa.

Pili, wapatiwe mpango wa kazi na nini wanatakiwa kufanya, yaani *terms of reference* kama kilimo ni zao gani wanatakiwa kusisitiza, tofauti na ilivyo sasa kwamba mtu huyo huyo yuko kwenye Mifugo, Ardhi, Kilimo, kwa mazao yote.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, tafiti nyingi zinazofanyika zinabaki kwenye makaratasi na kuwa matumizi ya Serikali kuombea misaada kutoka kwa wafadhili. Lakini walengwa wa tafiti hizo hawapewi tafsiri halisi ya tafiti hizo kwa maendeleo yao. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni kwa namna gani Maafisa Ugani wanahusishwa na matokeo ya tafiti hizo ili wao wazipitishe kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali yetu kushughulikia masuala yafuatayo:-

Kwanza, ni lazima Serikali itambue miradi yote inalenga kilimo ama ile ya Serikali au ile ya wafadhili na iingizwe katika Mipango Mikuu yetu ya Kilimo.

Pili, Serikali lazima itoe maelezo yaliyokamilika kuhusiana na mipango ya miradi yote ya Serikali inayohusu kilimo chetu kwa miaka mitano iliyopita ili ione ni vipi inaendana ama itaendana na miradi mipya ya Serikali ya Rais wa Awamu ya Nne.

Tatu, Serikali lazima ianzishe Benki ya Kilimo nchini itakayowezesha wakulima wa Kitanzania, wakulima wakubwa na wadogo kupata mikopo ya uhakika na yenye riba nafuu. Benki hizi lazima zielekeze nguvu zake zote Vijijini na kuepuka kuwanufaisha wenye uwezo tu waliopo Mjini.

Nne, Serikali ni lazima iangalie kodi zote za kilimo na mazao yake ili kumwezesha mkulima wa Tanzania kujiongezea kipato chake bila kutegemea mfumo wa kodi ambazo haumfikii yeye binafsi.

Tano, mpango wa miundombinu kama barabara za muda mrefu za kiwango cha lami unaondelea hivi sasa utilie mkazo matatizo ya wakulima wetu Vijijini na sio kuunganisha Mikoa tu.

Sita, Serikali ni lazima itilie mkazo suala la upatikanaji wa uhakika wa habari za masoko ya mazao yao, mahitaji ya mazao yao kama pembejeo na matrekta na mfumo mzima wa uvunaji wa vifaa vya mazao ya wakulima.

Saba, Serikali lazima itunge upya Sheria ya Ushirika ili iendane na mahitaji ya sasa kuhakikisha ushabiki wa kisiasa hauruhusiwi kabisa.

Nane, Serikali lazima iwaeleze wananchi kwa mapana yake hatua zitakazochukuliwa kwa wote waliohusika na ubadhirifu katika miaka iliyopita na hivi karibuni na ije na mipango maalum ya kuwajengea imani Watanzania kuhusu ushirika.

Tisa , zao la karafuu libinafsishwe kama ilivyo kwa mazao mengine ya biashara hapa nchini ili pawe na ushindani wa soko utakaomnufaisha mkulima wa karafuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa tunapendekeza mchakato huu wote ufanyike kwa kuwashirikisha kikamilifu wadau wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa Serikali itatumia uwezo wake wote pamoja na raslimali zake zote kuhakikisha kuwa Mapinduzi ya kweli ya kilimo yanafanyika kumkomboa Mtanzania mnyonge. Tunahitaji majibu ya kina katika maeneo yote tuliyohoji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya awali kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Uraia, unakatiza katikati ya Msemaji na Spika, lakini kwa leo nakuachia tu basi uendelee.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya awali kabisa kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Awali kabisa naomba niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Bajeti. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Wizara hii ya Kilimo, kwa Waziri mwenyewe, Manaibu wake wote wawili, pia Katibu Mkuu na Watendaji wake wote wa Wizara pia Taasisi zake zote kwa kazi nzuri ambayo inafanyika hadi sasa kutaka kuhakikisha kwamba Wizara hii inasimamia suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nami pia nichukue nafasi hii kuweza kutoa pongezi zangu za dhati kwa watu mbalimbali tukianzia kwanza kwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata, ushindi wa kishindo kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia kwa kuweza kupata ushindi wa kishindo kwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Pia, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wote, Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Karume, Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa humu ndani wa Majimbo, wa Viti Maalum na wale wa kuteuliwa. Niwapongeze Mawaziri wote walioteuliwa humu ndani. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa na naomba nilete salamu za pongezi kutoka kwa wananchi wa Manispaa ya Iringa, lakini pia wananchi wa Mkoa Ruvuma kwa kukupongeza kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu unayoifanya ya kusimamia na kuiongoza Serikali. Wananchi wana imani kubwa na wanakuombea sana uweze kuwa na afya nzuri wewe na Baraza la Mawaziri na wote ambao unawasimamia katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata maendeleo yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kutoa pongezi kwa Wajumbe wapya wa Sekretarieti ya CCM (Chama cha Mapinduzi) kuanzia Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote. Nami pia nichukue nafasi hii niwashukuru wananchi wa Manispaa ya Iringa kwa kunipa kura za kishindo na kwa kweli nawashukuru sana kwa heshima kubwa waliyonipa ambayo imeniwezesha mimi kuwa Mbunge kwa kipindi cha awamu ya pili na kwa kupitia Ubunge na mimi nimeweza kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. Nawashukuru sana.

Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoionyesha kwangu niweze kumsaidia katika kuongoza maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma. Mimi naahidi kwamba nitashirikiana na viongozi wote wa Mkoa Ruvuma,

lakini pia wananchi wa Mkoa wa Ruvuma katika kuhakikisha kwamba tunasimamia maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo na wewe mwenyewe nikupongeze kwa uongozi wako mzuri. Wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kutuongoza kwa *speed* na *standard* zinazotakiwa. Hakika hatukukosea katika kukuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naomba sasa nianze kuchangia hotuba hii ya Bajeti na kama nilivyosema, naiunga mkono kwa dhati na nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa kweli kitabu hiki kama laiti wananchi wangekuwa wamepata nafasi ya kukisikiliza chote kama ingekuwa sio tatizo la muda hakika wangeona jinsi gani Wizara hii imeweza kupanga mambo yote ambayo yamewekwa kwa ajili ya wananchi wa Tanzania wakulima. Hakika yote kama yataweza kutekelezwa ile Ilani yetu ya Uchaguzi ambayo inasema tunataka kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania inaweza ikapatikana kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa basi na mimi nianzie tu kwanza kutoa pongezi na shukrani kutoka kwa wananchi wa Jimbo langu la Manispaa ya Iringa. Lakini pia wananchi wa Ruvuma wanashukuru sana kwa Serikali kuweza kutoa ruzuku ya mbolea, kutoka shilingi bilioni saba hadi shilingi bilioni 21. Lakini wana ombi.

Ombi hili ni kwamba pamoja na kwamba ruzuku hii inatolewa na kwa kweli na mimi naona hata katika ukurasa wa 52 hapa inaonyesha kwamba kuna mpango mpya kupitia Mpango wa Abuja ambao wanasema kutakuwa kuna kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wasio na uwezo, hapa naona hiki ni kitu kipya na ni kizuri sana ambacho wananchi wenyewe wanazungumzia kwamba kuna watu wengi ambao hawana uwezo, basi Serikali ione kwamba bei ile ya mbolea isipande sana.

Kwa mfano mwaka 2005 ilikuwa Sh. 17,000/=, basi ibakie na mwaka huu iwe Sh. 17,000/= au kama ikiwezekana ipungue zaidi ili wananchi wasiokuwa na uwezo waweze kupata mbolea bila matatizo yoyote. Hii itasaidia sana kuinua kilimo. Kwa sababu kama tukipiga hesabu Sh. 17,000/= kwa ekari moja ambayo inahitaji pengine mifuko mitatu ya kupandia, kukuzia na kuzalishia, basi ni Sh. 51,000/=. Hicho ni kiasi kikubwa sana kwa mtu asiyekuwa na uwezo.

Lakini kama tutaendelea kuibakiza pale au kuipunguza, basi tuna hakika kwamba mwananchi akilima ekari moja na akaweza kutumia *modernization* kwa maana ya kutumia mbolea hizi, basi tuna uhakika kwamba atapata mazao ya kutosha yatakayomsaidia kupata chakula cha kutosha, lakini pia ziada akaweza kuuza ili iweze kuhakikisha kwamba anapata na yeye maisha bora.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, wanachoomba ni kwamba bei hii ya ruzuku itangazwe mapema. Mmekuwa na kawaida ya kutangaza mwezi Oktoba au Novemba. Pale wananchi hawana fedha kabisa! Lakini ikitangazwa mwezi huu wa Julai au Agosti, tuna uhakika wananchi wakati wanauza mazao yao hapa, basi watakuwa na uwezo wa

kutenga fedha kwa ajili ya kununua mbolea na kuiweka ndani wakingojea mvua ziweze kuanza. Tukichelewa zaidi haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba tayari Serikali inaona umuhimu wa kuhakikisha kwamba usimamizi wa utoaji wa mbolea hizi za ruzuku utakuwa unasimamiwa kupitia Mawakala wa pembejeo za kilimo huku Vijijini. Mheshimiwa Waziri anasema ifikapo Juni, 2007 utaratibu huu utakuwa umeanzishwa. Pia, kutakuwa na kuanzisha dhamana ya Kitaifa kwa mikopo ya pembejeo, nadhani ni utaratibu mzuri sana. Pia, kutakuwa na mtandao wa kikanda kununua na kusambaza mbolea, ni utaratibu mzuri sana.

Lakini nina ushauri kwamba tunacho chombo chetu labda na mimi nieleze kwamba nina *interest,* tunacho chombo chetu cha Kitaifa ambacho kimekuwa kikisimamia uuzaji wa mbolea *TFC*. Chombo hiki kiko chini ya Wizara ya Viwanda. Lakini chombo cha Kiserikali ambacho kimekuwa kikisambaza mbolea nchini ni chombo ambacho kina utaalamu wa kutosha, kina maofisi katika Wilaya nyingi nchini na Ma-*godown* mengi, chombo hiki kingetumika vizuri zaidi na kikawa chini ya Wizara ya Kilimo badala ya kuwa chini ya Wizara nyingine ambayo haihusiki na kilimo hasa kwa sababu kiko nje ya kilimo basi upelekaji wa mbolea inakuwa kama vile ni shughuli ya biashara. Lakini kwa kweli ingekuwa ni shughuli ya huduma kama kingekuwa chini ya Wizara ya Kilimo na kikaweza kusimamia chini ya Wizara ya Kilimo.

Kwa hiyo, nashauri sana mpango huu wa Serikali uliokuwepo kukifanya kuwa ni chombo cha kilimo, basi naomba ushauri wangu uzingatiwe ili chombo hiki ambacho kwa kweli kinaweza kutusaidia kusambaza mbolea kwa wakulima bila matatizo yoyote, bila ya upendeleo, bila ya kutokuwa na matatizo kama ambayo yamekuwa yakijitokeza sasa hivi kwamba mbolea haifiki kule inakotakiwa wangeweza kutufikishia.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, naomba niishukuru Serikali kwa ku-*modernise* kilimo kwa kupitia mashamba darasa. Nadhani hii ni njia pekee ya kuweza kutusaidia wakulima. Mashamba darasa haya yameanzishwa miaka miwili iliyopita na katika Mkoa wa Ruvuma nimeyakuta na zaidi sana nimeyakuta katika Wilaya ya Mbinga. Sasa yakienezwa nchi nzima hakika yataweza kusaidia kwa sababu wanatoa utaalamu, wananchi wataona kwamba wanatakiwa walimeje, wawekeje mbolea na wapande vipi, wawekeje mbegu zake na pia watunze vipi mashamba yao na mazao akishapata. Sasa tatizo ninaloliona ni kwamba bado kuna wataalamu wa kilimo wachache.

Katika hotuba ya Waziri, amezungumzia kwamba katika kipindi hiki kutakuwa na wataalamu wengi ambao watapelekwa kusomeshwa. Ninashukuru, lakini kwa kweli naomba iwe *speed* kubwa kwa sababu kama tunataka kilimo hiki kiweze kutuletea mabadiliko, tunayohitaji na tunavyojua kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kilimo sasa ni roho ya uchumi wetu, basi tuweze sasa kukisimamia inavyopasa kwa kupata wataalamu wengi. Lakini wataalamu hawa pia nao nashauri Wizara ifanye sensa kujua ni wangapi ilionao, wako wapi na wana utaalamu kiasi gani. Kwa sababu mnakumbuka kuna kipindi fulani nilikuwa na Kikao pale Songea, Afisa Ugani mmoja akazungumza kwamba yeye anaona kwamba kilimo hiki kinarudi nyuma kwa sababu

kwanza huko siku za nyuma kulikuwa na kuchanganya Wizara ya Kilimo na Mifugo. Sasa unakuta bado wengine wanakuwa na utaalamu wa mifugo sio utaalamu wa kilimo.

Kwa hiyo, wamepelekwa kule upande wa kilimo. Lakini pia walipata mafunzo. Mheshimiwa Waziri anasema nimepata mafunzo ya pamba na kakao. Niko Mbinga nasimamia zao la kahawa. Kwa hiyo, sitendi haki kwa wakulima kwa sababu sina utaalamu wa kuwapa inavyopasa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, naiomba Serikali iwape vitendea kazi wataalamu wetu. Mashamba darasa haya hayawezi kuenea katika nchi yetu iwapo Maafisa Ugani hawana hata baiskeli ya kuweza kuwafikia wakulima. Hili ni tatizo kubwa! Katika Kata nyingine ni tatizo kubwa sana kwa sababu ni eneo kubwa utadhani ni Tarafa. Kwa hiyo, anazunguka kwa mguu, kitu ambacho sio rahisi kuweza kuwafikia wakulima wote na kuweza kuwapa utaalamu unaotakiwa.

Kwa hiyo, naiomba Wizara ione ni moja ya kitu muhimu kuhakikisha kwamba vitendea kazi kama baiskeli, pikipiki zinawafikia Maafisa Ugani ili kwa kweli kuweza kupeleka utaalamu unaohitajika ili kuleta mageuzi ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia ili mkulima apate bei nzuri ya mazao, ninaomba suala hili la stakabadhi ya mazao ambayo imeanzishwa kwa majaribio na Mkoa wa Ruvuma ni moja ya Mkoa ambao uko kwenye majaribio, basi uenezwe katika nchi nzima kwa sababu ni mpango mzuri sana. Mwananchi anapewa stakabadhi, anapeleka mazao yake kwenye *godown* akisubiri bei, wakati huo huo anatumia ile stakabadhi kwenda Benki kupata mkopo ili mkopo ule aweze kuutumia kwa mahitaji madogo madogo anayohitaji. Aidha, kwa ajili ya ada, hospitali au kwa ajili kununua mbolea, lakini wakati huo anajua mazao yake yako kwenye *godown* yakisubiri bei nzuri na wakati akipata anakuwa na uhakika kwamba atakuwa anauza kwa bei kubwa na yeye mwenyewe ataweza kufaidika na kumletea maisha bora. Kwa hiyo, naomba stakabadhi ya mazao iweze kwenda katika Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika Mkoa wa Ruvuma tuna tatizo kwamba stakabadhi hizi za mazao tunatumia Benki. Katika Wilaya ya Mbinga tunatumia Benki ya *Community Bank*. Lakini inavyoelekea sasa Benki hii ya Wananchi haitapata fedha hizi za stakabadhi ya mazao. Ninaiomba sana Wizara ya Kilimo ikishirikiana na Wizara ya Viwanda ambako masuala ya masoko yapo kule, basi waweze kupeleka fedha mapema ili wananchi wa Mbinga kule na wao wakaone kule hakika Serikali yao inawajali na kwa maana hiyo wataweza kulipwa mazao yao au wataweza kupata mikopo kupitia Benki ya Mbinga ambayo wameizoea na ni ya kwao.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, nakubaliana na aliyezungumza Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wake wa 12 kuhusu ushirika. Ushirika huu ukiweza kusimamiwa vizuri, ndio utakaokuwa ukombozi kwa mkulima, ndio utakaokuwa mkombozi kwa mwananchi ili aweze kupata maisha bora. Lakini kama alivyosema, tuna matatizo ya uwezo mdogo au elimu duni ya wanachama kuhusu ushirika. Hilo ni sawa kabisa, lakini pia elimu ndogo tu ya wanachama, pia viongozi wale wanaosimamia ushirika.

Msemaji wa Upinzani amezungumzia habari ya kuleta adhabu kwa wale viongozi walioua ushirika kwa kipindi cha huko nyuma. Mimi naomba kwamba ya nyuma yamepita, tugange yanayokuja. Hii ni Serikali ya Awamu ya Nne, tuanzie sasa kutoa elimu kwa viongozi wa ushirika ili waweze kusimamia vyema ushirika. Lakini pia toeni elimu kwa wanachama kwa sababu, kwa utafiti nilioufanya kwenye Mkoa wa Ruvuma, hakika elimu ya ushirika hakuna. Lakini sio hao tu, Maafisa Ushirika nao hawana elimu ya kisasa ya ushirika.

Kwa hiyo, nao wapewe elimu hiyo. Pia, Maafisa Ushirika wengi waweze kuajiriwa, wapewe vitendea kazi kwa sababu hawana, wanatembea kwa mguu. Sio rahisi kuweza kusimamia vyama vingi vya ushirika ambavyo sasa hivi wananchi wameendelea kuvianzisha mahali pote na kwa kweli tukiweza kusimamia vyama hivi vya ushirika nina hakika vitaweza kutuletea mageuzi mazuri ya kilimo, lakini pia kuweza kuleta maisha bora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nami niungane na wenzangu kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu ambaye sasa ndiyo Mwenyekiti wa Chama kinachotawala ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Niipongeze pia Sekretarieti yake mpya ambayo ameiteua na bila kusahau, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyoipeleka meli hii katika ile nchi ya Ahadi yenye wingi wa asali na maziwa.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana hasa wakati ule wa njaa, sote tumeshuhudia akifanya mambo makubwa. Hakuna mtu ambaye tulipata taarifa amekufa kutokana na njaa. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Waziri Mkuu wa Nchi ya Malaysia mwaka 1981 alipokuwa anachukua nafasi yake kwa mara ya kwanza, alisema, atajitahidi kuitoa nchi yake kutoka kwenye nchi ya ulimwengu wa tatu na kuipeleka katika nchi ya ulimwengu wa pili ndani ya miaka kumi. Kwa kweli baada ya miaka kumi alifanikiwa kufanya hivyo. Sasa ingawa Waziri Mkuu hajasema kwa maneno, kwa vitendo nadhani ndiko anakotupeleka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bila kusahau namshukuuru na kumpongeza Waziri wa Wizara husika na Manaibu Waziri na wataalam wao kwa hotuba nzuri na Bajeti nzuri ya Wizara hii ya Kilimo na vile vile nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na pia nimshukuru aliyetoa maoni ya Kambi ya Upinzani. Nimpongeze sana kwa sababu maoni yake mengi yako kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kuisoma ilani.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, katika nchi yetu kwa kweli suala la kilimo ni jambo ambalo limechukua watu wengi sana ambao wako Vijijini zaidi ya asilimia 70 na tegemeo lao kubwa ni kilimo. Nchi yetu kama tunavyojua ni ya wakulima na wafanyakazi.

Sasa nadhani wakati umefika wa kujitahidi kumweka huyu mkulima aanze kufanana na mfanyakazi. Kwa sababu mfanyakazi mwisho wa siku yeye ana *terminal benefits,* ana pensheni. Sasa huyu mkulima ni lazima naye tujitahidi kumhakikishia kazi anayoifanya sio ya bure.

Mheshimiwa Spika, wakati mfanyakazi anafanya kazi kwa saa saba mpaka nane kwa siku na wakulima kule Kijijini wanafanya kazi wakati mwingine kwa saa kumi mpaka kumi na mbili. Sasa inabidi tujitahidi sana kumwezesha ili anapokuwa anawekeza katika kilimo asione kwamba ni kazi ya bure.

Mheshimiwa Spika, sasa yako maeneo ambayo nilidhani ipo haja ya kuweka angalizo. Nikianza na eneo la kwanza ni kwamba kilimo chetu sio sawa katika karne hii ya utawandawazi. Tunaposema tuna kilimo ambacho kinategemea mvua. Wakati umefika sasa wa kuhama kutoka kwenye mvua na kuwa na vyanzo vingine vya maji ili kuweza kuboresha kilimo. Sasa utakuta wakati mwingine hata hawa wakulima wanavyokwenda kuomba mikopo inakuwa ni ngumu sana. Kwa sababu anaulizwa una-*invest* kwenye nini. Akisema kilimo na *security* yake haieleweki vizuri basi hiyo inakuwa ni shida. Kwa nchi inayotegemea kilimo tusipojitahidi kuwekeza kwenye kilimo inaweza ikawa maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nilidhani ni muhimu sana tukaliangalia ni kujitahidi sekta hii ya kilimo kwa sababu sasa hivi inaonekana sekta isiyo rasmi, sekta binafsi kuifanya sekta hii ikawa rasmi. Kwa hiyo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, iwe na mikakati thabiti kabisa. Tumeandika mambo mengi sana na sisi ni wazuri sana wa kuandika sasa tuhame kutoka pale yale yote ambayo yameandikwa, tujitahidi tupeleke kwenye vitendo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuacha soko la bei ya mazao likategemea nguvu ya soko tunasema soko huria, sio sawa. Bei ya mazao lazima tuwasaidie wakulima wetu. Bei ya mazao hasa katika yale mazao ya biashara wakati mwingine linakuwa *regulated* na soko la dunia. Vitu kama kahawa, korosho na wakati mwingine bei ile inashuka ghafla kwa hiyo Serikali ni muhimu sana ikajitahidi kutenga ruzuku ili tuweze kuwafidia wakulima wetu pale inapobidi, na hivyo itapelekea watu wetu nchini kuwekeza katika kilimo. Kwa sababu sasa hivi kila mtu anakimbia kwa sababu kwanza bei haieleweki na hasa mimi ambaye natoka katika mkoa ambao unalima sana zao la mahindi baadhi ya mikoa michache katika nchini inayolima mahindi na kulisha nchi.

Nakumbuka katika repoti ya hali ya chakula tulioletewa wakati wa kikao cha *briefing* ndani ya nchi yetu ilikuwa ni mikoa sita sita tu ambayo ilizalisha ziada ikiwa ni

pamoja na Mkoa wa Iringa. Sasa ipo haja ya suala la bei inaweza ikawa ni suluhu juu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapokuwa ana-*invest* kwenye kilimo *let say* kama ni mahindi gunia moja sio pungufu ya dola 15 hii ni *obviously* kwamba watu wengi watawekeza katika kilimo. Lakini bei ni kitu ambacho kimeachiwa soko huria. Hilo inawezekana katika nchi ambazo zimeendelea lakini nchi ambayo inaendelea suala la bei ni lazima Serikali, Wizara iweke mkono wake na baraka zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo hata msemaji aliyepita amejaribu kulizungumzia ni suala la mbolea. Mengi yameshazungumzwa na hata katika hotuba zilizopita lakini suala hili la mbolea tuweke mikakati ya kuwa na viwanda vya mbolea katika nchi yetu. Kwa sababu tunatumia sana mbolea kwa hiyo tuweke utaratibu tutafute kama ni wafadhili tuwe na viwanda vya mbolea na kama ni mbolea ya ruzuku basi ipatikane wakati wote isiwe ni wakati wa msimu sijui mwezi wa sita, wa saba na wa nane, mbolea ya ruzuku ndiyo inapatikana lakini baada ya hapo haipatikani, kwa kweli imekuwa ni tatizo sana. Kwa hiyo suala la mbolea tuliangalie ili tuweze kujitahidi kuboresha kilimo kwa sababu pia kilimo kinachangia sana katika *GDP* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kwa kweli ningependa kuchangia ni juu ya Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Wizara hii ya Kilimo ni nyeti, muhimu sana na ndiyo uchumi wetu unategemea sana hapo.

Sasa Wizara isibakie na suala la kuratibu tu, iingie ndani zaidi inaweza ikawa na chombo au idara nyingine maalum ndani ya Wizara ambayo itakwenda kusaidia ukuzaji wa kilimo kwa wananchi wa *perce*. Iache kuratibu tu iende zaidi ya hapo, nadhani ni jukumu la Wizara kufanya shughuli hizo. Lakini pia suala la kutafuta masoko mimi kwa maoni yangu nadhani wananchi wanakuwa wamefanya majukumu yao kwa kiasi cha kutosha. Mwananchi anapokuwa ame-*produce* yeye wajibu wake unakuwa umefika hapo. Sasa suala la kutafuta soko la mazao na tunaposema tuwekeze katika kilimo basi liwe ni suala la vyombo vingine ikiwa ni pamoja na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi katika wageni uliotutambulisha nimesikia umemtaja Meneja wa *Mbinga Coffee Company*. Nikasema huyu Meneja leo ametu-*time* kweli kwenye Wizara hii ya Kilimo na nadhani sio bure kwa kweli, amekuja tumsaidie kutafuta masoko wa-*supply in containers and containers*. Kwa hiyo, tusilikimbie hilo jukumu ni la kwetu. Wananchi wanakuwa wamefanya kazi yao kiasi cha kutosha wamezalisha, wamelinda mazao yamefikia sehemu ambayo inapaswa kufikia. Lakini suala la kuwatafutia masoko na *connection* basi nadhani ni jukumu lake na huyu aliyefika leo asubuhi nadhani tutajitahidi tusimuangushe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la masoko na bei kama nilivyosema tunapoachia wakulima wanalaliwa sana na wafanyabiashara na sasa hivi kule kwentu maeneo ya Iringa utakuta wakati mwingine wanaweka pale juu cha ziada kinaitwa lumbesa. Tuweke na *centers* za masoko ya kilimo kuliko wakulima ambapo wanajitahidi kuuza mazao yao katika majumba. Kwa sababu kule vijiji bado hatuja-*highlight centers* za kuuzia mazao. Matokeo yake wanakuja wafanyabisha hawa wakubwa hasa katika mikoa ya mipakani

kuna mikoa kama Rukwa wanakuja watu wa mipakani, Zambia, Malawi wanakwenda wanawalalia sana wakulima wetu na wakati mwingine wananunua mazao yakiwa mashambani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia kwenye hili suala la kilimo ni suala la viwanda vya *processing*. Tunahitaji viwanda, sio sawa leo hii tunanunua maji ya matunda dola 3, matunda ya maembe, machungwa, wakati machungwa yamejaa Tanga, kwa sababu hatuna mashine za kukamulia maji ya matunda. Matokeo yake tuna *supply* malighafi kwa hiyo yanakuja kwenye boksi kinachofanyika wenzetu wanatuuzia wanasema *trade mark*. Wanakwambia *less calories, less sugar,* wakati tunda lenyewe halina *calories* hata sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilidhani hayo ni maeneo sasa ipo haja ya kuwekewa mikakati. Lingine ambalo hata msemaji aliyepita amelizungumzia ni kuhusu benki mazoa. Nchi kama Bangladesh, India wanawekeza sana kwenye benki mazao. Ni ngumu sana watu vijijini kuwa na pesa na *circulation* ya pesa. Kwa hiyo, kinachofanyika, kwa sababu amezalisha ana mazao ana kwenda ana-*bank* yale mazao yake anapotaka yale mazao yanakuwa yanathamani, anachukua inawezekana ikawa ni pesa au mazao hayo hayo.

Sasa nadhani ndiyo hii mnaiita stakabadhi ya mazao kwa hiyo ni muhimu sana kuwekeza huko na tunavyosema ushirika au hizi *SACCOS* kwa kawaida *SACCOS* na ushirika unatakiwa uweke kianzio. Sasa wananchi wanasema inakuwa ngumu sana hata hicho kianzio mnachosema tuweke hatuna, kwa hiyo tuwasaidie suala la hilo. Kwa sabubu tunaposema nchi inatakiwa kujitegemea kiuchumi bila kujitoshereza kwa chakula hata kujitegemea inakuwa ngumu; kwa sababu tunaendelea kuwa tegemezi.

Nakumbuka nchi ya Marekani kabla ya vita kuu ya kwanza wao walikuwa wanaitegemea sana Canada kwa chakula na ikawa ngumu kufanya baadhi ya maamuzi yake ilikuwa inaitegemea Canada na Uingereza ni mpaka pale walipoamua kusema sasa tunawekeza katika kilimo. Hali ya hewa ikibadilika mkulima anafidiwa bei ya soko la dunia ikibadalika mkulima anafidiwa. Kwa hiyo, kuna kuwa na uhakika wa kuendelea kuwekeza katika kilimo. Vivyo hivyo ni kama China wao walijitahidi kuweka mapinduzi ya kilimo wakiboresha vitu kama matrekta. Kwa hiyo, nilidhani na sisi tuweke mikakati mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye upande wa *donors*. *Donors* tunawashukuru sana kwa kushirikiana nao. Lakini hawa *donors* utawakuta wamejikita sana kwenye *research*. Kwenye *research* ukiangalia unamkuta Japan, Ireland, *European Union* na kwenye *policy* nako unawakuta *World Bank, Basket Fund*. Sasa tuhame hawa *donors* tuwaelekeze waende kwenye masuala ya *irrigation,* kuongeza kilimo moja kwa moja. Kwa hiyo, tuangalie maeneo haya. Maana hata hizi *donors funded projects* wakati mwingine zinakuwa na riba na zile riba kwa kweli zinakuwa ni kubwa; wakati mwingine zaidi hata ya mikopo ya benki zetu.

Kwa hiyo, kwa lugha nyepesi ni kwamba wao wanakuwa wanawekeza, haiwezekani nchi fulani ikawa inajadili mambo ya nchi fulani zaidi kuliko mambo yake. Lakini mkikaa nao mezani unakuta anakuonea huruma. Sasa hapa tutafanya hivi na hivi lakini *of course* tujitahidi sana kuwaomba watusaidie katika kuinua kilimo cha mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu na mimi sasa nimeanza kuwa mzoefu katika Bunge lako Tukufu nisingependa kengele ya pili inikute nikiongea. Baada ya hayo ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze pia kukushukuru kwa tangazo lako ulilolïweka vizuri jana kuhusu kualika Waheshimiwa Wabunge na watu mbalimbali wanaosikiliza kwenda kunywa kahawa ya Mbinga na kuinunua kuipeleka nyumbani. Lengo kuu ni kuhamasisha wakulima, lakini pia kuhamasisha umma wa Watanzania kuwa na mazoea ya kunywa kahawa ili kutanua soko la ndani la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Waziri pamoja na Manaibu Waziri na watendaji wao katika Wizara kwa kazi hii ambayo wameifanya. Lakini ninayo mambo machache ambayo nafikiri wakizingatia wanaweza wakaboresha suala hili la kilimo vizuri zaidi. Mimi naanza kwa kujiuliza kama kweli nchi yetu iko *serious* katika kushughulikia kilimo. Mimi naona ni maneno zaidi kuliko vitendo na unaweza ukaona hata hotuba yenyewe ni kubwa mno, *action* ni kidogo sana.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wakati atakapo kuwa anafanya majumuisho tuone zile *action*. Anaposema asilimia 70 ya wakulima wetu wanatumia jembe la mkono na *only 10 percent* ndiyo matrekta, tuone *action* katika mwaka huu tuna-*move* namna gani kuweza kuongeza hii *percentage* ya wanaolima kwa matrekta na wanaotumia wanyama na kupunguza *percentage* ya wanaotumia jembe la mkono. Ndivyo ilani inavyotutaka. *(Makofi)*

Lakini pia katika ukurasa wa saba anazungumzia juu ya mkutano wa wadau wa mazao mbalimbali ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitisha. Waziri anaelezea na anasema ametoa waraka kwa Wilaya na vijiji mimi ningependa kuona amezungumzia nini huko Wilayani na katika vijiji kuhusu masuala ya mazao na mimi nasema hivi kwa sababu pale kulikuwa na hatua mbalimbali ambazo tulikubaliana zichukuliwe. Kwa mfano, kwenye upande wa chakula kuhusu ruzuku watu wa mazao ya biashara pia wadau walilalamika kwamba wangependa kuona ruzuku hii inakwenda kwenye dawa. Lakini kwenye kitabu kwa bahati mbaya sijaona pengine macho yangu hayaoni vizuri, lakini *emphases* iko kwenye ruzuku ya mbolea. Dawa hakuna na mbegu pia hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu chakula katika ukurasa wa 19 hadi 20 ule. Ukurasa wa 19 Mheshimiwa Waziri anaelezea hatua za kukabiliana na njaa na anazungumzia hatua mbalimbali ambazo Serikali imechukua ikiwemo na kutoa msamaha wa kodi kwenye mahindi yaliyoagizwa nchi za nje na kupunguza ushuru wa forodha kwenye mchele uliagizwa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu kwamba njaa ni *symptom* tu siyo *course*. Sasa kama kwenye *symptom* tunakuwa *very serious* lakini kwenye *course* hatui *serious* hapa kuna matatizo. Kwenye *symptom* tunatoa msamaha wa kodi, wafanyabiashara wanaingiza chakula lakini pia hakuna ushahidi wa kutosha kuonyesha kwamba ule msamaha ulimsaidia mlaji. Je kwa nini sasa Serikali isifikirie kwa wakulima hawa wa Mkoa wa Ruvuma ambako mvua imeonyesha kunyesha kila mwaka na inaonyesha katika mwaka huu watajitoshereza kwa chakula pamoja na mikoa mingine ya Rukwa na Mtwara na Kigoma. Kwa nini sasa mbolea hii ambayo inasaidia kupunguza njaa hapa nchini Serikali isifikirie kuondoa kodi kama walivoondoa kwa hawa wafanyabiashara. Tukifanya hivyo tutaonyesha tunatibu tatizo sio *symptom*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ruzuku hiyo hiyo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inasema, kwa ridhaa yako naomba ninukuu inasema: "Mbegu bora na mbolea ni pembejeo zenye umuhimu wa kwanza katika mageuzi ya kilimo na kuongeza tija. CCM katika kipindi cha ilani hii itazitaka Serikali kuchukua hatua za dhati kuweka utaratibu wenye uhakika wa upatikanaji wa mbegu bora na mbolea na kuzifikisha waliko wakulima kwa kushirikisha Serikali za mitaa, vyama vya ushirika na watu binafsi. Aidha, utaratibu wa Serikali kutoa ruzuku ya mbolea utaimarishwa na kulenga zaidi kwenye uzalishaji katika kilimo kuliko manufaa ya kibiashara pekee." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Waziri imeelezea hatua ambazo wanatarajia kuchukua kuhusu *administration* ya ruzuku. Lakini katika maelezo hayo haimhakikishii mkulima kwamba ruzuku hii itafika katika ngazi ya kata au katika ngazi ya kijiji. Sana sana ukisoma inakuonyesha kama ruzuku hii itafika katika ngazi ya Wilaya. Mwaka ambao tunauzungumzia umekwisha, mwaka huu ilifika katika ngazi ya Mkoa na kwa hivyo bei ya ruzuku hii haikumnufaisha sana mkulima na hasa wakulima wetu kule Mbinga. Je, Serikali inaweza kuja kutuhakikishia kwamba sasa mbolea hii itapatikana katika ngazi ya kijiji. Pia ningependa kujua kuhusu dawa na mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye zao la kahawa ambapo kwenye kitabu hiki cha hotuba inaelezewa katika ukurasa wa 76. Katika mkutano ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu aliuitisha wa wadau wa mazao kahawa ilikuwa ni zao mojawapo ambalo lilizungumziwa kwa kina na katika mkutano ule tulimpa Mheshimiwa Waziri Mkuu na hakika Wizara ilipata *copy* ya mapendekezo ya wadau wengine waliokuwa wamekaa kuhusu zao hili kuhusu Sheria ya kahawa namba 23, pamoja na *regulations* zake za mwaka 2003 ambazo kwa kiwango kikubwa nyingine hazijatekelezwa lakini zingine pia zinakuwa ni *disincentive* kwa zao lenyewe la kahawa. Mimi natarajia na ningemwomba Mheshimimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho angeweza kutuelezea. *(Makofi)*

Kwa mfano, *Tanzania Coffee Board* inatakiwa ifanye *registration* kwa wakulima wote wa kahawa. Mpaka sasa hawajafanya na tulikubaliana katika kile kikao kama wanashindwa basi waziombe Halmashauri za Wilaya waingie nazo mikataba zifanye kazi

hiyo kwa niaba yao. Ziko faida nyingi, faida mojawapo ni kwamba mkulima atatambulika, atafahamika na hivyo kuaminika katika vyombo vya fedha. Kama ambavyo nasema siku zote kule Mbinga iko Benki ya Wananchi wa Mbinga kama wananchi wake watakuwa wameandikishwa vizuri namna hii kuna uhakika wanaweza wakakopesheka. Lakini pia itaweza kusaidia kuongeza ubora wa kahawa kwa sababu kila atakaye kuwa anauza kahawa atakuwa anafahamika.

Lakini pia sheria za kahawa zinaondoa *originality* wanapouza kule kwenye *auction* kahawa ile haifahamiki ni ya nani. Kwa hiyo, *originality* inapotea na ilipendekezwa kwamba hili suala lingerudishwa ili kila mtu anayeuza kahawa afahamike ni nani. Ziko sheria pia ambazo zinamfanya kila mtu akanunue hiyo kahawa kule Moshi hata kama ni ya kwako mwenyewe. Lakini pia tumeona hata katika hotuba ya bajeti wakulima wa kahawa sasa wanahamasishwa kui-*process* hii kahawa sasa ataisindikaje kama sheria hizi zinamzuia yeye mwenyewe kusindika kahawa yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali ijaribu kuangalia hili katika majumuisho i-*come up very clearly*. Lakini pia kuna suala hili la *revenue* ambazo Halmashauri zinaruhusiwa kutoza kwa asilimia tano. Naipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua kwa kufuta ili *contribution* ya mkulima kwenye bodi ya mazao. *(Makofi)*

Lakini pia hili lingeangaliwa maana katika ule mkutano tuliambiwa kwamba imeachiwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuamua kama Halmashauri inaweza kuendelea kutoza hiyo *revenue* ya *five percent* au hapana. Lakini mbaya zaidi kule Mbinga *revenue* inawagawanya sasa wakulima, inawapendelea wengine na kuwaumiza wengine. Inawapendelea wale wakulima ambao wanauza kahawa yao ikiwa shambani na *revenue* wanatoa pale pale. Lakini wakulima ambao wamejiunga katika vikundi vya ushirika na wanapenda kuuza kahawa yao kule Moshi, *TCB* imeingia mkataba na Halmashauri ya Mbinga na *TCB* inakata kule moja kwa moja.

Sasa inamuumiza mkulima kwa maana nyingi sana. Kwanza ile *rate* wanaokata pale wanakata kwa *foreign exchange,* lakini pili pia haiangalii gharama zile za mkulima. Yule mkulima aliyeuza shambani hana *transportation cost,* huyu ana *transport cost.* Lakini haiangalii ina-*charge at turn over*. Hii ni *disincentive* kwa wale wakulima ambao wanataka kuuza kwenye *auction,* lakini pia wanataka kuuza nchi za nje. Pengine *clarification* ingeweza kutolewa ili hawa wakulima wanusurike ili waweze kuhamasika zaidi katika kuuza hii kahawa katika mnada kule Moshi na nchi za nje moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la magunia ya kahawa, kiwanda kipo kimoja tu kile cha Moshi nina habari kwamba kimefungwa kwa hiyo, mzalishaji wa magunia ni mmoja tu. Kwa hiyo, kuna *monopoly* na tatizo la *monopoly* unajua kwenye *price*.

Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie vizuri mkulima huyu wa kahawa analipa kodi nyingi sana na gunia lile lina *VAT* kwa hiyo, wakati Serikali inakuja na lengo hili zuri la kuhakikisha huyu mkulima anapata kipato kilicho bora zaidi kwanza kwa Serikali

yenyewe kuondoa ule ushuru wa bodi za mazao lakini pia ingetusaidia katika uzalishaji wa haya magunia.

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumzia hili katika kile kikao cha wadau, Mheshimiwa Naibu Waziri alisema si vizuri tukaruhusu magunia toka nje kwa sababu tunataka ku-*encourage production* ya ndani. Lakini tunapotaka kuwa na hili lengo zuri la ku-*encourage production* ya ndani tuhakikishe kwamba we *don't encourage at the expence of this poor farmer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba tena kumshukuru Waziri lakini ningepanda sana atoe *clarification* katika mambo ambayo tumeongelea hasa katika hii *Coffee Act* ambayo pia inafanya kule mnadani wanunuzi wanakuwa wachache sana na mbinu nyingi zinatumiaka katika jambo hili. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa mara ya kwanza katika jengo hili jipya la Bunge. Kabla sijaendelea ningependa na mimi pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kuchaguliwa juzi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa salaam za pongezi kutoka kwa wanaweke wa Mkoa wa Morogoro. Ningependa pia nichukue fursa hii kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa pamoja na Rais wetu kuongoza nchi yetu na kwa juhudi zake kubwa za kuboresha mazingira hasa katika Mkoa wetu wa Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kwa kishindo na kwa kufanya kazi ya uhakika kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wanaendelea kuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri Mkuu, kwanza kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu na Bunge hili kumthibitisha kwa kishindo na pili kwa kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba kasi mpya inachukua nafasi yake katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwapongeza pia wale wenzetu wote waliochaguliwa katika sekretarieti ya chama chetu tawala, Chama cha Mapinduzi wakiongozwa na Katibu wao Mkuu, Mheshimiwa Yusuf Makamba, napenda kuwapa salaam za pongeza kutoka kwa wanawake wa Mkoa wa Morogoro.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais, nawatakia kila la kheri katika utendaji wao wa kazi na ningependa pia kuwapongeza Wabunge wote wa Bunge hili kwa kupewa imani na wananchi wa

Tanzania kuja kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu na mimi napenda kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Morogoro kwa kunipa imani kuja kuwakilisha katika Bunge hili Tukufu la awamu ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa salaam zangu hizo ningependa pia nikupongeze wewe. Tumekuchagua kwa kishindo kwa sababu tulikuwa na imani kwamba utafanya kazi nzuri ambayo kweli umeionyesha kwamba unaifanya kwa *speed* na *standard*. Ningependa kuwapongeza Naibu Spika, na Wenyeviti wote wawili waliochaguliwa kukusaidia katika kuendesha Bunge lako Tukufu na wameonyesha umahiri wao. Ningependa kukuhakikishia kwamba wale ni wasaidizi wazuri kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ningependa sasa kuelekea kwenye hoja iliopo mbele yetu ambayo ni hotuba ya Waziri wa Kilimo. Napenda nichukue fursa hii kumpongeza yeye Manaibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri ambayo imekuwa *very scientific* kutekeleza mipango na yanayotendeka katika nyanja za kilimo nchini. Nawatakia kila la kheri kutekeleza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ningeanza kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Baada ya kuunga mkono hoja naomba sasa nizungumze machache. Kabla sijasahahu ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba ameonyesha nia yake ya kuendeleza Mkoa wa Morogoro ili na sisi tuweze kuwa kwenye *big four,* nafikiri kwa sasa itakuwa ni *big five* sio *big four* kama Mkoa wa Morogoro utaingia katika hiyo *sub set*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amesema katika ukurasa wa 56 kwamba kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na usanifu wa skimu 63 katika mabonde ya mito ya Wami na Kilombero Mkoani Morogoro ambayo yana maji ya uhakika na rutuba ya kuwezesha hekta 315,000 kuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimefurahishwa sana kwa sababu Mkoa wa Morogoro zamani ulikuwa ni kati ya Mikoa ambayo ilikuwa inalisha nchi hii. Lakini sasa kwa sababu tumeshindwa kuwa na mipango madhubuti ya kilimo cha umwagiliaji, Mkoa wa Morogoro umeendelea kuwa na matatizo ya kukumbwa na ukame mpaka tunafikia mahali kwa Mkoa kama Morogoro tunaletewa chakula cha njaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ilikuwa ni aibu lakini ni aibu kwa sababu tulikuwa hatukujiandaa na kutengeneza mikakati ya kuanzisha kilimo ambacho kitakuwa ni endelevu na ninaamini kama kweli huu mpango upo, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba usanifu huo unakwenda haraka ili haya mabonde, kama hili bonde la Kilombero linaweza likalisha Tanzania kama kweli mipango madhubuti ya kilimo cha umwagiliaji itakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa mpaka sasa hivi mchele mzuri ambao tunauita tule na bwana unatoka Morogoro na ndiyo sababu wapemba wanakuja kununua. Mchele huu unatoka katika bonde la mto Kilombero. Sasa sambamba na kutotayarisha miundombinu

ya umwagiliaji, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba Mkoa wa Morogoro basi tunaomba na sisi tupewe ruzuku ya pembejeo ambayo ni mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulima tunalima lakini kwa bahati mbaya mavuno yetu siyo mazuri kwa sababu wakulima wetu hawana uwezo wa kununua mbolea kwa bei kubwa. Tatizo lingine kubwa ni utayarishaji wa mashamba.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wengi wamerudi kulima kwa jembe la mkono kwa sababu hakuna matrekta na bei ya kulimiwa kwa trekta ni kubwa. Kwa hiyo, mkulima wa kawaida aliyekuwa analima ekari tatu mpaka tano, anashindwa kulima kwa sababu uwezo hana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili basi kuleta mapinduzi ya kilimo katika huu mkoa ambao una uwezo mkubwa wa kuweza kuchangia katika kupunguza janga la njaa katika nchi hii, naomba Mfuko wa Pembejeo basi uangalie namna ya kuwa wezesha kwa namna ya pekee kwa makusudi kabisa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro tuna mabonde makubwa ambayo wala hayahitaji mbolea, lakini uwezo wa kulima wananchi wetu hawana. Siyo wavivu, huwezi kulima ekari tano kwa mkono na unaona trekta inapita lakini huwezi kuchangia ile bei ambayo wanakuambia na wanapandisha, hakuna *control*. Wanakuambia kwamba leo hapa wanalima kwa 14,000/=, unaenda kwingine 20,000/=, kwingine mpaka 30,000/=. Unauliza kwa nini, wanakwambia kwani wewe mama hujui kwamba mafuta yamepanda bei! *Diesel* imepanda bei. Tunaomba Serikali yetu iangalie namna ambavyo inaweza ika-*subsidise Diesel* ambayo inatumika kwenye matrekta ambayo yanalima vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni lile ambalo mwaka jana Serikali ilikuja na mpango wa kusema kwamba tuwe na zao moja la chakula na tulime pia na zao lingine la biashara. Mkoa wa Morogoro uliamua kulima mahindi, mpunga pamoja na zao la Pamba.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba Mwenyezi Mungu alitupa baraka tukaweza kuvuna Pamba, hususan katika Wilaya ya Kilosa. Lakini ile Pamba nyingi imeozea ndani kwa sababu wanunuzi hawakuonekana. Sababu hatukujua, lakini mpaka sasa hivi kuna Pamba ambayo imeozea ndani kwa sababu hakuna aliyekuja kununua na aliyekuja kununua anakuja kwa mtindo wa bei ambayo mwananchi anaona ni afadhali Pamba hiyo ioze kuliko kumpa yeye, kwa sababu unakuta kwamba gharama za kulima pamoja na gharama za kuhudumia ile Pamba mpaka ije kuvunwa, zinakuwa ni kubwa kuliko ile bei ya yule mtu anayekuja kununua Pamba. Naomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ningependa kuzungumzia zao la Mkonge. Ukiacha Mkoa wa Tanga, Mkoa wa pili ambao unaweza ukazalisha Mkonge kwa wingi ni Mkoa wa Morogoro, hususan Wilaya ya Kilosa. *(Makofi)*

Naomba niseme kabisa wamba Wilaya ya Kilosa, walio wengi walikuwa wanategemea sana zao la Mkonge, aidha, kwenye kufanya kazi mle au kuweza kupata

kuendeleza biashara zao kutokana na wale wafanyakazi waliokuwa wanakuja kufanya kazi katika mashamba ya Mkonge. Sasa kuna ambao wamenunua yale mashamba, badala ya kuyaendeleza yale mashamba sasa wanakodisha watu wanalima mahindi mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona ile mikonge ipo tu, inazidi kufa, hakuna anayevuna, hakuna anayefanya nini. Lakini nimejaribu kusoma humu, nikafikiri labda kutakuwa na mkakati mkubwa kabambe wa kuweza kufufua zao la Mkonge hasa katika Mkoa wa Morogoro, sijaona kwa bahati mbaya. Mimi naomba Wizara itupie jicho Mkoa wa Morogoro katika harakati za kufufua zao la Mkonge kwa sababu lile zao lilikuwa ni uchumi hasa katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kuona kwamba Mheshimiwa Waziri ameandika juu ya mazao mapya. Sasa haya mazao mapya ameyazungumzia. Lakini ningefurahi kuona kwamba kati ya haya mazao aliyoyaainisha katika hotuba yake, angetueleza kwamba haya mazao yanastawi vizuri katika maeneo gani, kusudi wananchi wa maeneo hayo sasa waanze harakati za kujitayarisha au mchakato wa kuweza kulima hayo mazao kama njia mojawapo ya kupunguza umaskini na kumuongezea mkulima kipato.

Mheshimiwa Spika, hii kama itafanikiwa kwamba wakulima wanakuwa na mazao ya uhakika ya biashara, wakulima wanaweza sasa wakawa na uwezo wa kuhifadhi chakula cha kutosha badala ya kuuza chakula chote ili waweze kupata mahitaji yao muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye hifadhi ya chakula. Kila mkulima angependa kuhifadhi chakula chake ili aweze kula kwa mwaka mzima. Lakini uwezo wa kuhifadhi kutokana na wadudu waharibifu, haupo. Haupo kwa sababu dawa nyingine ambazo tunaletewa za kuhifadhi mahindi, sijui zinaongezea basi hata ile *speed* ya kuliwa na wadudu. Lakini mwananchi au mkulima anaona kwamba kuliko kuweka yale mahindi yaje kuharibika, ni afadhali ayauze, aje kununua chakula. Sasa katika mtindo huo, basi anafikiri mwenzake amewekeza, kumbe hakuna anayeweka, kila mmoja anauza. Wengine tunauza, tunacheza ngoma kwa sababu ni afadhali ukauza ukacheza ngoma ya mtoto wako kuliko kuyaweka hayo mahindi yaje kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sasa utafiti unaofanywa kama alivyoainisha Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kwamba utafanyika utafiti ambao utamsaidia mkulima kujikomboa na matatizo yanayomkabili. Tatizo kubwa ni hifadhi ya mbegu za chakula hasa mahindi ni tatizo kubwa pamoja na maharage. Naomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu masoko ya mazao yanayoharibika kama nyanya, nyanya chungu, matunda hasa machungwa na mananasi kutoka Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga na Mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa niishukuru Serikali kwamba imeonyesha nia kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko kujenga masoko ya wakulima wa

matunda katika eneo la Segera ambako watakuwa wanatoa huduma kwa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga pamoja na Morogoro na watajenga Soko la Nafaka katika eneo la Makambako. Watatoa huduma kwa Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa pamoja na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoiomba Serikali ni kwamba tusitamke tu na kuwapa wananchi matumaini, basi tukisema, tutende kweli. Haya masoko, tunaomba kwamba tujue yatajengwa mwisho wake na ni lini yataanza kufanya kazi. Tupewe muda maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia kwenye hiki kitabu kuangalia kwamba namna gani Wizara inashirikiana na Vyuo Vikuu ambavyo vinashughuli za Kilimo kama *SUA*. Pale *SUA* kuna kitengo cha kuhifadhi chakula, lakini mimi nashangaa kwamba kile kitengo kiko pale kinafanya *Research* za *Academic experience* tu. Mimi naomba Wizara itafute mchakato wa kuweza kushirikiana na Vyuo Vikuu tulivyonavyo. Vinapofanya utafiti wa mbegu, utafiti wa hifadhi na usindikaji wa vyakula. Mimi ninaamini kwamba Chuo Kikuu cha Sokoine kikipewa mkakati wa kuhakikisha kwamba kinatayarisha wananchi wa Morogoro na Mikoa mingine namna ya kuhifadhi matunda yanayoharibika hususan machungwa na mananasi, nafikiri Serikali yetu itakuwa imepata faida kubwa kutokana na hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mfuko, hizi hela ambazo zimetengwa kwa ajili ya *Research*, naomba hizi hela Wizara badala ya kuzitumia ndani ya Wizara kwenye *Research* ambazo nyingi zinaishia kwenye *shelves* zetu. *Research* zinafanyika, tunaona wanafanya *workshops,* zinatoka kwenye magazeti, tunaona kwenye Televisheni, baada ya hapo hatua ya ku-*move* kutoka pale sasa *from the shelf* kwenda kwa mkulima, haipo. Sasa hawa wataalam wetu tunawafaidi namna gani kuboresha maisha ya mkulima ambaye anatoka jasho pia alimsaidia akaweza kusoma? Naomba Wizara ijenge mahusiano mema kati yake na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na vyuo vyetu vikuu hususana Chuo Kikuu cha Sokoine cha Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie huduma za ugani. Huduma za ugani hazipo kabisa vijijini. Akienda bibi kilimo kule au bibi shamba tunavyomwita, anaenda kulima mahindi yake. Analima mahindi. Ukimuuliza, anakwambia sasa nifundishe nini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa nafasi hii nipate kuchangia kwenye hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Lakini kabla sijafanya hivyo, ningependa nianze kwa kufanya la kiungwana. Kwanza kabisa ni kutoa pongezi zangu za dhati kwako wewe mwenyewe kwa nafasi hiyo, kwa Waziri Mkuu na Baraza zima la Mawaziri na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kufanikiwa kufika hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa wale ambao wako nje ya Ukumbi huu, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Kwanza, nimpongeze kwa kura nyingi alizozipata, lakini pia kwa kukiwezesha chama chake kuingiza Wabunge wengi sana katika Bunge hili. Lakini, pia nimshukuru mimi mwenyewe binafsi kupitia uteuzi alioniwezesha nikawa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza nimsaidie kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mengi unaweza ukazungumza kwenye Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini nimeamua nijikite kwenye mambo matatu tu. Nizungumzie tumbaku kidogo, halafu nigusie pamba na muda ukiniruhusu, nitazungumzia *Nyanza Corporative Union(NCU)* ya Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri Mkuu kwa juhudi aliyoifanya pale alipoanza kuitisha mikoa mbali mbali nchini, Dar es Salaam pale na kufanya mikutano na wadau wa mazao makubwa haya yanayolimwa hapa nchini likiwemo zao la Tumbaku na Pamba. Mkutano wake wa tarehe 17 Mei, 2006 tulizungumzia Tumbaku na suala kubwa lililojitokeza ni je, nini tufanye ili tuweze kuongeza uzalishaji wa Tumbaku kutoka kwenye hizi kilo za sasa hivi takriban milioni 55 twende kwenye kilo milioni 100 ifikapo mwaka 2010. Mazungumzo yalikuwa mengi, mchango ulikuwa unafaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini moja lilijitokeza bayana kwamba hapa akitazamwa mkulima vizuri, hakika mengine yote yatakuja yatachukua nafasi yake. Sasa namna nzuri ya kumtazama mkulima ni kupitia kwenye bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei ya mkulima wa Tumbaku haifai, ni hafifu, iko chini sana. Nitajaribu kuonyesha baadae kwa tarakimu, lakini uzoefu unaonyesha mkulima wa Tumbaku anapata asilimia 35 tu au chini ya hapo ya bei ambayo ni ya faida ya wale ambao wanakwenda ku-*process* hiyo tumbaku hapo baadae. Nitaonyesha baadae kwa tarakimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme utakapompatia huyu mkulima bei nzuri, basi itampa motisha na lile la pili litatokea kwa sababu huyu atakuwa anataka kutengeneza pesa kwa hiyo na yeye atajua hakika ili apate pesa nyingi, lazima azalise tumbaku kwa wingi, lakini ili pia apate tumbaku kwa wingi, kwa ufanisi mkubwa atataka atumie utaalam zaidi ili uzalishaji wake katika eneo dogo uongezeke mara dufu. Sasa hapo hiyo itakuwa ni sehemu ya pili ambayo Serikali imekuwa inafanya na nadhani itatakiwa kufanya kwa bidii zaidi. Kuna njia mbali mbali mojawapo ikiwa ni kupitia kwenye huduma hizi za ugani kwa kuhakikisha kwamba wataalam wanakuwepo wa kutosha na wanafanya kazi ipasavyo. Lakini pia la pili ni kuhakikisha kwamba masoko yanakuwa ni yale ambayo yanamsaidia mkulima ambaye vinginevyo hana taarifa na uwezo wa kusaidiwa na mtu mwingine yeyote mbali ya Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa bei ya mkulima ndiyo tunasema mimi naiona kama ndiyo *prime mover* ya kuongeza uzalishaji. Lakini ndani yake humo nadhani lengo letu ni hawa wakulima wafikie hali bora katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, sasa naweza pia nikasaidia, hii bei ya mkulima inapandaje! Mimi naona kuna sababu kubwa mbili, kuna ile ya nje ya nchi yetu na kuna zile za ndani

ya nchi yetu. Sababu za nje ya nchi yetu, hizo hatuna sana uwezo nao kwa sababu hizi zinahusu hilo Soko la Dunia ambako sisi hatuna uwezo wa kulidhibiti hilo soko la dunia lenyewe. Lakini tuna uwezo wa kudhibiti yale ya ndani. Kwa mfano, tunafanya nini kushusha gaharama za uzalishaji za mkulima! Tunamwangaliaje mkulima katika kumpunguzia mizigo ikiwa ni pamoja na kuondoa kodi zile ambazo kama inawezekana kweli ziondolewe. *Cess* kwenye Halmashauri au hata kama *Cess* basi itaenda basi imrudie kweli huyo mkulima. Lakini vile vile kuna gharama zingine kama za usafirishaji, unamsadiaje mkulima.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna hili lingine la ruzuku ambalo hakika linafanywa dunia nzima. Ruzuku unampelekeaje na kwa njia zipi mkulima wa Tumbaku. Hili la ruzuku nadhani watekelezaji wakuu wake ni wawili, ni Serikali kwa upande mmoja na kwa upande wa pili ni watengenezaji wa bidhaa za Tumbaku, watengenezaji wa sigara. Hawa wawili wana nafasi kabisa ya kutoa ruzuku hii. Wanaweza wakaketi wakaangalia utaratibu ama mmoja mmoja kila mmoja kwa utaratibu wake. Lakini ni bora kama utaratibu huo utakuwa *coordinated,* utakuwa unasimamiwa kwa utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano ambao nadhani utasaidia katika hili la ndani hasa hasa kupitia hii ruzuku. Haya mengine niliyoyataja ya kushusha *production cost, Cess* na kodi yenyewe yanajieleza vizuri na nafikiri Mheshimiwa Waziri anaweza akayaangalia vizuri sana kama ambavyo ameanza kuyaangalia kwenye mazao mengine kupitia kwa mfano Pamba. Kwenye Pamba kuna makato mengi yameondolewa ambayo makato hayo kwa kuondoka kwake yanaongeza kile ambacho mkulima wa Pamba anafikisha nyumbani kwake. Nadhani hata kwa Tumbaku vile vile yako ambayo wanaweza wakayaangalia.

Mheshimiwa Spika, kwenye Gazeti la *Daily News* la tarehe 22 Machi, 2006 Kiwanda cha Sigara *(TCC)* walitoa taarifa yao ya mapato ambayo kwa kweli ukiangalia hii unaweza pia ukaona ni jinsi gani unaweza kumsaidia mkulima wa Tumbaku.

Mheshimiwa Spika, nilisema kuna kilo kama milioni 55 sasa hivi za Tumbaku tunazozalisha kwa mwaka, lakini inasikitisha kwamba wastani wa bei ya mkulima wa Tumbaku ni shilingi 950 tu. Sasa hapa nataka nitoe hesabu kidogo, hawa Kiwanda cha Sigara peke yake inasemekana wananunua asilimia 10 ya hii Tumbaku. Sasa chukua asilimia 10 ya hizi kilo milioni 55, utapata ni kilo milioni 5.5 kutoka kwenye hizo, Serikali ilipata shilingi bilioni 59 kupitia *Exercise Duty* na *VAT* na kodi ya shilingi bilioni 7. Hiyo inafanya jumla ya shilingi bilioni 66 ambazo zimekwenda Serikalini kutoka wa *TCC* peke yake. Hivyo kwa kilo milioni 5.5, Serikali ambapo nimesema ilipata shilingi bilioni 66, ni sawa na kusema pia kwamba Serikali ilipata shilingi 12,000/= kwa kilo moja na awali utakumbuka nimesema mkulima amepata shilingi 950 wastani wa kilo na hapo bado hujakata makato ambayo natakiwa kuyalipa. Kwa hiyo, hapo inaonyesha kuna nafasi hapo ya kumsaidia mkulima kutoka Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nikihamia upande wa watengenezaji wa bidhaa zenyewe na kwa maana hii hawa *TCC,* wao walipata *net profit* kutoka kwenye hiyo *5.5 million kilograms*. Walipata *net profit* ya *17 billion* au kwa maneno mengine hiyo ni

shilingi 3,000 kwa kilo moja, faida, naongelea faida. Lakini mkulima alipata shilingi 950/= kwa kilo na hapo bado hajakatwa makato.

Mheshimiwa Spika, sasa utaona kwamba haya maeneo mawili kwa hakika yanaweza yakamsaidia sana mkulima. Nadhani hilo linatosha kama utangulizi, lakini nafikiri taarifa hii inaweza ikafanyiwa kazi vizuri zaidi kwa kujenga hoja hiyo hiyo ya kumpatia ruzuku mkulima ili huyu naye apate maisha bora kama ambavyo tunatarajia maisha bora yawafikie Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mengine ya kiutendaji ambayo yanaweza pia yakashughulikiwa katika kuendeleza kumsaidia huyu mkulima wa Tumbaku kama yale ya kuhakiki mizani. Bado vurumai ambazo zinatokea kwenye sakafu za mauzo. Pamoja na Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001, bado kuna matatizo hapa yanatakiwa kuendelea kutatuliwa. Lakini zaidi ya hapo kuna kifungu kabisa, kwa mfano kifungu cha 17 kwenye hii sheria ya Tumbaku na kifungu cha 18(2), zinaweza zikaendelea kutumika vizuri ili kumsadia mkulima kupata haki yake katika sakafu ya mauzo.

Mheshimiwa Spika, naona muda unakwenda, nihamie kwenye lingine. Mkoa wa Mwanza kama ilivyo Mikoa mingine, Shinyanga, Tabora, Pwani na mingine mingi wanalima Pamba. Katika kulima Pamba, mojawapo ya mafanikio makubwa sana katika kilimo hiki ilikuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Ushirika ambao uliendelea na ukawa Mkubwa sana kama vile *Nyanza Cooperative Union*. Lakini tunavyozungumza hivi *Nyanza Cooperative Union* ina matatizo makubwa. Tulikuwa na kikao cha kuteua wanunuzi wa Pamba hivi majuzi, *Nyanza Cooperative Union* ilibidi tuwaweke kando kwanza si kwa sababu hatutaki wanunue, la hasha! Kwa sababu tunataka wanunue lakini katika mazingira ambayo yatawasaidia pia wakulima wa Pamba.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna mambo kadhaa ambayo mimi naamini, pamoja na hali ambayo *NCU* inayo sasa hivi, mimi bado nina nia ya kuisaidia *NCU* na namuomba Mheshimiwa Waziri na watu wake wote wanisaidie tusaidiane, tuwasaidie *NCU* wanunue Pamba. Wasiponunua Pamba itakuwa ni *catastrophe*. Ni *machinery* kubwa, huwezi kui-*maintain* bila kufanya biashara. Lazima isaidiwe ifanye biashara. Usipoisaidia ikafanya biashara, basi umeisukumiza kwenye kifo. Mimi nasema hivi kwa sababu ni chombo kikubwa, kina heshima yake. Kimeanzishwa na watu wenye heshima zao, wamefanya kazi nzuri. Kama tutaiacha *Nyanza Cooperative Union* katika hali hii maanake tumei-*condemn* ife. *(Makofi)*

Mimi ningependa tuizike kwa heshima kubwa, tuifilisi. Tutumie taratibu zote zilizopo, tuifilisi, na hilo mimi mwenyewe silipendi. Kwa kweli mtachukua kazi kubwa sana kuni-*convice* kwamba tunaweza tukaifilisi *Nyanza Cooperative Union*. Ninaloliona ni kuisaidia hii kurudi na ifanye biashara. Ina matatizo mengi, ninakubali hivyo, lakini kuna njia za kuisaidia. Nimeangalia Sheria ya *The Coorperative Society's Act 2003*, ina vifungu vinavyoweza kutumika kuisaidia hii Nyanza ikarejea kwenye biashara. Kwa mfano, kuna vifungu ambavyo anaweza kuvi-*invoked* Waziri mwenyewe, lakini kuna vifungu mbavyo kwa mfano kifungu cha 67(1), kinaweza kuwa-*invoke* na *Registrar* akatengeneza *Care Taker Committee* ambayo ndiyo tunaitaka iende ikasaidie pale

kufanya biashara lakini Waziri pia anaweza akasaidia na pale anapoona yeye yuko mbali, sheria inamruhusu anaweza akamsukumia Mkuu wa Mkoa akafanya hilo. Nataka ni-*declare* hapa kwamba kwa kweli sisi tumejiandaa na tunafanya kazi mchana na usiku kuona *Nyanza Coorperative Union* haizami bali inarejeshwea uhai wake ifanye bishara iuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ana wataalam wengi sana pale Wizarani kwake na nashukuru amekuwa akitusaidia pamoja na hawa wataalam wengine wamekuja kule Mwanza. Wanafanya kazi nzuri na wanaendelea kufanya kazi na nina imani watampatia taarifa nzuri, lakini nataka nimkumbushe, msimu wa kununua Pamba umeanza jana na hatuwezi kuendelea kusubiri kama tunataka kuisadia Nyanza, wakati ndiyo sasa. Kama hatutaki, basi tuamue vile vile, sasa hivi tuizike Nyanza kwa heshima, jambo ambalo mimi naliogopa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya niliyoyasema, napenda nisiendelee sana kwa sababu muda nao hauniruhusu sana. Lakini nirejee tu kwa kusema kwamba nia ya Serikali kupitia bajeti yake hii ya kwanza katika Serikali hii ya Awamu ya Nne ni njema, juhudi zinaonekana ziko thabiti, maelezo yanaonekana na mengine yanatakiwa na najua yapo. Mimi naunga mkono haya na mimi kama Mbunge natoa ahadi ya kuipatia ushirikiano kamili ili yale ambayo yamekusudiwa yafanyike kwa wananchi wetu yatekelezwe tufikie hilo lengo la kuwasaidia wakulima wafikie maisha bora na wao kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana! Ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda uliosalia hautamtendea haki yeyote ambaye ningeweza kumwita kuchangia. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala ya Bunge atoe hoja ya kuahirisha Bunge kabla ya muda wake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, muda uliobaki hauwezi kutosha kwa mchangiaji mwingine. Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lisitishwe mpaka saa 11.00 jioni. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimearifiwa kwamba naruhusiwa tu kusitisha kabla ya muda. Lakini mimi napenda kutumia demokrasia, kwa hiyo naomba muamue hii hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa )*

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo na mimi leo niweze kutoa changamoto kidogo kwenye Wizara hii.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na leo na mimi niko katika Bunge hili. Lakini wa kwanza kuwashukuru ni wapigakura wangu wa Jimbo la Igalula, wamenipa imani kubwa sana kwa kipindi kingine kuweza kunichagua kwa kishindo pamoja na *corrugation* zilizokuwepo, lakini nikaibuka mshindi na kuwastaajabisha waliokuwa wananipinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais kwa ushindi mkubwa ambao tumeupata Chama cha Mapinduzi, kupitia kwao na pia nimpongeze Waziri Mkuu, kwa kuweza kuibuka na ushindi mkubwa sana katika Bunge hili. Tunamfahamu ni kijana mchapakazi, mpenzi wa watu na mpenda kazi. *(Makofi)*

Pia nimpongeze ndugu yangu Spika, kwanza kwa kurudi katika jimbo lake la uchaguzi la Urambo Mashariki. Naamini wana Urambo bado wanahitaji huduma zake na upendo wake kwao na hapa pia tumethibisha kwamba Wabunge, tuna imani naye, ni mtu ambaye kakulia kwenye kazi na mchapakazi. Nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Anne Makinda na nyie Wenyeviti pia niwapongeze kwa kuchaguliwa kwenu na hasa wewe Mwenyekiti ndugu yetu ambaye umemudu na tunajivunia sana kuweko kwako katika nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Mawaziri na Manaibu Waziri, kwa kuteuliwa kwao. Wafahamu kwamba kazi hii ni mchezo wa kijiti, kupokezana. Kwa hiyo, wamepokea vizuri na waendeleze vizuri ili Awamu ya Nne ionekane kwamba ina ma-*reference* wazuri na wachapakazi, watii, wapenda kazi na wenye heshima kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa Wizara kwa kuwasilisha maelezo yao ya Wizara, sina wasiwasi naunga mkono hoja. Lakini tu naomba tu nizungumze machache katika kuboresha na kuweza kuwasaidia katika utendaji wao wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora ni Mkoa wa kilimo, unalima mpaka matunda. Hatuwi sawa na Tanga, lakini matunda yetu ni maembe, maembe mengi sana pale na bahati nzuri tuna Kituo cha Utafiti cha Tumbi. Kinachofanya pale ni kutafuta matunda ya porini kutengeneza *juice* na ambayo watalii wakifika pale wanayapenda sana. Kuna Ntalali, kuna ukwaju na kadha wa kadha. Lakini yanaishia pale pale, sidhani kama Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, inafahamu kituo hiki kinafanya nini na utafiti wao unaishia wapi. Kwenye maonyesho ya kilimo tu ili tuweze kunywa wenyewe au kueneza utafiti huu nchi nzima na pia kuendeleza kutoa matunda haya mbadala katika nchi zingine.

Lakini pia tuna tumbaku na pamba. Limeongelewa na wenzangu lakini kwa kuwa jimbo langu la uchaguzi la Igalula wanalima tumbaku, wanalima na pamba. Lakini

ulimaji huu sidhani kwamba utawaletea mabadiliko ya uchumi. Wanakuwa watumwa wa tumbaku kutokana na mikopo wanayoipata pembejeo na kutokana na wana ushirika kutokuwa waaminifu wale viongozi wa ushirika hasa watendaji. Mkulima anakopeshwa pembejeo ya laki nane, anakuja anakatwa zote ataanzaje sasa? Maafisa Ushirika hasa wa Wilaya yangu ya Uyui wamekaa miaka na miaka nimelizungumza katika vikao vya chama, katika vikao mbalimbali hata kwenye kikao cha Waziri Mkuu, alichofanya kwa viongozi wa tumbaku na pamba. Nimelizungumza sana sidhani kama Wizara imelichukua na kulifanyia kazi.

Naomba hizi Wizara mbili ziwe na mawasiliano ya karibu kwa utendaji, ili wananchi wafaidike na manufaa ya hii Wizara. Watendaji wako chini ya Halmashauri TAMISEMI. Utakuta Afisa Ushirika anakaa miaka kumi katika kitu kimoja hafanyi lolote hawasaidii wana ushirika kwa lolote lile zaidi ya kuwadai madeni ambayo wanashindwa kulipa na kila mwaka mkulima wa tumbuka anakuwa mtumishi anakuwa kikongwe wa kilimo cha tumbaku. Sasa kama ushirikiano hamna kati ya Wizara na TAMISEMI nini maana ya kuwa na watumishi ndani ya TAMISEMI ambao wanasaidia wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza katika vikao mbalimbali maafisa kilimo, kuna kata yangu moja, kata ya Kizenge, Afisa Kilimo amekaa miaka 20 kila Mkurugenzi anayekuja atahamishwa anazidi kuoa, ana watoto mpaka wajukuu keshapata. Kazi hiyo ya kilimo katika kata ile hafanyi chochote, haendi kwa hawa wakulima. Sasa tunaleana au kakaa pale kwa ajili ya kuonekana kwamba hiyo nafasi imepata mtu?

Naomba sana Wizara hii mshirikiane na TAMISEMI hata kama ukikaa sana katika Bunge, si wanakuambia kwamba umezeeka aje Mbunge mwingine, sasa sembuse hawa watendaji inakuwaje miaka 20 kituo kimoja, kijiji kimoja. Si katika vijiji, si katika kata, watendaji hawaondewi, akiondolewa kata hii anapelekwa kata hii wakati hakuonyesha ufanisi wowote wa kazi. Sasa hicho kilimo mnasema kwamba tutahakikisha kwamba kila Mtanzania atakuwa na maisha bora ikiwa hali yenyewe ni hii watalaam wetu, nani atakayemsukuma mwenzake? Mwisho wana kijiji wanakuwa watalaam kuliko hata huyu ambaye tumemweka na kumlipa mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mshikiriane na TAMISEMI mfanye *reshuffle* waliopo wamekaa muda mrefu kiasi ambacho wamekuwa wenyeji, wana vijiwe vya pombe, wana wake mle mle ndani, wameolewa mle mle. Sasa unafikiri atamkemea nani pale? Kila mmoja shemeji yake, rafiki yake, mkwewe, shangazi yake. Ingawa kuna ufanisi kufanya kazi mahali pa nyumbani lakini basi inategemea kada ya kazi yenyewe. Naomba sana Maafisa Kilimo hasa katika Jimbo langu bado hawafanyi kazi zao zaidi ya kukaa kuwa wenyeji katika maeneo hayo. Hakuna tumbaku itakayokuwa nzuri wala wakulima watapata faida yoyote hata kwenye pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba inalimwa si muda mrefu katika Jimbo langu. Lakini *SHIRECU* ambao tunawauzia bado hawawalipi walimaji wa pamba katika jimbo langu. Sasa utamwambia leo akalime pamba, anasema siwezi ndiyo maana wanaondoa pamba, wanalima mahindi kwa ajili ya chakula. Kwanza hakuna *incentive,* pili hakuna

watalaam wa kuweza kuwasaidia watu hawa. Sasa huu uchumi kwa mwananchi huyu hatakuwa nao kama hali hii ya utendaji itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuwa Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira, alishughulikia sana mavazi ya bwawa shamba. Akaja Mheshimiwa Anna Abdallah, yeye akashughulikia ushirika. Sasa na wewe ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, ukisema utachagua moja Wizara yako ina mambo mengi, naomba uende nayo pamoja ionekane kwamba kweli Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, imepata mtu siyo mtu kapata Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakujua wewe mchapakazi, ni *veteran* katika utumishi na ni mkulima hodari katika maeneo yako, basi tafadhali eneza ukulima wa kisasa, wa kisayansi katika majimbo yetu ya uchaguzi na hasa ukiwa wewe mwenyewe Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukulima wa tumbaku unapigwa vita na mambo mawili, matatu, moja tumeridhia mikataba kwamba tumbaku inaleta athari kwa binadamu watu wasivute Tumbaku. Mimi mwenyewe nimekuwa Naibu Waziri wa Afya, nimekuwa nikihubiri kabisa kwamba msivute tumbaku lakini wakati ule ule tumbaku ni zao la biashara hasa katika Mkoa wa Tabora. Lakini wakati ule ule tumbaku ya Tabora inatumia kuni nyingi kupata tumbaku ya kukausha. Lakini wakati ule ule Wizara ya Maliasili na Utalii inasema kwamba tusikate miti.

Sasa kama hali hiyo Mkoa wetu wa Tabora hauna uchumi mwingine wowote zaidi ya tumbaku na pamba kidogo. Asali inatoka kwenye miti, miti ile inapandwa kwa ajili ya kukaushia tumbaku. Miti ile inakatwa hatupati mbao na ni Mkoa wenye mbao nzuri inayotengeneza *furniture* mpaka kupeleka nje. Sasa msuguano huu wa kutokukata miti, msuguano huu kwamba tumbaku ilimwe ikaushwe kwa miti, mbadala gani Waziri anatazama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana Tabora wakiacha kulima tumbaku, halafu hatuna kiwanda, ikiwa usafiri wenyewe wa taabu, barabara kama hivi jana amesema zinaota mbawa, reli ndiyo hiyo inataifishwa, viwanda vya ndege hamna, tumefungwa katika kisiwa, uchumi haupo, tumbaku ndiyo hii ambayo ni aina ya kukausha na moto tunaambiwa tusikate miti na ni kweli tusikate miti kwa sababu itakuwa jangwa kama Shinyanga au na Mwanza. *(Makofi)*

Sasa mbadala gani mmefanya utafiti ili Wizara hii itatusaidia, waendelee kupata uchumi wao watu wa Tabora, wajikwamue katika maisha ikiwa tumbaku ndiyo zao kubwa lakini mikwara, lina mizengwe lina malumbano ya kutokukata miti? Tumekaa tunafanya utafiti pale Tumbi sijui utafiti gani ambao unasaidia Mkoa wa Tabora au unasaidia tu Wizara kujua mnawafanyia kitu gani.

Lakini Chuo cha Utafiti Tumbi, hakimsaidii mwana Tabora. Naomba sana Wizara hii, iangalie maisha ya mwana Tabora, tumbaku na pamba kwa mizengwe iliyopo na ushirika ambao wana ushirika wenyewe hawatusaidii unaanzishwa ushirika lakini uendelezaji wake kila siku ni malumbano katika vyama vidogo vidogo vya msingi kwa

sababu watalaam wetu hawapo. Wanaishia *WETCO* basi ikusanye tumbaku. Ndiyo maana sasa kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha hawakulima tumbaku na kuelimishwa namna gani ya matumizi yao ndiyo maana tumbaku inatoroshwa anaweza kutoka hapa akauza Urambo badala ya Igalula, akatoka Igalula akauza Sikonge au akatorosha kabisa akaja akauzia hata Morogoro kwa sababu hakuna mtu aliyemsaidia jinsi gani aishi na ukulima huu wa tumbaku asiharibu misitu wakati ule ule aweze kuendesha huu ushirika wake kwa sababu wana ushirika hawapo. Wana ushirika wetu wa Wilaya wamechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna ushirikiano mimi nafikiri hamuwatakii heri watu wa Jimbo la Igalula. Naomba sana muweze kushirikiana kiutendaji, siyo Wizara iwe peke yake na watendaji wa Halmashauri wawe peke yao. Maamuzi ya kusema kwamba tujikwamua kiuchumi hayatakuwepo, mwananchi huyu atabaki peke yake, ushirika haupo na Wizara haipo. Sasa hicho mtaipataje kama huyu mkulima hataweza kupata nafasi ya kupata elimu na kueleweshwa nini afanye katika kujipatia uchumi ambao tumeupigia makelele katika Awamu ya Nne, kwamba kila Mtanzania awe na mahali pa kukaa awe na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho jimbo la Igalula bado lina njaa. Tuliahidiwa kwamba awamu ya pili itapita watu wachache waliopata chakula, lakini kuna maeneo karibu nusu ya jimbo bado wana matatizo. Naomba siyo Mikoa mitano tu iliyotajwa katika kitabu kwamba ndiyo wameanza kugawa, kinatoka chakula Shinyanga kinapita Tabora kinakuja Dodoma au kitoke Dodoma kinakwenda Kilimanjaro. Tabora bado tuna njaa, naomba sana wanaofanya utafiti waendelee kufanya utafiti lakini tayari watu wana njaa. Kama kuna njaa amani hakuna, utulivu hakuna. Naomba sana lirudiwe tena zoezi la kugawa chakula, nusu ya jimbo langu wananchi wana njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nashukuru na naunga mkono hoja, naomba ushauri niliotoa wauzingatie na mimi pia nipate taarifa kabla sijarudi jimboni ili niweze nikajibu hoja hizi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita msemaji wetu wa pili ambaye ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa heshima naomba niwatambue wageni wa Wizara ya Miundombinu kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao kwa umoja wao wako wakiongozwa na Brigedia Jenerali Adam Mwakanjuki, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuna Ndugu Salim Senga, Katibu Mkuu Wizara hiyo hiyo ya Mawasiliano na Uchukuzi, Ndugu Abdallah Juma na Ndugu Abdulla Mohamed. Tunashukuru sana kwa kuja kushirikiana nasi jioni ya leo. *(Makofi)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kidogo hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nianze na mimi kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kama Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi. Ushindi ule alioupata unaonesha dhahiri kwamba CCM tuna mshikamano, naipongeza sana, nawapongeza wote waliochaguliwa kwenye sekretarieti wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mheshimiwa Yusuf Makamba. Lakini vile vile nimpongeze sana

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya inayoonekana ya kuiongoza Serikali. Nimpongeze Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti, niwapongeze kwa ujumla wetu Waheshimiwa Wabunge wote tuliomo ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tena kuwashukuru tena wananchi wa Jimbo langu la Handeni, kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao na naendelea kuahidi kwamba tutafanya nao kazi kwa pamoja ili kuleta maendeleo katika jimbo letu. Nichukue fursa hii haraka haraka niwakumbushe Madiwani wenzangu wa Kata za Jimbo la Handeni tuendelee na utaratibu wetu wa kufuatilia miradi kama ile ya *TASAF*, *MMEM* na *MMES,* miradi katika sekta ya afya na miradi katika sekta ya kilimo, ambayo mingine imezungumziwa katika hotuba ya leo na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ili tuweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia mia. Ni hotuba nzuri imeeleza mambo mengi kwa upana wake. Kama walivyosema wenzangu wengine ni kwa sababu tu ya muda lakini hotuba hii ingeweza kusikika yote kwa ujumla wake ingewafaidisha sana wananchi ambao wangesikiliza kwa ukamilifu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imeleta changamoto, kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Hotuba hii imezungumzia mageuzi ya kilimo, imetaja mambo ya *green revolution*. Lakini hoja hizo hizo zinazojiendesha kwenye hotuba hii zinatakiwa ziiguse vile vile Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika lazima wafanye sasa mapinduzi. Lazima wawe ni *think tank* ya kuona ni jinsi gani kilimo kitaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi ya kiuchumi inasema kwamba katika uzalishaji tunahitaji ardhi, nguvu kazi na mitaji kwa maana ya *(labour, land and capital).* Kwa hotuba hii inaonekana wazi kwamba Serikali, imejitahidi kwa uwezo wake kuona kwamba inasawazisha kile kigezo kilichokuwa na mapungufu kwa maana ya kigezo cha mitaji. Huu ni ushahidi mwingine wa kutuelezea Waheshimiwa Wabunge, ni fedha kiasi gani zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu za Wilaya, ili kuleta maendeleo. Kwa hiyo, *challenge* inabakia pale pale kwamba bado kuna haja kubwa ya kuimarisha usimamizi wa fedha katika Halmashauri zetu za Wilaya. Mimi nina hakika kabisa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kama inafanya kazi kitaalam kabisa hotuba hii itaweza kutusaidia katika kuendeleza kilimo na kukifanya safari hii kichangie vizuri katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi sasa tujiulize wapi ambapo tunataka kuparekebisha ili kilimo chetu kiendelee vizuri na kuhakikisha kwamba rasilimali na fedha zote zinazokwenda kwenye sekta hii tunapima na matokeo yake. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, lazima tupime *value for money*. Kwa sababu hizi ni fedha nyingi sana na zinakwenda kwenye ngazi za Halmashauri za Wilaya hadi kufikia vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko haja kubwa ya kuliangalia kwa mapana yake suala zima la *modernization* ya kilimo. Hili Waheshimiwa Wabunge wote wamelizungumzia. Asilimia ya wakulima ambao wanatakiwa wafuatilie kilimo cha kisasa ni lazima tuiongeze. Lakini changamoto nyingine aliyonayo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo,

Manaibu na Wataalam wao waelewe kwamba kilimo ni sekta mtambuka *(is cross cutting)*. Sasa saa nyingine unajiuliza Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa hotuba hii nzuri je, amewasiliana na sekta nyingine kwa mfano sekta ya miundombinu, sekta ya maji, sekta ya viwanda, mambo ya barabara? Kwa sababu hata kama tukipeleka ruzuku ya kutosha kama ilivyoonyeshwa kwenye hotuba hii, lakini bado wakulima wanapolima wanahitaji huduma nyingine ambazo zitawasaidia katika kuendeleza kilimo chao, kukuza ajira zao na kukuza mapato yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kama wananchi wanalima vizuri lakini barabara si nzuri, hicho kinakuwa ni kikwazo. Kama wananchi wanalima mazao yao na soko halijakaa vizuri tunaelewa kwamba hicho nacho ni kikwazo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vizuri Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ikafanya jitihada za makusudi kujaribu kuratibu yale yanayotokea kwenye Wizara ambazo moja kwa moja zinachangia sekta ya kilimo ama sivyo tutashindwa kupima matokeo kutokana na rasilimali tulizoziweka katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mdogo tu, Jimbo la Handeni sasa hivi ndiyo *green basket* ya Mkoa mzima wa Tanga. Tunalima mahindi mengi, ukichanganya na Jimbo la Kilindi, tatizo ni usafiri. Sasa hata kama watapata pembejeo, mbegu bora, kama barabara bado hazijaangaliwa vizuri hilo linakuwa ni tatizo ambalo linatakiwa lifuatiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepita kipindi kigumu sana. MheshimiwaWaziri Mkuu alitumbia juzi hapa, sitaki kusema kama alivyosema yeye moja kwa moja, lakini nataka kusema nilivyomwelewa, amesema sisi Wabunge hebu tuangaliane, halafu umwambie Mbunge mwenzako bwana mimi sina chakula, hebu naomba chakula. Sasa hiyo akaitafsiri kwa ngazi ya Kitaifa akasema ni aibu kubwa kwa Taifa kukimbia hapa na pale kuomba chakula, ambayo ni kweli kabisa. Hilo ni la msingi kabisa. Sasa niliposoma kipengele cha tahadhari ya njaa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri imenipa wasiwasi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ambalo lina watu karibu milioni 35 haiwezekani tukawa tunazungumzia *strategic grain reserve* za tani 110 au 150 haiwezekani kabisa. Nchi nyingine wenzetu wao kwa kutumia teknolojia ambayo ni kawaida tu wanakuwa na *strategic grain reserve* ambayo inaweza kudumu miaka mitano, Uchina nasikia inakwenda mpaka miaka 10. *South Africa* ni kama miaka mitano hivi. Teknolojia hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyokuja hiyo programu ya umwagiliaji maji na nikamsikia Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, anasema wataanza na *design,* ni muhimu sana tukaingia katika mkakati wa kuimarisha hifadhi za chakula kuanzia kwanza ngazi za Wilaya. Tuhakikishe kwamba kila Wilaya *at least* inaweka hifadhi ya kama tani 5,000 mpaka 10,000 ili njaa inapotokea tusimuone tena Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, tukamuona Mheshimiwa Rais wetu anakimbia huko na huko kuomba fedha za chakula na kadhalika, fedha tulizopata kwenye chakula zingeonekana kwenye misaada ya chakula humu kama tungezitia kwenye hifadhi ya chakula tungekuwa tumepiga hatua kubwa sana. Sasa hotuba hii inasema kwamba tumejitosheleza na chakula, mimi napata

wasiwasi sana labda watalaam wa kilimo wataniambia tunajitosheleza kwa chakula kwa mwaka huu au tunakwenda kwenye lengo la kujitosheleza kwa chakula Kitaifa? Maana kuna suala la *food self sufficiency.* Sasa hili sijui linatafsiriwaje? Lakini naona tafsiri iliyotumika katika hotuba hii bado hatujafanya Tanzania tuwe katika kujitosheleza kwa chakula. Kwa hiyo, ni eneo ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri nalo aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika uwekezaji mkubwa katika kilimo. Hatuwezi kuendelea bila *investment drive* katika kilimo hasa miradi mikubwa, hatuwezi. Lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba uzoefu tunaonyesha tunapopata *investors* katika kilimo kikubwa bado wanapambana na tatizo la urasimu, bado wanapambana na tatizo la kutotoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati fulani tulipata mwekezaji wa kiwanda cha maembe hapa, alihama alikwenda Msumbiji kwa sababu hilo linajulikana tunalizungumza sana. Lakini sasa hivi yako maeneo kule Handeni kuna maeneo makubwa sana ambapo wawekezaji wanaonyesha *interest* ya kuwekeza kwenye miwa, kuwekeza kwenye jatrofa, taratibu zinafuatiliwa lakini zinachukua muda. Sasa zinapochukua muda namna ile inawezekana wale wawekezaji wakachoka, wakaenda kuwekeza mahali pengine. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo namuomba Waziri alitupie jicho ambalo ni *locust*.

Programu zote kama nne zinapeleka fedha ngazi za Wilaya, *Agricultural Sector Development strategy, District Agricultural Sector Investment, Participatory Agricultural Development and Employment.* Namuomba Mheshimiwa Waziri aone ni utaratibu gani kama Wizara ikisaidiana na Wizara ya Fedha itafuatilia fedha hizi hasa kuona matumizi yake kule vijijini zinazokwenda, kule Wilayani zinazokwenda. Ule utaratibu wa Wizara kutoa fedha kwenda kwenye Halmashauri na nakusema kwamba kazi yangu Wizara imekwisha, baada ya *Accounting Officer* kutoa zile fedha nadhani huu ni utaratibu ambao inabidi tuuangalie upya. Wizara ndiyo inayotafuta fedha, Wizara inapata taabu, fedha zetu zinapokwenda kule basi ifanye jitihada ya kuzifuatilia mpaka kule. *(Makofi)*

Mwisho nilitaka kutoa tu kama angalizo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba katika vile viwanda vilivyobinafsishwa kimetajwa kiwanda cha *TANGOLD* katika Mkoa wa Tanga, kiwanda kile hakipo. Yaliyopo pale ni magofu, kwa hiyo, hata kama tukiweka kwenye rekodi kwamba kuna kiwanda, hakuna kiwanda. Nilitaka kuweka hilo angalizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena kuunga mkono hoja hii na ni jukumu letu sisi Wabunge, jukumu letu Watanzania, jukumu la Wizara na Serikali kuona kwamba mipango hii ya Kilimo tunaiendeleza ili tupate maendeleo katika maeneo yote na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii nzuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Lakini kwanza naomba nikupongeze wewe mwenyewe Mwenyekiti, kwa kukalia kiti hicho. Wachache wanaokalia kiti hicho kwa kweli. Naomba na wananchi wapiga kura wa Peramiho basi mwaka 2010 *inshallah* wakuchague tena kwa sababu hawakukosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Manaibu Waziri pamoja na Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii nzuri yenye matumaini. Niseme moja kwa moja kwamba naiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuzungumzia ushirika. Ukurasa wa 13 inasomeka kwamba ushirika ndiyo njia kuu ya uwezeshaji kwa wananchi walio wengi. Ushirika ni njia ya kukusanya nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Mkuu wangu wa Mkoa alizungumzia Chama cha Ushirika cha Nyanza. Nafikiri alieleweka kama Mkuu wa Mkoa na Mbunge. Naomba sana Serikali kwa sababu Nyanza ina historia yake. Leo unapoambiwa kwamba Nyanza haiwezi kununua pamba kwa msimu huu kwa kweli inasikitisha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Leo kama ingekuwa inawezekana Marehemu Paul Bomani afufuke, Mwalimu Julius Nyerere afufuke akute kwamba Nyanza leo haiwezi hata kununua pamba ni aibu kubwa kweli kubwa kweli kweli kwa sababu Nyanza ndiyo siasa ya Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla. Naomba sana Serikali suala hili la Nyanza lisimamiwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia la pili, katika kitabu hiki ukurasa wa 11 mwisho pale, inasema kwamba Vyama vya Ushirika vinakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo *bullet* ya kwanza ubadhirifu wa fedha na mali za wanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana kuna jengo liko Mwanza kwa bahati nzuri nilimwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu jengo lililoko Mwanza ambalo lilikuwa linadaiwa shilingi milioni 42 la *KAUMA*. Lakini cha kusikitisha thamani ya lile jengo ni shilingi milioni 600 mpaka shilingi milioni 700. Lakini likapigwa mnada kwa shilingi 72 milioni. Mali ya Ushirika, hata kama ingekuwa namna gani jengo la thamani ya shilingi milioni 600 lipigwe mnada kwa thamani ya shilingi 72 milioni. Naiomba Serikali suala hili iliingilie, kama yapo matatzo basi taratibu zifanyike. Hatuwezi kuachia mali za ushirika ziteketee. Wahusika nafikiri wapo, basi mkondo uchukue utaratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naomba nizungumzie Bodi ya Pamba na kwenye Bodi ya Pamba, yapo matatizo. Nafikiri hata Rais alisema kwamba mtu anaweza kukaa mahala hata miaka 15 na bahati nzuri mama yangu amesema pale. Viongozi Wakuu wa Bodi ya Pamba ni kama vile pale Bodi ya Pamba wana hatimiliki ni mali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawataki hata kutoka, naiomba Serikali kwa utaratibu wake mzuri watolewe pale. Kwa sababu yapo matatizo mengi na makubwa. Serikali inasema vingine na wao wanasema vingine. Kwa mfano kwa upande wa makato ya pamba, Serikali ilisema hivi, mnamo tarehe 28 Juni, 2005 Serikali ilijadili kuhusu kulazimisha majukumu, kazi na upatikanaji wa fedha za kugharamia Taasisi na Asasi zinazohusika na mazao ya kilimo na kuamua kwamba wakulima wasitozwe ushuru kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza mazao, wakulima wasitozwe. Msimu umeanza jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti yao wameweka kipengele kimoja, kinasema *sources of income, farmers contribution* shilingi 20/= kwa kilo moja. Hivi nani Serikali, Bodi ya Pamba au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mmeamua kwamba wakulima wasitozwe makato. Leo wanakatwa makato. Tunakwenda wapi, tunamsaidia nani na mimi ningeshukuru zaidi kama makato hayo yangeweza kutumiwa na yule anayekatwa, lakini pesa hizo hazitumiwi wala hazionekani. Matokeo yake mbegu zinazokuja ni kidogo, madawa yanayokuja ni mabovu yasiyokuwa na ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunaendeleza zao la kilimo cha pamba, hatuendelezi, tunaididimiza, hata hizi takwimu wanazotoa hizi mimi nina mashaka nazo.

Lakini kwa kweli mimi naomba Bodi ya Pamba na mlisema katika swali langu kwamba Bodi ya Pamba ni mzigo. Watolewe pale, wawekwe watu wengine, wasimamie zao la pamba Mkoa wa Mwanza, Shinyanga, Tabora mikoa 12 wanalima pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mzigo mzito na si kila mzigo mzito apewe Mnyamwezi na wao wabebe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie hali ya kilimo. Hili nilizungumzia hata katika bajeti iliyopita. Asilimia 70 ya wakulima wanatumia jembe la mkono, asilimia 20 wanyama kazi na asilimia 10 matrekta. Tunasema kilimo ni uti wa mgongo. Kwa hali hii ya asilimia 10 matrekta, asilimia 70 jembe la mkono hata kama tukifanya namna gani kama hatutaweka jitihada za kusema kwamba tununue matrekta, tufanye sababu za makusudi, tupeleke matrekta ili kusudi yakapanue kilimo, majira yameshabadilika, tuseme tu wanyama kazi, wanyama kazi hao ni sawa sawa na jembe la mkono. Kwa mfano katika ruzuku sijui kama Mkoa wa Mwanza utakuwa umepangiwa shilingi ngapi ruzuku ambavyo mimi sijawahi kuona Mkoa wa Mwanza, chukua shilingi milioni 2 au milioni 1 kwa kuanzia, ile pesa ya ruzuku iende ikanunue matrekta, kama nchi yetu tunaweza tukaruhusu watu kuagiza mitumba ya magari, hivi hatuwezi tukaruhusu watu wakaagiza mitumba ya matrekta kwa bei ya nafuu? Hiyo itasaidia kuongeza kilimo na kupanua kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la ugani. Katika Wilaya yangu ya Kwimba, Majimbo mawili, Sumve na Kwimba tuna vijiji 111. Nilitoa takwimu siku ile kuhusu utunzaji wa chakula, namna ya kulima na kupanda pamba, mtama na mahindi.

Tunahitaji Maafisa Ugani ili kilimo kikue, lazima elimu itoke kwa Maafisa Ugani ipelekwe kwa wakulima. Bila Maafisa Ugani hatuwezi kuendelea. Naomba Wilaya yangu ya Kwimba, naomba Mheshimiwa Waziri yuko pale, najua ni msikivu mzuri, ananisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyikiti, naomba Maofisa Ugani 84. Tunataka kwenda kuchapa kazi ya kupanua kilimo. Umwagiliaji, jumla tunazo hekta 29 milioni lakini tumeambiwa zinazotumika ni hekta 249 tu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais amemchagua Mheshimiwa Christopher Chiza kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni changamoto kwako Mheshimiwa Rais hakukosea. Sasa nakuomba usimwangushe Mheshimiwa Rais, kilimo cha umwagiliaji tunataka tukione ndani ya miaka mitano uwe umekwishaonyesha matunda ya umwagiliaji. Tunalalamika njaa, maji tunayo mengi sana. Kwa hiyo, naomba sana ili kilimo chetu kiwe cha tija na bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kengele ya kwanza imeshalia, sitaki nigongewe kengele ya pili. Lakini msisitizo wangu ni kwamba Bodi iondoke. Makato haya yasikatwe tena. Kwa sababu mmeshakaa na kukubaliana sasa inasikitisha sana kuona kwamba bado wanaendelea kukata, wakulima wameshaanza kufika kwangu tangu jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Nikushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuwa msemaji wa pili jioni ya leo na mimi niungane na Wabunge wenzangu kukupongeza kwa nafasi ambayo umeishika kwa kweli unaihimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwapongeza wote waliopata nafasi mbalimbali nilipochangia hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba niende moja kwa moja kwenye mchango ambao nimedhamiria kuchangia kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema napongeza kwa hotuba nzuri ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kama nilivyokuwa nasema mimi ni mdau mmojawapo wa kilimo labda katika Wilaya zingine zote ambazo zinalima. Lakini nimekuwa nikiguswa sana kwa uchungu kwamba hotuba unapozisoma kwa miaka yote zinakuwa ni nzuri sana. Lakini unapokuja kuangalia kile ambacho kinapatikana huko kunakolimwa hasa sisi huko vijijini siyo kile ambacho kinasemwa ndani ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tunayozungumza ni Awamu ya Nne ya Serikali ambayo iko chini ya Chama cha Mapinduzi, Waziri Mheshimiwa Joseph Mungai, ni Mtaalam wa Kilimo na ameshika Wizara hii siku za nyuma, naamini

yaliyoandikwa huku ndiyo yatakayotekelezwa kwa kipindi hiki cha mwaka huu mmoja wa Bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze Naibu Waziri wa Ushirika, kwa sababu alikuwa kwenye nafasi hii na sasa amehamia chini ya Wizara hii, ninaamini ataendeleza yale yote ambayo ameyafanya Naibu Waziri wa Ushirika na mimi naomba nianze huko huko kwenye ushirika kwamba tatizo bado hatujasikia, hatujaona kwamba Ushirika ina-*perform* vipi katika nchi yetu na ndiyo maana Waheshimiwa wengi wakichangia wanasema hatujapata. Watu wanaogopa kuingia kwenye Ushirika kwa sababu hawajaona tayari kwamba faida ya ushirika huu inayopatikana. Sana sana utasikia kuibiwa. Utasikia haifanyi vizuri watu wanachanga michango yao inaibiwa. Inaliwa na wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa naguswa kwamba ni miaka mingi, mwaka juzi nafikiri tumepitisha sheria mpya ya ushirika ambayo ilikuwa inarekebisha mapungufu yote ambayo yalikuwa kwenye ushirika. Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ni shahidi ametembelea Wilaya yangu na ametembelea ushirika nyingi sana ziko zaidi ya 12 ameziona na taarifa ameziona na migogoro mingi ameshiriki kutatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wasi wasi wangu ni kwamba je, hii sheria tulipoipitisha hawa watu kweli wanajua mabadiliko ya sheria za ushirika? Na ni mwaka mmoja umepita tulikuwa tunajaribu kuona kwamba je, wanaushirika wenyewe wamepata elimu ya sheria mpya? Na viongozi ambao wameshikilia hizo nafasi je, wanaelewa? Kwa sababu tulisema kwamba nafasi za kitaalamu kama Uhasibu itangazwe ili waweze kupata mtaalamu ambaye ana *qualifications* za kuweza kutunza mali za ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mambo yamekuwa yakienda kwa Kanda, ukimwuliza Mkuu wa Ushirika anasema sasa tuko Kanda ya Magharibi, je tutafika? Kwa hiyo, mimi nilikuwa tu naomba niseme tu nichukue nafasi hii, kwa Wizara hii kwamba sasa wakati umefika, kwa sababu ushirika ndiyo tegemeo letu sisi Watanzania tukiungana pamoja ndiyo tutaleta maendeleo kwa haraka. Sasa wapite basi kuhakikisha kwamba elimu inafanyika kama ilivyokuwa Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi imetolewa elimu kwenye Wizara na sehemu mbalimbli kwa wadau wote wajue kwamba utaratibu wa manunuzi ukoje na utaratibu wa kutunza fedha ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na hii Sheria ya Ushirika itiliwe kipaumbele kutoa mafunzo. Kwa sababu watu wamezihodhi hizi nafasi ukisema wafanye uchaguzi na wafuate utaratibu hawafanyi. Bali wanataka kuendelea kushikilia nafasi na ninaamini ni kwa sababu tu elimu hii haijafika kwao. Kwa hiyo, ni changamoto kwamba sasa tuanze kazi kama mlivyosisitiza kwamba ushirika utapewa kipaumbele. Sasa elimu ianze kwanza ili kusudi taratibu zote ziweze kufuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji tumekuwa tukisema kwamba ndiyo peke yake kitakachokuwa kinaleta kilimo cha uhakika kwa Tanzania na ndiyo kitakachotuondolea kwenye janga la njaa lakini vile vile

tunategemea kwamba kilimo ndicho kinachochangia asilimia kubwa sana kwenye Pato la Taifa na mfano tu ambao ninao kwenye Wilaya yangu, Wilaya ya Mbarali ilibahatika kwa sababu ni sehemu ambayo iko kame kufanyiwa utafiti mkubwa sana katika skimu za umwagiliaji na tukabahatika kupata wafadhili ambao waliweza kuanzisha skimu zaidi ya 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninavyozungumza leo ni skimu tatu tu ndizo zinazofanya kazi. Katika skimu tatu zote ni kubwa ambazo zinachukua sehemu kubwa ambazo zinakuwa hekta kubwa na ndizo hizo hizo Wizara husika ndiyo zinataka kuziuza. Sasa nilitaka niseme kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwamba basi sasa kama Serikali imeshaamua kwamba inauza zile skimu za uhakika mashamba yale ya uhakika ambayo yangeweza kuwaletea kipato wananchi wa Mbarali sasa iwe ni wakati muafaka kwa kupitia skimu zote hizi zimegharimu mahela mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *IFAD* wameweka miradi yao pale, *FAO, GTZ, World Bank* na *ADB*. Lakini ile imekufa na hawakuweza kukabidhi kwenye Serikali kwa sababu ilikuwa haijakamilika. Sasa milioni 300, milioni 600, bilioni moja, zimetumika katika kuanzisha skimu zote. Hazifanyi kazi, sasa niombe Wizara kwamba baada ya hapa ipitie mradi mmoja baada ya mwingine skimu moja baada ya nyingine, kuhakikisha kwamba je zinafaa kufufuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeshaingiza kwenye vitabu vyetu kwamba wafadhili hawa wametuchangia Watanzania kwa pesa nyingi sana lakini zimemwagwa zimetupwa na hazifanyi kazi. Wapitie kama zinafaa kama hazifai zimekufa ziendelezwe kusudi ziweze kusaidia wananchi wa Mbarali na Tanzania nzima kwa sababu zikizalisha chakula kitalisha Tanzania nzima na ni vizuri kwa sababu Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Peniel Lyimo ambaye alikuwa Wizara ya Fedha alishiriki kikamilifu katika kufanya utafiti wa skimu mbalimbali za Wilaya ya Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri atakuwa na upeo mzuri wa kuzifuatilia kwa ukaribu. Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji nilitaka nizungumzie hilo kwa sababu wengi wamekuwa wakizungumza kwamba ni mabonde mengi ambayo yamekuwa yakihitaji kuwekezwa. Mimi nilipata bahati ya kusafiri na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kwenda nchini Marekani na Mheshimiwa Rais alikuwa anaguswa sana na alisafiri na wafanya biashara, wafanyabiashara walikuwa wamejiandaa vizuri pamoja na Mkurugenzi wa *TIC* waliweza kuyaa-*identify* maeneo mengi, mabonde mengi ambayo yangeweza kuwekezwa kwa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wengi wa Marekani walionekana wana *interest* ya kuwekeza kwenye kilimo. Sasa Wizara ifuatilie ili kuona kama kuna maeneo ya mabonde ambayo yanatakiwa kuwekezwa ili tuweze kuvutia hawa wawekezaji waje wawekeze ili tuweze kuwa na chakula cha uhakika na tuongeze pato letu la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nilichangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka leo niseme kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na

Ushirika kwamba mimi Mbarali naguswa sana na nitaendelea kusema mpaka Serikali mtakapokuwa mmesema neno, naamiini mme-*advance,* lakini kilio mnachotupa watu wa Mbarali ni kikubwa kwa yale mashamba mawili ambayo yanauzwa. Naamini taratibu zote zimefanywa kabisa siyo rahisi kurudi nyuma na haya mambo yalifanywa kama vile kule Mbarali hakuna Mbunge, kama kule Mbarali hakuna viongozi, kwa sababu mwaka 2003 nikiwa Mbunge, tamko la Waziri wa Kilimo ambalo naamini huwa halibadilishwi bila kuletwa tena Bungeni, lilisema kwamba mashamba yatabinafsishwa ya Hanang na mashamba mengine yalitajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mashamba ya Mbarali kwa maana ya *Mbarali Rice Farm* na Kapunga yatakagawanywa katika sehemu ndogo ndogo ya ekari nne, nne, wanapewa wakulima ambao wanatataka kununua, siyo kupewa bure, maana yake anunue. Wakishauziwa uundwe ushirika wa pamoja ili kuwa rahisi wa kuendesha yale mashamba na ukaandika barua, kwa ruhusa yako, ikapelekwa Mkoani kwa Afisa Tawala wa Mkoa kwamba aandaye Kamati ya Wilaya ambayo itashughulikia ugawaji wa mashamba hayo na mtaalam kutoka Wizara ya Kilimo na Mtalaam kutoka *PSRC* waongozane kwenda kule Mbarali kuhakikisha kwamba haya mashamba yanagawanywa na yanapangiwa thamani ili kusudi hawa wakulima wanaotaka kununua wanunue ili wamilikishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge nikaenda nikawaambia wananchi na wananchi walisikia na kipindi chote tumekuwa tukisubiri *PSRC* waje wapime ili wananchi hawa wapewe. Lakini cha kushangaza unasikia yaani yanasemwa maneno au mnunuaji anakuja pale anaangalia shamba, anaondoka na Serikali ikatangaza vile vile kuwa mashamba ya Mbarali yanauzwa. Sasa siyo kuwekeza tu, ni kuuza maana yake unamuuzia mtu mmoja. Lakini anauziwa *a hundred percent.*

Sasa wananchi baada ya kusoma gazeti wakahangaika kuunda ushirika haraka haraka na wenyewe wakaomba wauziwe, lakini kupitia tathmini *PSRC* wakaanguka wakawa watatu/wanne kwa sababu ya kukosa utaalam wakapata hao waliopata. Sasa mimi nilikuwa na shaka hivi Serikali inaamua kuuza hawakutengui kile kitu ambacho walikisema ndani ya Bunge kwa nini hawajaleta hoja hii ndani ya Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi nilifikiri kama mliona ni vigumu kugawa, mngekuja tena ndani ya Bunge mkatoa taarifa ndani ya Bunge kwamba sasa ule uamuzi wa Bunge umebadilishwa, tumeamua sasa kuliuza kwa sababu moja, mbili, tatu ili sisi tuelewe na wananchi kule waelewe. Sasa hiki kimekuwa kikinisitikisha. Sasa nimekaa najiuliza tu na mpaka hatimaye nikaenda *PSRC* nauliza naambiwa amepatikana mnunuzi, shamba la Mbarali na shamba la Kapunga.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati wa kampeni na Mheshimiwa Rais alipokuja tulimweleza na mimi nilikuwa nikiwaambia wananchi kuwa Serikali inafikiria utaratibu mpya wasubiri. Cha kusikitisha tukasikia kuwa mnunuzi anakwenda kukabidhiwa shamba na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Joseph Mungai, angalau hata kwa kuniita Mheshimiwa Mbunge kuwa Baraza la Mawaziri tumebadilisha uamuzi, lakini umeendelea kupeleka kwenye *Cabinet* kwa *approval* ili

apewe yule ambaye anatakiwa auziwe yaani ni kitu cha kusikitisha. Sasa hawa wananchi watakuwa na imani gani na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini Mheshimiwa Rais ni mtu anapenda watu wake, sasa naomba tusije tukampotosha kwa hili. Wananchi wa Mbarali wanampenda sana, wamemchagua kwa asilimia 80 na zaidi na wanaguswa sana na hamna kitu kingine. Lakini hata unawapenda wakulima wakubwa kuliko wakulima wadogo, hawa wakulima wadogo umewatafutia sehemu gani ya kwenda kulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kwa niaba ya wananchi wa Mbarali nataka niseme kwamba sisi tunaukubali uamuzi wa Serikali lakini kama wakulima hatutakuwa na nafasi ya kuwaachia mpaka tuonyeshwe sehemu ya kwenda kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtutafutie nafasi muhimu ambayo wakulima wote 15,000 ambao walikuwa wanalima kwenye mashamba haya wapewe sehemu ambayo itakuwa mbadala ili waendelee hawa ambao watauziwa na kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali yao, wote Mbarali mnaifahamu, mchanganyiko wa Mbarali mnaufahamu na wananchi wamesema wamechoka kurudi tena kwenye umanamba, kwenye utumwa, wanahitaji kujikomboa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hoja yangu kubwa ilikuwa ni kusisitiza kwenye mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nilipokuwa nimechangia kwamba naomba jibu la Mheshimiwa Waziri wa Kilimo atuambie tunakwenda wapi watu 15,000. Mheshimiwa Rais anataka kuajiri watu zaidi ya milioni moja, ajira mojawapo ni hiyo ya kilimo ambayo itaajiri watu zaidi ya 30,000 na si wa Mbarali tu, lakini na Waziri wa Maji na Bodi yake imesema hakuna sehemu nyingine tena ya kuendeleza kwa sababu ni chanzo cha maji. Tukishawauzia watu wawili tayari maji hayatapelekwa sehemu nyingine yoyote tena na huna nafasi nyingine yoyote ya kuanzisha mashamba mbadala, kwa sababu yale mashamba yetu sisi tuko kwenye chanzo cha maji, na yale maji yanatakiwa kwenda katika Mto Ruaha. *(Makofi)*

Lakini tumesema vile vile tunataka kuwawezesha wananchi, hivi Serikali haiwezi kuitengeneza ile mifereji ikawaachia wananchi wakamwagilia yale mashamba kweli? Tunawawezeshaje wananchi ili waweze kujipatia ajira. Lakini lingine tumezindua juzi Ofisi ya Waziri Mkuu, mwaka jana, stakabadhi za mazao ghalani, ya masoko, kwa sherehe kubwa kwa Makatibu Wakuu wa Wizara zaidi ya watano, walikuja pale Chimala na *CRDB* wakajitolea shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuwakopesha wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza sasa hivi maghala yote yamejaa mpunga ambao umetoka kwenye yale mashamba. Sasa leo ule mpunga haujauzwa lakini tunauza yale mashamba. Umaskini utaendelea kubaki, hawatakuwa na uwezo tena wa kufanya chochote.

Mimi ninachoongea hapa ni kwa uchungu, siongei kwa sababu nina *interest,* lakini ninaangalia kwa upeo kwa jinsi ninavyoona mbele zaidi. Kuna kata mbili, ipo ya Ubaruku pale, ukiwakuta vijana wamefungua viwanda, wanakiita Makambako jina la sehemu moja ya Mkoa wa Iringa. Viwanda vya kukobolea mpunga vimekuwa vingi.

Wamenunua matrekta yao mengi sasa watalimia wapi hayo matrekta. Kwa sasa wana kiburi cha uchumi maana yake wanajidai wana pesa, wana *income* yao leo unawaambia acheni. Watakwenda wapi, kwa kweli nina uchungu na masikitiko makubwa, kama ningekuwa nimeshirikishwa ingekuwa afadhali na ningetoa elimu kwa wananchi wetu. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia kidogo kuhusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mimi nilikuwa Mbunge toka mwaka 1995 mpaka 2000 na hotuba za Wizara hii ya Kilimo, naziona zinakwenda vile vile na hakuna *improvement* ya kilimo katika nchi hii na tutakwenda hivi hivi mpaka tumalize 2010 hatutakuwa na chakula cha kujitosheleza wala cha kuwa na *surplus* ya kusafirisha na kupeleka kwa wenzetu, kwa nini basi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna ardhi nzuri sana, tuna maji ya kutosha, wataalam wapo, kilichokosekana ni sera nzuri za kilimo. Hebu tuchukue mfano mdogo tuna hichi hichi tunachokizalisha kwa upande wa matunda, tumewaandaje Watanzania wakaweza ama kusindika matunda yao au kuyasafirisha kupeleka nchi za nje. Tuchukue mfano, Mungu amegawa dunia kila upande na rasilimali zake, Mashariki ya Kati, Dubai, Abu Dhabi, Sharja, Bahrain , Oman na nchi nyingine zote. Mungu amewajalia amewapa mafuta, lakini hawana ardhi ya kilimo, kutokana na kwamba watatumia maji mengi kwa njia ya *irrigation.* Sasa kwa nini Mungu amewapa neema ya mafuta kwa sababu wao wapate uwezo wa kuagiza bidhaa kutoka kwa wenzao wanaozizalisha. Sasa chukua mfano, India, Bangladesh, Pakistan, Iran, Malaysia, Indonesia, Philippine na Thailand, wanazalisha matunda, chakula na mbogamboga na zote zinakwenda *Middle East* wana Cocoa uchumi wa *Middle East* na wanajenga nchi zao. Sisi tunafanya nini kuwahamasisha vijana wetu, walau kwa kusafirisha matunda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ndege ya *Emirates* inaondoka kila siku Dar es Salaam kwenda Dubai, *daily*, *seven days a week,* ndege mbili *now,* tunasafirisha walau mboga, tani moja ya mchicha, tuna safirisha angalau choroko, maembe, machungwa. Kwa nini tusitumie nafasi ile, tena basi kama wale ambao wanaliendesha lile shirika ndege wakiona kwamba Tanzania kuna matunda na sisi tukazungumza nao kwamba inaondoka ndege tupu ili tuweze kusafirisha angalau viwango fulani vya matunda na mboga mboga zetu watatukubalia kwa sababu ndege yao itakuwa inachukua mzigo fulani wa kuingizia tija katika shirika lao la ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi amekuja Waziri Mkuu kutoka China, ameonana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na akamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba China itaondosha ushuru wa bidhaa zitakazoingizwa nchini China. *Is a big chance,* lakini je, tunaweza kufanya hicho kitu? Pana *AGOA,* Wamarekani walitupa zaidi ya miaka minne kwamba bidhaa zetu ziende Marekani lakini zenye viwango vinavyokubalika. Tujiulize tumesafirsha nini mpaka leo kupeleka Marekani, muda unakwisha na Wachina watatupa nafasi lakini hatujawaandaa vijana wakafanya kazi ambayo itawaletea tija na kuondokana na mzigo huu wa ajira kwa vijana na kuwafanya wabakie vijijini badala ya kuja miji mikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana tunawahitaji wakati wa uchaguzi tu, ukimalizika basi hatuna haja nao mpaka mwaka 2010. Tuna kahawa mimi jana nimeona kahawa hapa kutoka Mbiga ni *well packed*. Kibati kimoja ni shilingi elfu moja za Tanzania wanauza hapo. Kahawa ile kama kutakuwa na watu madhubuti wa uhakika, wenye busara na mawazo ya kibiashara, kama watakwenda *Middle East*, Oman, Dubai, Abu Dhabi na hata Uingereza, wanaweza wakapata soko na tukawapatia soko watu wa Mbinga wakauza kahawa yao nzuri katika Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani. *(Makofi)*

Lakini kahawa wamekuja kuuziwa Wabunge, tunakunywa kahawa gani sisi Wabunge, isipokuwa hawa wenzetu wamekuja kutuonyesha mwamko wao kwamba wako tayari kufanya biashara. Sasa sisi tutawasaidiaje? Hebu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, njooni tukae mimi na ninyi halafu mnipe tiketi ya kwenda Dubai moja ya kwenda na kurudi kama sijakupatieni soko japo la bidhaa moja. *(Makofi)*

Leo unakwenda *Shoprite* unakuta *juice* ya *box* eti inatoka Afrika ya Kusini, si aibu hii kwa Watanzania. *Juice* toka Afrika Kusini, mbatata zitoke Afrika ya Kusini, *chilly sauce*, *tomato sauce* hata kama ni biashara huria, lakini lazima tuangalie baadhi ya biashara zimilikiwe na Watanzania, zifanywe hapa Tanzania kutokana na *raw material* ya matunda yanayooteshwa Tanzania, ndiyo! Kama tukikijenga, tukakithamini chetu, tutathamini cha Afrika Kusini, cha Botswana, cha Dubai, sisi tupeleke, sio sisi tuwaagizie tukatumie pesa za kigeni, hata kama zinachukuliwa na mtu binafsi mfanyabiashara, lakini bado tunaumia kiuchumi sisi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, zabibu Makutupora pale, palikuwa na *grape irrigation* ilianzishwa na Wayahudi karibu miaka 30 nyuma wakatandika ma-*pipe,* JKT wakawa wanazalisha zabibu, tumefanya nini zimekufa? Na Dodoma ni mahali pazuri pa kuzalisha zabibu. Tunaweza tukazalisha zabibu, tukasafirisha, zikatumika nchini na nyingine zikatengenezewa *juice* hapa hapa nchini ni viwanda vidogo vidogo tu *small scale industries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tusingojee *investors,* hebu na tuanzishe kitu kinaitwa *farmers bank,* tuwakopeshe hawa wakulima na vijana wetu pesa ndogo ndogo. Waanzishe hivi viwanda vidogo vidogo vya kubangulia korosho, waagizie viwanda vidogo vidogo vya kutengenezea hizi mboga mboga na haya mambo ya *juice* wasafirishe. Kasulu kulikuwa na tangawizi, walikuwa *encouraged* kwamba wazalishe tangawizi, wakazalisha tangawizi, matokeo yake hakuna mnunuzi. Akatokea Mjerumani anakwenda kununua tangawizi kilo kwa shilingi 50, aibu, lakini anatumia nafasi ile kwa kujua kwamba hawa wanaouza wana njaa na inabidi sasa wauze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika masoko yetu ukienda utakuta kuna tangawizi za unga, mdalasini wa unga, hiliki, pilipili manga, zinatoka ati India, Indonesia, Pakstan, kwa nini? Tufanye hili ndio dampo la kuleta bidhaa zao, sisi tumelala? Tanzania kama tuta-*determine* tukawa na kilimo cha kweli kweli, tukawaandaa vijana wetu basi itakuwa ni *bread basket of Africa* na kama hatukufanya maandalizi mazuri itakuwa ni *bagging*

*bowl of Africa instead of bread basket of Africa, yes* kwani nini. Leo wazungu wa Zimbabwe walikuwa na matatizo yao ya kisiasa wakaondoka pale, wakaenda Msumbiji, wakaenda Zambia, wakaenda Nigeria, tumeitumiaje nafasi ile kuwa *encourage* wale watu kuja kwetu hapa. Kwa sababu makaburu wana ugomvi na Serikali yao, hapana, sisi kilichokuwa kizuri tukilete katika nchi yetu kwa manufaa ya nchi yetu.

Kuhusu maua, juzi tulikwenda ziara nchini Kenya, kuna kampuni moja ya maua inaitwa *home growers*, wanachukua mpaka maua ya wakulima wadogo wadogo na kila siku kuna ndege moja ya 747 inaondoka Nairobi inakwenda London na Amsterdam kupeleka maua. *They are making a lot of money,* sisi tunafanya nini, maua mpaka ifike ile siku gani wanaita nini *Valentines day*, tutie sisi kichwani na kwenye koti basi, kumbe maua yanathamani Ulaya, kumbe mboga zinatakiwa *Middle East,* madafu yanaingizwa kwenye vibati leo nchini Thailand, wanauza *juice* ya madafu ndani ya vibati na unaikuta ipo mpaka Dar es Salaam, kwa sababu wameamka kibiashara, wanajua soko liko wapi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa sisi Waheshimiwa Wabunge, mimi ninachotaka niseme kwamba tunazalisha tena kwa wingi lakini je, viwango vyetu vya kuzalisha, vinakwenda sambamba na *world market*. Mchele unatoka Kilombero, Morogoro, unatoka Mbeya, unatoka Shinyanga, lakini mchele ule ule unaotoka Shinyanga unaukuta Zanzibar unauzwa shilingi 1,000 na mchele wa *Basmat* unaotoka Pakstani, Karachi unauzwa shilingi 1,000, tujiulize sasa kitu gani, kwa nini bei za Tanzania za bidhaa zinakuwa zinapanda. Ili tukijua tatizo hilo na tukaliondosha, sisi Watanzania tunapenda vyetu zaidi, mchele wa Shinyanga, Mbeya, wa Morogoro Kilombero, ni mzuri kuliko wa Pakstani, una radha, una harufu nzuri, lakini je, tumejiandaa sisi mchele ule kuwafikia wananchi kwa bei rahisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasisitiza tu Mheshimiwa Waziri na watendaji wake muwe *serious* kuwaandaa vijana na *group* ndogo ndogo waandae mipango kabambe na kuwapatia viwanda vidogo ili wasindike, wachague matunda mazuri, waya-*pack* vizuri yasafirishwe, yatapata tu soko kwa nini yasipate soko? Juzi Dodoma walisafirisha Mbuzi 400 kupeleka Dubai na nyama imekwisha kwa wiki moja tu, kwa nini tusipate soko kwa machungwa, kwa nini tusisafirishe maembe, pilipili hoho ni zao ambalo lina bei kubwa sana dunia ni *vanilla* inaota nchi nne tu duniani sasa hivi, Indonesia, Malagasy na nchi moja *South America.* Sasa hivi zao la *vanilla* limechukuliwa na Waganda, wanapata pesa nyingi sana kwa zao la *vanilla* sisi hatuna maeneo ya kuanzisha hili zao la *vanilla?* Tena basi linakuwa na soko kwa sababu kuna kimbunga huwa kinapita mara kwa mara Malagasy ambacho kinaitwa *huda*, kinaharibu mimea ya *vanilla* pamoja na mpunga pale Malagasy.

Kwa hiyo, wanaanzisha tena kilimo ambacho kinachukua miaka mitatu kuweza kuzalisha, leo zao hili linabei sana Ufaransa, lina bei sana Ujerumani, Marekani, Kampuni ya *Cocacola* inatia *aroma* ya hii *vanilla* katika soda zao kwa sababu limepanda bei. Lilifika mpaka kilo moja dola 400 kwa mwaka 2003/2004, lazima tuamke kiuchumi tusiamke kisiasa peke yake, tuwajenge vijana wetu waweze kumudu soko la ulimwengu kwa kusimamiwa na Wizara hii. Sikwambii haya mambo ya *irrigation* ambayo ndio kabisa tumeyatupa, leo *from hand to mouth,* tunazalisha *from hand to mouth,* hakuna zaidi kuna nini unawakuta watu wanamwaga ngano au mahindi chini ndio wayasafishe,

wayatie kwenye magunia. *It is a primitive system,* kutakuwa na mawe ndani, tuandae maghala ya kisasa, vijana wa kileo tuwape pembejeo, vitendea kazi, mikopo midogo midogo watabakia vijijini wafanye kazi ya kuzalisha matunda bidhaa, mboga mboga na tutumie haya mashirika ya ndege kusafirisha bidhaa zetu kupeleka *Middle East*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Emirates* ni ndege kubwa sana yaweza ikabeba hata tani moja, mbili za mboga mboga kila siku, *just go to* Dubai, utaona ndege asubuhi zimejaa pale hii inateremsha mboga, hii pilipili, hii matunda, hii muhogo, sisi tumelala kwa sababu shirika limekuja pale, bwana mkubwa upewe *first class* ukae ndani, hujui lile shirika unaweza ukalitumia ukasafirisha vitu vyako na bidhaa zako ukapeleka nje na ukapata mafanikio kwa vijana wa nchi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ni mategemeo yangu kwamba Wizara hii sasa itaamka kivitendo, haitaamka kisera kwa kutuandikia mahotuba marefu, marefu kumbe hakuna utekelezaji. Nchi haina trekta, nchi haina *irrigation,* nchi haina mabwana shamba inakuwa ni nchi kama haina wenyewe, lazima tuamke kwa njia za kisasa na kilimo cha kileo ili tulikomboe Bara letu na nchi yetu iweze kuwa ni *bread basket of Africa.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kuwepo hapo katika kiti hicho, kimeku-*fit* kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri, imeeleweka, mimi nitakuwa na sehemu chache tu, za kuchangia. *(Makofi)*

Sehemu ya kwanza ninayochangia ni katika suala la umwagiliaji. Amelieleza vizuri sana nilikuwa tu naomba nimkumbushe kwamba katika Jimbo letu la Mlalo kuna mradi wa umwagiliaji wa kitivo, mradi ule sasa hivi hauko katika hali nzuri, ni mradi wenye *potential* kubwa sana, kuna mahitaji yanayohitajika, sasa naomba kwa vile kaeleza kwamba nguvu kubwa itaelekezwa kwenye umwagiliaji, basi wakati wanafanya hivyo asiusahau mradi ule wa kitivo. *(Makofi)*

Sehemu ambayo nilikuwa nataka nichangie kidogo kwa undani ni katika suala la akiba ya chakula. Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda amelieleza vizuri sana na mimi naomba niongezee, sasa hivi tunayo *strategic green reserve,* akiba ya chakula, mimi siiti *strategic greein reserve* ni *emergency green reserve*. Sio *strategic* kwa sababu kama ni *strategic* chakula tunachokiweka pale kinaweza kukidhi mahitaji ya Watanzania wangapi na kwa muda gani? Mwaka huu tumeona tulipopata matatizo ya chakula kidogo tu ilibidi tuagize tugawe chakula na chakula tulichogawa ni tani 1,414,955 kuwapa watu chakula bure. Chakula hicho kilitosheleza watu 564,000, tufikirie kwamba Tanzania ina watu milioni 30, hebu tuende mbali tufikirie kwamba nchi tunapatwa na janga balaa la njaa ambalo litakaa miaka miwili miaka mitatu, inawezekana kukawa na vita, tukajikuta kwamba tumekuwa *blockaded* hata hatuwezi kuingiza chakula kutoka nje. Hivi Watanzania tunafanya nini? Tumeelezwa hapa kwamba sasa mwaka huu tunazalisha

chakula cha kutosha, imeelezwa katika ile ibara ya 34 kwamba sasa mahitaji ya chakula katika nchi ni tani milioni 9.7 lakini inatarajia kwa taifa litajitosheleza na chakula kwa asilimia 110, lakini fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya kununulia chakula tani laki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafanya chochote hapo kwa sababu chakula hiki hakitawatosheleza Watanzania kama tutapata matatizo. Kitakachojitokeza hapa ni sisi kushika bakuli na kwenda kuomba omba ili kudhihirisha umaskini wetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ameeleza hapa kwamba angalau basi tuwe na mkakati wa kuongeza kiwango cha chakula ambacho tunakuwa nacho katika akiba. Kiwango hicho ni kiwango gani tunaweza tukazungumza, lakini mimi nilidhania kwamba tunaweza tukasema kama mahitaji ya chakula katika nchi yetu hii tani milioni 9 basi angalau tuanze na asilimia 10 ya akiba, iwe ndio akiba yetu ya chakula, kwa maana ya tani laki tisa, ndio mahali pa kuanzia najua kwamba watu wengine wataanza kufikiria inawezekanaje, lakini inawezakana kama Halmashauri hizi zitaambiwa kila moja lazima ianze sasa kuweka utaratibu wa kuwa ghala katika eneo lake la Halmashauri angalau hizo tano 5,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusiishie hapo, mikoa nayo inaweza ikaambiwa mkoa uwe na tani 10,000 ni akiba na Taifa nalo ni lazima liwe na akiba, hapo ndipo tunaweza tukasema lazima tuwe na akiba ya tani labda laki mbili kwa kuanzia. Najua kitakachoanza kuulizwa, fedha zitatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, kila mara tunaambiwa na viongozi wetu sasa akiba yetu ya fedha za kigeni *(Foreign Reserves)* zinatutosheleza kwa miezi, sita, miezi saba, hapo ndio pa kuanzia, fedha maana ya kuwa na *foreign reserves* ni kwa ajili ya kukidhi iwapo tuna matatizo kuweza kuagiza vitu muhimu mafuta, dawa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mafuta ambayo tu ndio tunayapa kipaumbele hayana maana yoyote kwa Mtanzania kama Mtanzania yule ana njaa, lazima sasa tuseme asilimia 10 ya *foreign reserves* zetu ziwe zimewekezwa katika chakula, hapo ndio tutaanza kujenga ari zetu za chakula. Haina maana kuwa na dola huko nje wakati hapa ndani hatuna chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kulizungumza hili kwa sababu suala la chakula ni suala la uhai wa Taifa, suala la chakula kwa nchi ni muhimu na linagusa usalama wa nchi hii, suala la chakula lina umuhimu kama vile ambavyo tuwe na majeshi, lakini majeshi hayo ni mazuri kwa kumlinda Mtanzania kwa sababu yanaimarisha usalama wake. Lakini Mtanzania huyo unayemuimarishia usalama wake kama ana njaa na anakufa na njaa hakuna tofauti, ni sawasawa kama ameuawa na adui tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima *foreign reserves* zetu ziwe kwa kiwango fulani *committed* kuweka katika *food stock* zetu na *green reserve* hapo ndio tutaweza kusema tuna *strategic green reserve,* sasa hivi tunakosea tukisema tuna *strategic green reserve* tuibadilishe jina kabisa kwa tani 100,000 tunazoweka, tuite *emergence green reserve*.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa kifupi tu, suala la maafisa ugani, nashukuru juhudi zinafanywa tuwapate, tuongeze idadi yao. Lakini hawa ni watumishi wa umma kama walivyo watumishi umma wengine, tumekuwa na mpango wa *MMEM,* tumejenga madarasa, tukajenga na nyumba za walimu na tunaendelea kujenga nyumba za walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waganga, zahanati na vituo vya afya tunawajengea nyumba, sikuona mahali popote tunapozungumzia maafisa ugani hawa ambao kila mara tunawalaumu kwamba hawakai katika vituo, wao tunawaweka katika fungu gani? Kwa nini hatuwaweki katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba hapo walipo nao tunawapatia nyumba? Kwa sababu vinginevyo miongoni mwa wananchi tu na tunajua matatizo ya mwananchi anapopanga katika nyumba za wenyeji kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza nitazungumza kwa kifupi namna hii kwa sababu nilidhania kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, inakidhi. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe maoni yangu juu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa pongezi hasa za hivi juzi za Rais wetu kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Chama kitukufu cha CCM. Pongezi nyingi sana na uwezo anao. *(Makofi)*

Sasa nikitazama hii *speech* nataka kabisa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa hotuba yake nzuri, imetimia, inatupa matumaini, anazungumzia *Tanzania Green Agricultural Revolution,* mapinduzi makubwa ya kilimo ya kijani ya Tanzania, haya maneno ni makubwa sana na hatua ya kuitamkia dunia kwamba sasa Tanzania imeamua, haitaki tena kuwa omba omba katika chakula maana yake nini? Maana yake haiwezi kuwa *Sectorial Ministry* haiwezi kuwa Wizara ya Kilimo tu hapana, maana yake Serikali nzima ifanye *commitment* ifanye jambo moja tu sasa kwa miaka ijayo, kazi kubwa ya Tanzania ni kuleta mapinduzi ya kijani katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Mheshimiwa Rais wa nchi hii awe ndio jemedali *number one,* kule Misri mathalani, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Waziri wa Maji, hawa wanatoa ripoti kila siku kwa Mheshimiwa Rais wa Misri, tunasema sasa hivi Mheshimiwa Rais wa nchi hii awaweke hawa kilimo, hasa kilimo na maji wawe wana ripoti kila siku maendeleo ya kilimo katika nchi hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ninaloliona mimi ninaanza pale nilipozaliwa, kilimo nimekiona wakati nakua na kilimo nakiona sasa. Inaelekea kilimo hakina mwenyewe, zamani kulikuwa na ma-*DC* wa kikoloni, walikuwa wanapita katika mashamba, vile vile Mkurugenzi akiingia katika kile kiti anasahau kwamba ana kazi ya kufanya ila anadhani kazi yake ni kuangalia ankara zile, wangapi wamefanya hivi kwamba kilimo katika Wilaya, ndio maendeleo, ndio uti wa mgongo na ni msingi wa maisha ya wale watu katika Wilaya ile kwa hiyo, *DC* na *DED* lazima wawe mbele pale,

Kitaifa tunamuomba Rais awe mbele na katika Wilaya *DC* awe mbele maana yake nini? Maana yake lazima kubuniwe utaratibu wa *quarter,* tuelewezwe bonde la Rufiji linaweza kutoa mazao kiasi gani kwa mwaka kama likilimwa kwa ukamilifu na hamuwezi kuleta ubishi wowote kwa sababu ni historia katika miaka ya 1950 na 1960 kulikuwa na taasisi ya *Tanzania Agricultural Cooperation* imefanya *study* pale na mazao yote yanaweza kuota pale yameratibiwa katika Wizara ya Kilimo na nakumbuka katika miaka ya 1960 Mheshimiwa Iddi Simba alipelekwa Amerika kwenda kubuni mradi ufanane na *The Tenesii Value Authority of America* ambayo ndio kapu la chakula ya Amerika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kurudi mambo yaliyotokea, nasikia kumetokea *Rubada,* mimi bado Mheshimiwa Waziri, atanieleza hivi *Rubada* inafanya nini, ilitakiwa ifanye nini, imefanya na sasa inafanya nini na baadaye itafanya nini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninaomba huu mtiririko wa Rais katika kilimo uwafikie Wabunge wote. Mbunge siku moja asimame aseme mimi katika Wilaya yangu au Jimbo langu ekari zilizokuwa zinalimwa kabla ya mapinduzi ya kilimo ilikuwa kiasi kadhaa baada ya muda imekuwa kiasi kadhaa na kwamba *productivity* kulikuwa na *turnage* yaani kiasi cha mavuno kadhaa lakini baada ya haya mapinduzi tumepata kiasi kadhaa na tunakwenda mbele na hiyo ndio maana ya *revolution,* kwa sababu gani? Itakuwa aibu sana Bunge hili linaloheshimiwa dunia nzima tutangaze sasa tumekwenda katika mapinduzi ya kilimo kesho twende tena kuomba chakula, itakuwa aibu sana. *(Makofi)*

Kuna suala hapa la kupanua kilimo. Tuna taarifa Bonde la Rufiji na haya ni maandishi yapo katika Wizara ya Kilimo, ukiweza kulitumia kwa ukamilifu kwa maana ya upanuaji wa kilimo, mbegu bora, huduma za ugani, *productivity* yaani mazao yatakayozalishwa Rufiji yatawalisha Watanzania wote na vile vile tutakuwa na uwezo wa kusafirisha nje ya nchi kwa mauzo tutakuwa na *export surplus*. Tatizo ninalolipata mimi ni lile lile la ubinafsi. Mtu anajua shamba lake ni ekari moja na ekari nyingine kapewa mdogo wake na nyingine kapewa mdogo wake mwingine imekwisha. Bado hela hizi nyingi naye anataka apate, utalimia wapi? Peleka hela hizi kwenye *area* kubwa kubwa ambapo watu wanaweza kupata ekari nyingi wakalima na wakanyanyua upatikanaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama ukurasa wa 14 wa *budget speech, bullet number* tatu, hatuelezwi, ekari milioni moja itafikiwa miaka saba hivi kila mwaka tunaendaje? Mwaka huu tumewekewa namba pale je, mwakani tunaendaje hatua kwa hatua yaani mpaka wale wanaosoma wanajua baada ya miaka miwili tutatakuwa tumefika nusu baada ya miaka mitatu tutafika hapa, sasa hii haionekani vizuri. Nadhani Mheshimiwa Waziri atatueleza vizuri wakati anapojibu hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mtanisema tu lakini siwezi kuacha kuzungumza habari ya Rufiji kwa sababu gani, kuna mfano. Tumetumia matrekta Rufiji tangu wakati wa kikoloni kwa sababu haya majembe ya ng'ombe hayafai kule magugu makubwa hayawezi kabisa kupindua magugu na kama mnabisha mwende kutazama. Kule tunataka

matrekta yaje kwa wingi unaweza kutukopesha au ukatuuzia bei nafuu na *infact* bila kuleta *gimmicks* zozote uwe tu na matrekta ya kutosha Rufiji na watu wanapita kuhimiza na *DC* hakai katika kiti chake na Mkurugenzi hakai katika kiti chake ila anaangalia mashamba mangapi yamelimwa kwa Tarafa basi haya mapinduzi yatafikiwa hata kabla ya hiyo miaka saba iliyowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefikia mahali sasa tuwe wakweli kwa mambo tunayotaka kufanya. Naomba kuwepo na *audit* ya watumishi bora katika kilimo, wale wenye kufanya kazi kwa uzoefu watupishe. Unajua yuko *Agricultural Officer* wa miaka na miaka hana habari mpya yoyote, nadhani hawa jamani tungeelezwa tu kwamba wako kadhaa na namwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie Wizara yake halafu baadaye atuambie tu kwamba katika nchi hii wako Maafisa kadhaa na katika hao nimefanya utafiti kadhaa kadhaa hawafai tumewapumzisha na nimefanya *recruitment* mpya yaani unajua unaeleza hii habari huku kile mtu anakushangilia kwa sababu anajua sasa tumepata askari bora wa kutusukuma katika vita yetu ya kuleta mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba tena na tena suala la matrekta, suala la kufahamu na kutenda kwamba ukiwa na mazao mengi ya kilimo basi utakuwa na *manufacturing sector.* Kule Rufiji na kwa mzee wangu Ngombale, Matumbi pale yaani machungwa yanaoza kabisa watu wanakanyaga badala yake tunakwenda *supermarket* tunanunua machungwa ya *South Africa. Manufacturing* nayo iwe sehemu ya haya mabadiliko makubwa yanayoitwa *Agricultural Green Revolution*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, sekta nyingine nazo ziwemo katika mapinduzi haya. Kwa mfano kama barabara hazipo, kama *facility* za umeme hazipo vijijini, utakuta makundi makubwa ya vijana yanakuja Dar es Salaam. Pale Temeke nadhani nusu ya wananchi wa Rufiji wako Temeke na vijana wanauza karanga na nguo za mkononi yaani kwa kweli hawa tukiwatengenezea mazingira mazuri kule Rufiji nasema kila sehemu vijijini watarudi, watafanya kazi nzuri na tutapata mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wote wawili na wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi. Naridhishwa sana na ushirikishwaji wa Kamati nzima na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo na Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi nimemfahamu Mheshimiwa Joseph Mungai, ana tabia ya kuthubutu ili mradi ana hakika kwamba mpango huo uko kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Nina hakika kabisa kwamba akishirikiana na Manaibu wake pamoja na wataalam nimeangalia angalia wamethubutu katika maeneo mengi, wamegusa hata maeneo ambayo yamesahaulika muda mrefu hayajaguswa, nina hakika angalau

bajeti hii ina matumaini, nina hakika kwamba tutapata mafanikio katika awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara kwa kunipatia mradi wa umwagiliaji kule Ulyanyama uliopo Wilaya Sikonge zaidi ya shilingi milioni 140. Napenda nikuahidi Mheshimiwa Waziri kwamba nitahakikisha fedha hizo zinatumika vizuri kama ulivyoniomba na nitahakikisha kwamba ninawashirikisha wananchi wenzangu pamoja na viongozi wenzangu katika kukamilisha mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukipongeza basi unasema na ya kwako. Kwanza naomba niende kwenye matumizi ya mbegu bora. Ukurasa wa 16 kwenye kitabu chako umezungumzia matumizi ya mbegu bora. Ukiangalia pale unaona kwamba mahitaji ya mbegu bora ni zaidi ya tani 120,000, mwaka 2004/2005 matumizi yalifikia tani 12,830,000, hii ni sawa na asilimia 10.7. Kwa hiyo, hapa tunajifunza kwamba matumizi yetu ya mbegu bora yako chini kwa wastani wa asilimia 10. Sasa kama huna mbegu bora, huna mbolea kwa sababu tuna matatizo makubwa sana ya mbolea kutokana na ugawaji wa mbolea huwezi kuifukuza njaa. Naomba sana Serikali kwa kweli ijielekeze katika mambo haya makubwa mawili kuhakikisha kwamba wakulima kwa kweli wanapata mbolea kwa bei ya chini lakini vile vile wakulima wetu wanapata mbegu bora katika kutimiza zile kanuni bora za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye mbegu nataka nitoe tahadhari, tuna mbegu nyingi sana za mahindi humu nchini. Tuna mbegu zinaitwa *Kagil, Cidico, Pana* na kwa bahati nzuri ama mbaya mbegu hizi zinatangazwa sana kuliko mbegu zetu za asili ambazo zimetengenezwa kwa mazingira yetu hapa. Tunazo mbegu nzuri sana kwa mfano Kilima, mimi ni mkulima, Katumani na zinatofauti kubwa na hizi mbegu zinazotoka nje. Kwanza, mbegu zinazotoka nje hizi nilizozitaja zinaharibiwa mapema sana na wadudu hata kabla hazijaingia kwenye ghala, lakini vile vile mbegu hizi kwa matumizi ukapeleka kukoboa debe moja unapata nusu debe zina pumba nyingi sana.

Naomba uzalishaji wa mbegu zetu za asili hapa nchini kwa kweli uongezeke na wananchi wetu kwa kweli wasisitizwe kuzitumia sana. Sisemi hizo za nje ziachwe kutumiwa lakini kwa kweli umuhimu uendelezwe katika kuwaelimisha wananchi wetu watumie mbegu zetu ambazo ziko katika mazingira yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye tumbaku, kwanza niwapongeze wadau wote wanaoshiriki katika kuliendeleza zao hili. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuita wadau wa tumbaku ili kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo matatizo, naiomba Serikali kwa kweli iyaangalie kama kweli tunayo dhamira ya kuongeza uzalishaji wa tumbaku lazima tuyatafutie ufumbuzi matatizo haya. Kwanza ni tatizo ya bei kubwa sana ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzalisha tumbaku bila mbolea. Nataka kutoa mfano hapa. Mkulima wetu anatakiwa atumie mifuko minne ya *NPK* kwa ekari moja na kila mfuko gharama yake ni shilingi 28,000. Serikali kwa mwaka huu uliopita imetupa ruzuku ya shilingi 800 kwa mfuko mmoja. Sasa hizi nazilinganisha na pesa ambazo tunawapa ndugu zao kina Mheshimiwa George Lubeleje hapa Dodoma hapa shilingi 800 kwa shilingi 28,000 kwa mfuko, huu ni utani. Lazima tulete mabadiliko, tuwasaidie wakulima. Sizungumzii tumbaku peke yake tujielekeze kwenye pamba, tujielekeze katika mazao yote hata yale ya chakula bado ruzuku ya mbolea kwa kweli naona kama tunacheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema ruzuku hii ambayo inatolewa na Serikali kama hili haijaliangalia vizuri tutaendelea kuwaneemesha wafanyabiashara lakini wakulima haiwafikii. Watu sasa hivi wanafanyabiashara sana ya mbolea na inalipa na ina mtaji mkubwa sana, lakini wakulima hawafaidiki. Sisi kwetu huko hii mbolea ya ruzuku tunaisikiasikia tu kwa mchezo huu wa shilingi 800, tunasikia sikia tu. Naomba sana Serikali kwa kweli ione jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nijielekeze kwenye suala la utaratibu wa mikopo ya pembejeo ya tumbaku. Mimi naomba sana Serikali kwa hili itusaidie na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama unataka hayo mabadiliko ulipotuita kwa kweli hili nalo ni jambo la msingi sana. Upo utaratibu wa kuwakopesha wakulima wa tumbaku wote nchini. Wanakopa kwa yule yule anayenunua tumbaku yaani yule anawakopesha wakulima lakini huyo huyo anawasubiri awakate fedha zake lakini anunue tumbaku yake yaani unakopa kwa mlango wa kushoto halafu unachukua kwa mlango wa kulia. Ndio maana yapo masharti mengi sana tunawekewa, hatuwezi kujikwamua kwa sababu eneo ni hilo hilo moja. Ni huyu huyu ndiye anayekupa pembejeo kwa hiyo huwezi kumkwepa. Ikijitokeza labda benki labda inataka kuwakopesha wakulima utaona mizengwe inaingia hapa. *CRDB* imejitokeza, mizengwe inaingia hapo, kuna nini? Tunataka wakulima wafunguliwe milango wanapotaka kwenda kukopa mbolea waende wakakope haya makampuni ya tumbaku yamekuja kununua tumbaku, hayakuja kufanya biashara ya kukopesha wakulima mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo nalo naomba Serikali itusaidie. Wapo wakulima ambao wameamua kujikwamua kwamba hawataki kukopa. Hawa wananunua pembejeo zao kila kitu wanajitegemea lakini siku ya kwenda kupeleka mazao yake kwenye chama cha msingi, chama cha msingi pale kwa sababu huyu mnunuzi anachohitaji ni deni lake lote hata yule mkulima aliyejitegemea naye anaondolewa fedha zake zote kulipia madeni ya chama cha msingi, huu ni uonevu. Naomba hili kwa kweli liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, *ATTT*. Kipindi kilichopita tumesema sana enzi za Mheshimiwa Charles Keenja mpaka ameondoka. Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Waziri Mkuu, *ATTT* ni kero kubwa. *ATTT* kwa wasiofahamu ni muungano wa wafanyabiashara wa tumbaku. Ukishakuwa na watu wanafanya biashara katika mfumo wa soko huria, wanaungana lengo lao hawa ni kunyonya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alipolihutubia Bunge tarehe 30 Januari, 2002 alimnukuu ndugu Adam Smith. Napenda na

mimi ninukuu kwa ruhusa yako: "Kwa miaka kumi Adam Smith aliandika kitabu kiitwacho kwa kifupi Utajiri wa Mataifa kilichochapishwa hatimaye mwaka 1976 na kumfanya akubalike hadi leo kuwa baba wa maendeleo ya nadharia ya uchumi wa kisasa. Kwenye kitabu hicho anasema watu wafanyao aina moja ya biashara hawakutani mara kwa mara na wakikutana mazungumzo yao huishia katika kula njama dhidi ya umma au mbinu ya kupandisha bei. Anasema siwahukumu wafanyabiashara lakini najenga hoja kuwa jinsi tunavyozidi kuelekea kwenye uchumi wa soko ndivyo inabidi uwezo wa udhibiti wa Serikali uongezeke." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATTT* tumeisemea hapa lakini Serikali kila wakati inapata kigugumizi. Serikali ya Awamu ya Nne naiomba itusaidie. Huu muungano huu kama utaendelea wakulima wetu wataendelea kupata bei ya chini ya tumbaku, wataendelea kubaki katika hali hiyo duni na wataendelea kuzalisha tumbaku kwa manufaa ya hawa wanunuzi ambao kwa kweli muungano wao lengo lao ni kuwanyonya. Kwa hiyo, naiomba Serikali, chonde chonde huu muungano wa hawa ufe. Nasema ufe usipokufa basi nitajua kuna mkono wa mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naitakia kila la kheri Wizara hii, naielewa majukumu ambayo Wizara hii inayo. Kila kheri majukumu haya ni makubwa, Mheshimiwa Joseph Mungai nakuombea kila la kheri, najua pamoja na wanaokuangalia kwamba umri wako ni mkubwa, najua afya yako ni njema sana. Nakutakia kila la kheri, kazi njema na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Manaibu wake na wataalam wote kwa kutayarisha hotuba nzuri ambayo inatupa matumaini kwamba labda sasa kilimo kitakuwa mkombozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye katika hotuba yake alisema kilimo ni kipaumbele chake namba mbili baada ya elimu. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Napenda vile vile niipongeze Serikali kwa kutenga shilingi milioni 500 ziende kwenye Mikoa yote ili wakulima na wafanyabiashara waweze kukopa na kupunguza umaskini. Naiomba Serikali hizi hela Serikali ishirikiane na asasi ambayo ina uzoefu wa ku-*handle* na ku-*manage micro-finance* vinginevyo zitaishia mifukoni kwa watu. Kama Serikali haijapata asasi yenye uzoefu, shilingi milioni 500 zinaweza kununua matrekta 11 kwa kila Mkoa na yanaweza kupelekwa kwenye Halmashauri na tukawakodishia wakulima kwa bei nafuu ili tuweze kuinua kilimo na kulikomboa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri yote ambayo yako kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nichangie ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini tuna vyuo vya kilimo vingi sana kiko Chuo Kikuu, Vyuo vya *Diploma, Certificate,* naomba vyuo hivi navyo vilime kama wanavyofanya Chuo Kikuu na vikilima mazao hayo Serikali iwahakikishie kwamba itayanunua. Pia naomba vyuo hivi vitoe mafunzo kwa ajili wakulima wa kawaida, mafunzo ya muda mfupi mfupi labda kujifunza kupanda, kuvuna na fani zote za kilimo. Kwa hiyo, vitoe mafunzo kwa wakulima wa kawaida sio lazima wasomi najua wakulima wanaotaka kujifunza kilimo watapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemaji wote wanapiga kelele kuhusu bei za mazao hapa nchini karibu wote tunapiga kelele kuhusu bei za mazao. Mimi naomba nitoe *story* ya mzungumko wa tumbaku. Mwezi wa tisa wakulima wa tumbaku wanatengeneza vitalu vya tumbaku, mwezi wa kumi na mbili wakulima wanapandikiza tumbaku mashambani na kuanza kulima na kuipalilia. Mwezi wa nne wakulima wanavuna na kuikausha na kazi ya kukausha ni ngumu sana ambapo wakulima hasa wanaume inabidi wakae nje ya nyumba zao kwa muda wote wanapokausha tumbaku mpaka kuna miiko mingine wanasema wewe mkulima wa tumbaku wakati wa kukausha tumbaku huruhusiwi kumsogelea mkeo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sababu tu wanataka ulale nje ya nyumba ukiangalia tumbaku yako. Ikishakauka sasa hapo ndio *saga* inaanza hapo. Kuna makampuni yanayonunua tumbaku, kuna bodi ya Tumbaku sasa wao wanakaa kupanga bei ya tumbaku kwa mwaka huo wakati tumbaku imeshakauka. Wakishapanga wanakwenda kufungua soko la tumbaku sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye soko la tumbaku anakuja Mheshimiwa *classifier* wa kampuni inayonunua tumbaku amevaa tai, anakuja na *classifier* wa bodi kavaa tai wanaingia ndani kwenye gulio la tumbaku kwenda kupanga daraja za tumbaku bila mkulima, wanampangia daraja mkulima. Mkulima anauza kwa daraja hiyo na kwa bei ambayo wamepanga wao. Lakini ikienda kwenye gulio wanalosema soko la dunia Morogoro hapa hapa yale makampuni ambayo yamenunua tumbaku na wale wanunuzi toka nje wanakaa pamoja wanajadiliana na kununua tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mwaka huu bei ya chini ya tumbaku ilikuwa ni senti za Marekani 70 bei ya chini na bei ya wastani ilikuwa shilingi 950, lakini Morogoro huko ninakosema kwenye soko la dunia bei ya chini ilikuwa dola za Marekani 3.5 huku senti 70 kwa mkulima pale dola za Marekani 3.5. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika najua Serikali yenu ya Awamu wa Nne nzuri sana na mna mtindo wenu ambao mimi ninaufurahia sana mnafanya *management by walking about,* nakuomba sana Mheshimiwa Waziri mwaka huu msimu wa tumbaku uende kwenye magulio ambako wananunua tumbaku ya mkulima na pia uende kwenye soko la dunia hapo Morogoro wanapouza uangalie jinsi mkulima wa tumbaku anavyoonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mhubiri mmoja alikuwa anahubiria waumini wake siku ya mwaka mpya. Anawaambia, waumini hivi unamwomba Mungu uingie mwaka mpya unaingia halafu mwaka unaisha tu. Mwaka mwingine unamwomba Mungu uingie mwaka mpya Mungu anakuruhusu unaingia mwaka unaisha tu. Huyu mhubiri anasema angekuwa na uwezo angemwambia Mungu usiende mwaka mpya mwingine. Kama unaingia mwaka mpya huleti *impact* kwenye familia yako, jamii inayokuzunguka, kazini kwako, basi Mungu asikuruhusu kuingia mwaka mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mungai hii ya kwamba tunafanya uchaguzi Rais anakuteua unakuwa Waziri wa Wizara "A", unakaa tu inaisha. Uchaguzi mwingine Rais anakuteua unakuwa Waziri wa Wizara "B", inaisha. Ningekuwa mimi ningemwambia Rais asikuchague. Nataka ukiwa kwenye Wizara ulete *impact*. Nakuomba sana Mheshimiwa Joseph Mungai, mimi nakuamini sana wewe ni kaka yangu, ulete *impact* kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba uwakomboe wakulima wa tumbaku na wa mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano mmoja. Nchi moja jirani ilichukua mbegu ya tumbaku toka Urambo, Tabora miaka ya 1960 mwanzoni sasa hivi nchi hiyo inazalisha kilo za tumbaku milioni mia mbili kwa mwaka. Sisi tunazalisha kama walivyosema wenzangu wengine milioni 56.5 na 57. Sasa nchi hiyo na yenyewe imegubikwa na hali hii hii ya wakubwa fulani ambao wanasema wao ndio wana-*control* zao za tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu nchi hiyo kiongozi mkuu wa nchi walipomletea hao wanunuzi wa tumbaku kwamba hapa itakuwa senti 70, 80 akawaambia hivi tumbaku ya nchi yangu bei ya chini mwaka huu ni dola 1.7 kama hamtaki ondokeni, iacheni tumbaku yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wamenunua tumbaku. Sasa sisi hatutaki tufike huko kuwaambia wanunuzi wa tumbaku kwamba bei ya tumbaku iwe dola 2 kama hamnunui ondokeni, tunataka tushirikiane nao ndio maana nakuomba Mheshimiwa Waziri kwamba ukifika msimu wa kununua tumbaku umchukue hata Waziri Mkuu mwende kwenye soko la tumbaku kwa wakulima mkaangalie bei wanayopangiwa, muende Morogoro kwenye soko la dunia ukaangalie wakulima wanavyopangiwa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuondoa makato kwa mkulima makato ambayo alikuwa anakatwa ili waendeshe Bodi za mazao kama ya tumbaku, nawapongeza sana kwani inampa unafuu sana mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda nimuunge mkono Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali na kumwambia kaka yangu Mheshimiwa Joseph Mungai kwamba wewe ni kaka yetu, tunakupenda, ni mchapakazi, tunakuheshimu sana lakini naomba hii hoja ya mashamba ya Mbarali na Kapunga uipe majibu ya kutosha sana ili usije ukatulaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba maelekezo yako, majadiliano hapa yamekwenda vizuri sana, lakini tunaomba maelekezo yako.

Baadhi ya Wabunge wanapoongea, hawaongei na wewe wanawa *direct* Mawaziri wenyewe jambo ambalo si zuri sana tena kwa majina, ningeshauri utoe maelekezo ili Waheshimiwa Wabunge tunapochangia wakuelekee wewe kuliko mtu binafsi kwa mfano *statement* iliyopita kwamba Mheshimiwa Joseph Mungai, ingekuwa ndiyo mimi ningemwomba Rais asikuweke, vitu vya namna hii siyo vizuri, haileti utamu kwenye mjadala. Kwa hiyo, ningeomba wakuelekezee wewe badala ya Mawaziri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelekezo yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:**Waheshimiwa Wabunge, ipo Kanuni inayomruhusu Spika au Mwenyekiti wa kikao cha Bunge kupotea mwongozo na kutoa ufafanuzi wa kitu chochote ambacho kimeletwa mbele ya meza.

Nakubaliana na mwongozo alioutoa *Chief Whip* na kuwaomba Wabunge watakapozungumza mara zote wakumbuke kumwelekeza Spika na si Mbunge ama mtu yeyote, si lazima awe Waziri ama Mbunge yeyote yule. Naomba kutoa msisitizo wa suala hilo.

Naomba tuendelee Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge ajiandae na Mheshimiwa Ephrahim Madeje, ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia leo hoja ya bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa, hivyo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda niwapongeze wadau wa tumbaku, Waheshimiwa Wabunge leo waliochangia vizuri sekta hii ya zao la tumbaku kwanza Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mheshimiwa Said Juma Nkumba na mwisho Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala hili la tumbaku wenzangu leo wamelizungumzia vizuri sana na mimi pia ni mdau mkubwa wa zao hili leo nisingependa kusema sana kwa sababu wenzangu wamepita katika maeneo yote. Ila tu napenda kusema

kwamba naiomba Serikali iweke utaratibu utakaowezesha mikataba ya wakulima na makampuni haya yanayonunua tumbaku iweze kuangaliwa au isaidiwe na wanasheria wa Halmashauri husika au Serikali ili kuepusha wakulima kubanwa katika maeneo yanayomkandamiza na kumnyima haki ya msingi mkulima ili mikataba hiyo iwe ya haki kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nirudi kwenye mazao ya chakula, kwa mujibu wa takwimu za mwezi Februari, 2006 kutoka katika kilimo Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Namtumbo tunategemea mavuno ya mazao ya chakula mahindi tani 68,133, mpunga tani 24,623, muhogo tani 24,710, maharage tani 3,400 na ulezi tani 1,536.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 82, *paragraph* ya 128 mstari wa 3 ambayo inasema: "Ili kujenga upya akiba ya chakula mwaka 2006/2007 Wizara imepanga kununua jumla ya tani 80,000 za mahindi na mtama. Aidha, tani 30,000 za mahindi zitaagizwa kutoka nchi za nje na hivyo kufanya akiba yote kufikia jumla ya tani 110,000."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dharura hasa ukichukulia maanani maeneo mengi ya nchi yetu yalikumbwa na uhaba wa mvua na hivyo yakakosa chakula, hifadhi hiyo ni kidogo sana, tunaomba Serikali iangalie upya ununuzi kwa ajili ya hifadhi hiyo ya chakula. Hivyo kutokana na hali halisi ya upatikanaji wake katika Mkoa wa Ruvuma tunaiomba Serikali iangalie kwa kina suala la kuiongezea bajeti *SGR* ili iweze kununua kutoka kwa wakulima chakula kwa wingi na vile vile itangaze bei mapema ya kununulia chakula kwani wakulima wanapangiwa bei ya chini kabisa na wanunuzi holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SGR* ikitangaza bei yake mapema basi ndiyo inakuwa kigezo kikubwa cha kupangia bei wanunuzi wengine. Lakini vile vile *SGR* wakati wanapopanga bei watazame pia gharama halisi za mkulima kwani mkulima gharama zake ni kubwa na zimepangwa hivyo, wanapopanga bei yao iangaliwe na mkulima naye aweze kupata maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumkomboa maskini mkulima baada ya kazi nzito ya uzalishaji soko lake lisiwe la kubabaika kwani kuna wababaishaji wanaolazimisha kununua mazao kwa vipimo visivyo halali na kumpunja mkulima, kazi kubwa inayofanywa na Serikali ili kumuinua mkulima apate unafuu lakini nguvu yote inapotea katika uuzaji wa mazao yake, anapunjwa sana mkulima na wababaishaji wa soko hivyo naomba Serikali kwa nia nzuri ilionayo tupaangalie sana hapa kwenye soko na tumnyanyue mkulima naye afaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma una hekta 60,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, napenda kuishukuru Serikali kwa kutuletea miradi ya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Liyuni, Wilaya ya Namtumbo, Nambecha, Lusewa na Mradi wa Msindo uliofadhiliwa na *JFACF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna maeneo makubwa katika mabonde kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kama bonde la Likonde, tunaomba Serikali ipatapo

pesa iendeleze miradi ya Mputa, Mchomolo, Likonde nayo ikamilike, tunaiomba pia ikamilishe ile iliyoanza katika Mabonde ya Nambecha na Kitanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizunguzie pia shamba la *NAFCO* ambalo liko Namtumbo lililokuwa la *NAFCO*. Kesi yetu ya Namtumbo inafafana sana na Mbarali, mwaka jana *PSRC* nayo ilitangaza kuuza shamba hilo ambalo wananchi wa Namtumbo walishiriki kukata miti na kung’oa wakati ule mradi huo ulikuwa ukiendeshwa na Warusi na mradi huo ulipokufa wananchi wale waliendelea kulima katika mashamba yale na wamehamia kabisa ni eneo ambalo wanapatia riziki na chakula chao kutoka katika Vijiji vya Namtumbo, Suluti, Rwinga, Mchomolo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nao wali-*tender* katika shamba lile mwaka jana lakini shamba lile baadaye lilizuiwa lisiuzwe lakini sasa hivi tumesikia tena nalo linauzwa lile shamba lakini wananchi wa Namtumbo wamenituma na wanaiomba Serikali kwamba kwa nini wasipewe wao? Kwa nini Serikali isifanye kama Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ilivyogawa shamba lake la mifugo katika Halmashauri ya Songea Vijijini? Tunaomba na sisi kama inashindikana kuwapa wananchi, waipe Halmashauri na wananchi nao watajisikia kwamba shamba lile ni la kwao ili waendelee kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali ilifikirie hilo kwani wananchi wanategemea sana shamba hilo la Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia katika ukurasa wa 82 miradi ya maendeleo, Ibara ya 129 Waziri alisema Wizara inatekeleza miradi na programu za Taifa kama sehemu ya utekelezaji wa *ASDP,* kiambatanisho namba 6, miradi au programu hizo ni kwanza, mradi wa uwekezaji katika sekta ya kilimo Wilayani, halafu kazi zake ni kutekeleza, kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya katika maeneo ya miradi ya kuandaa mipango ya Wilaya maendeleo ya kilimo inayozingatia mahitaji ya mkulima na uunda timu ya uwezeshaji wa Wilaya na Kata na kuzipatia mafunzo ili kuzijengea uwezo wa kufundisha wakulima kuibua, kuandaa na kutekeleza miradi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiambatisho hiki namba 6 Mkoa wa Ruvuma haupo, mkoa wa Ruvuma kama tunavyofahamu wote ni Mkoa ambao unategemea sana kilimo. Ni Mkoa ambao pia umechangia sana katika adha iliyotupata ya matatizo ya njaa mwaka huu lakini hauko katika mipango hii yote mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itufikirie, tumekosa nini sisi Ruvuma wakati sisi ndiyo wazalishaji wakubwa? Tunaomba mtufikirie kwa hili ili na sisi tuweze kuingia katika mipango hii kwani Halmashauri bila kuwa na mipango mahususi au bila kuwa na taaluma ya kuendeleza miradi ya kilimo hatutatoka hapa au hatutaongeza uzalishaji. Tunaomba sana Mkoa wetu wa Ruvuma nao uweze kuingizwa katika miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama nilivyosema mwanzo huwa nazungumza sana kuhusu suala la tumbaku lakini wadau wenzangu wamezungumza vizuri, leo sina ya kusema ni hayo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu katika hotuba hii nzuri ambayo imewasilishwa na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Kwanza kwa idhini yako naomba nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri ambayo kimsingi ina vitu vyote muhimu na tunachofanya nadhani ni kuongezea ili iweze kutekelezeka vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa nitaongelea mbolea nadhani ni vyema niongelee vile vile kuhusu chakula na hapa kwa idhini yako tena naomba nimpongeze sana Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa kugawa chakula kwenye sehemu zilizokuwa zinatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisema hili kwa sababu mimi nimejifunza vitu vitatu ambavyo vilifanyika wakati huo, kitu cha kwanza ambacho Ofisi ya Waziri Mkuu ilifanya wakishirikiana na Ofisi ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ilikuwa ni kufanya tathmini ya kujua ukubwa wa tatizo, kujua ni kiasi gani njaa ipo sehemu mbalimbali na tathmini hii ilionyesha kaya hadi kaya, ikaonyesha kijiji hadi kijini, ikaonyesha Kata, Wilaya hadi Mkoa na hadi mahitaji ya Kitaifa, kwa hiyo, nadhani kujua tatizo ilikuwa ni suala la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo nawapongeza ni kutafuta chakula baada ya kujua hali halisi ya chakula ilivyo walifanya juhudi za kila aina kutafuta chakula na kikapatikana. *(Makofi)*

La tatu, ambalo linanifanya niwapongeze sana baada ya kupata chakula kazi kubwa ambayo mara nyingi huwa inatushinda ni ya kusambaza kile chakula. Tulipewa taarifa mbalimbali hapa zikaja na hakukuwa na malalamiko ya kwamba chakula hakikufika na kama yalikuwepo basi ni asilimia ndogo karibu 0.001 ambayo ilikuwa ni marekebisho madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuitumia hii kama *challenge* ambayo labda ni kama funzo tungelitumia kwenye tatizo hili la mbolea. Mbolea imelalamikiwa karibu na kila msemaji aliyesimama, mbolea inalalamikiwa karibu na kila Kata hata katika Jimbo langu la Makete kila Kata niliyopita wanalalamika kwamba mbolea haiwafikii, sasa nimekuwa najiuliza kwamba tumeweza kusambaza chakula vizuri kabisa kwa nini tunashindwa kusambaza mbolea ikawafikia wakulima? Swali ambalo nadhani ningeweza kusema kwamba kama ile tathmini ilionyesha kaya hadi kaya, Kijiji, Kata na Wilaya, kwa nini leo kwenye ile tathmini pale walipoandika chakula tuka-*delete,* tukaandika mbolea? Tukatumia hiyo tathmini kusambaza mbolea kwa wananchi sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo una matatizo, naweza nikatoa mfano kwa sasa hivi vibali vinatolewa na viongozi wa Wilaya mfano mmojawapo ni katika Wilaya yangu ya Makete, kibali kilitolewa cha mtu kwenda kuchukua kilo 80 kule Makambako lakini huyo mtu baadaye aliongeza moja mwanzoni ikawa kilo 180, kwa hiyo, alipokwenda Makambako akachukua kilo 180. Cha kwanza hakuipeleka hiyo mbolea Makete akaiuza, lakini cha pili zile kilo 100 alizoziongeza zikafanya mtu mwingine akose mbolea kwa hiyo, hii ni wazi kabisa kwamba ule utaratibu siyo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba kama ingewezekana kwa sababu tuko Dodoma sasa hivi mpaka mwezi Agosti, tarehe 15 kama Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika waandae hiyo *formula* mpya na ikiwezekana hiyo *formula* ije basi hapa kama tulivyokuwa tunaletewa tathmini ya chakula tuipitie na tuona kwamba mbolea inaweza ikawafikia vipi wakulima wetu nchini. Hilo litatusaidia kuwa-*encourage* wananchi ili waweze kuona kwamba Serikali inawajali na mojawapo vile vile wangeweza kuangalia kuzitumia *council* za Wilaya ambazo zinawawakilishi Madiwani wa kila Kata kuona kwamba wangeweza kushiriki katika kugawa hizi mbolea ziweze kuwafikia wananchi. Huo ni mchango wangu kuhusu suala la mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuhusu zao la pareto, hapa pia kwa idhini yako naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa juhudi zake zote anazozifanya kulifufua hili zao la pareto. Kwetu sisi wananchi wa Makete zao la Pareto lilikuwa ndiyo zao kubwa lililokuwa linawaletea uchumi wananchi wa Makete na kufa kwake mimi naainisha kwamba kumekuwa sambamba na umaskini uliopo sasa hivi na hayo matatizo yaliyopo ni kwa sababu ya kukosa zao la biashara. Hata hivyo, ningependa kumnukuu aliyekuwa mgombea wetu wa Chama cha Mapinduzi alipokuja Makete alisema wazi kabisa kwamba hakuna sehemu inayoweza kupata maendeleo bila kuwa na zao la biashara na hivyo kuahidi kulifufua hilo zao. *(Makofi)*

Lakini kutokana na juhudi zote ambazo zinafanywa, nilikuwa naomba kwamba basi Wizara iweke wazi haya mambo, kuna mambo ambayo wananchi wanauliza kwa mfano wanauliza bei, huo mkataba, huyo mtu aliyekuja kuchukua hiki kiwanda atachukua kwa bei gani, hizi pareto na ni kwa muda upi, tunawaambia miaka mitano, je, baada ya miaka mitano itakuwaje? Hilo zao litakufa tena au vipi? Je, hizi mbegu tulizoambiwa ambazo zina sumu nzuri 500 kwa hekta moja je, watazipata wapi wananchi? Kwa hiyo, nadhani hapa suala muhimu vile vile ni kutoa taarifa sahihi kwa wananchi, *information* ziweze kusambaa ili ituwezeshe sisi Wabunge kulisemea kwa wananchi na kuwashawishi waweze kurudi kulima lile zao kwa sababu kimsingi walikuwa wameshakata tamaa na walikaa na yale mazao kwa kuda mrefu hayakununuliwa kwa hiyo, nadhani siyo kitu rahisi leo hii ukaenda kumwambia mkulima aanze kulima pareto wakati walishawahi kukaa na hiyo pareto kwa muda wa miaka miwili au mitatu ndani, bila kuuzika.

Kwa hiyo, naomba Serikali itamke rasmi ili wananchi wajue soko likoje na lina muda kiasi gani na bei zipi na hizi mbegu zinapatikana wapi ili tuweze kuisadia vile vile kuwaelimisha wananchi waweze kulima hili zao la pareto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa tatu uko kwenye vipimo vya mazao. Nalazimika kusema hili kwa sababu tunasema tuna matatizo ya usafiri, barabara mbovu, kwa hiyo, walanguzi wanakwenda kwenye Wilaya, Vijiji, Kata na kujipangia bei zao ili waweze kuchukua yale mazao. Mfano mdogo ni zao la viazi ambalo linastawi sana katika Mkoa wa Iringa na hususan Makete, Mkoa wa Mbeya, Arusha na Mikoa mingine, kama ukipita leo barabarani katika vijiji vya Makete utakuta magunia, gunia moja limefungwa linaungana na lingine la pili ambalo wanaita lumbesa.

Sasa taratibu zipo nafahamu, sheria ipo iliyowekwa kwamba vipimo viwe vipi kwa hiyo, nadhani tatizo hapa ni usimamizi, watu wamekuwa wakisema kwamba barabara ni mbovu ndiyo maana hivyo vita vinachangia lakini hata ukitoka Mbeya ukiwa unaelekea Tukuyu yale maeneo ya Isyonje, Simambwe unakuta kuna magunia yameshonwa mara mbili yamepelekwa karibu na barabara ya lami kabisa kumpelekea huyu mfanyabiashara ili aweze kuchukua hayo mazao. Kwa hiyo, nadhani juhudi za makusudi zinatakiwa Serikali izichukue za kuhakikisha kwamba inawalinda wananchi hasa kwa kuzingatia kwamba hawaelewi hizi taratibu, hilo ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuongezea katika hili niende katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 9 kuna suala la hali ya kilimo. Mimi nadhani imefika wakati tujiwekee mikakati na tujiwekee malengo kama leo hii mwaka 2006 karibu miaka 44 toka tumepata Uhuru tunasema 70% ya wakulima wanatumia jembe la mkono ni kama tunajishtaki kwa sababu hiyo miaka sasa tumepunguza kiasi gani? Ni kiasi gani tumeongeza utumiaji wa matrekta? Kama leo hii ni 10% kwa miaka hii 44 ni kiasi gani tumewezesha utumiaji wa majembe ya kukokotwa kama leo hii ni 20%? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikua nadhani ili tuweze kufanikiwa huko mbele, basi Waziri anayehusika na wataalam wake wangeweza angalau kutukadiria kusema katika kipindi hiki cha miaka mitano tunategemea kuinua utumiaji wa matrekta kutoka 10% kwenda asilimia kadhaa na tunategemea kuinua utumiaji wa jembe la kukokotwa kutoka 20% kwenda asilimia kadhaa na kupunguza matumizi ya jembe la mkono kutoka 70% kwenda asilimia kadhaa nadhani hiyo ingekuwa ni mkakati mzuri ambao nadhani hata mwaka 2010 tunaweza tukajipima vizuri kwamba tumetekeleza vizuri ilani yetu ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba tena nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na nasema naunga hoja mkono hotuba hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo ningeomba nitoe pongezi kwa niaba ya wananchi wa Dodoma Mjini kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Luteni Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na hapo hapo nisiwasahau Wabunge wenzetu ambao pia wamechaguliwa katika Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kwa kuipongeza Wizara hii kwa hotuba nzuri ambayo imegusia maeneo muhimu na pia imeleta sura mpya na matarajio mapya katika kilimo na katika nchi yetu. Matarajio yetu pia ni kwamba yale yaliyoandikwa katika hotuba hii kwa kweli wanaohusika wafanye kila wanaloweza ili yaliyolengwa yaweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia katika kuchangia hoja ningeomba nianze na tatizo la njaa. Naomba radhi kwa kuanza na matatizo kwanza ingebidi nianze na masuala ya maendeleo lakini hili suala ni suala zito kidogo na linawagusa sana wananchi wa Dodoma Mjini ambao ninawawakilisha na sitakuwa nimewatendea haki kama sikuileta mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo inashughulikia suala la misaada wa chakula cha njaa kwa watu wa Jimbo la Dodoma Mjini na pia tunaendelea kuishukuru Serikali kwa sababu tayari imeshapata taarifa ya kubaini kwamba Jimbo letu bado litaendelea kuwa na tatizo la njaa katika mwaka huu ambao tumeuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo ambalo tumekuwa nalo katika Jimbo hili ambalo linaitwa Dodoma Mjini ni kwamba mgao wa chakula kwenye vijiji ambavyo viko katika Jimbo hili kwa sababu Jimbo hili siyo Dodoma Mjini tu peke yake kuna vijiji ambavyo vinalizunguka Jimbo hili kwa kweli umekuwa ni mdogo sana wastani wake umekuwa kama tani 200 kwa miezi miwili hivi nimeshapata migao minne na mimi ninavyoliona hili tatizo linatokana na sababu mbili kuu. Nia ya Serikali ni nzuri kwamba kweli wananchi wasaidiwe katika hili tatizo lakini matokeo yamekuwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kwanza ambalo ninaliona mimi lile la mtazamo wa sera ya Serikali ambayo ni sahihi ni kwamba wale watu wa mijini kwa kweli wasihusike na mgao wa chakula cha bei nafuu hilo tunakubaliana nalo kabisa. Sasa tatizo tulilonalo hapa Dodoma Mjini ni kwamba Dodoma Mjini ina vijiji 40 vinavyozunguka huu mji na hivi vijiji vinakaliwa na wakulima, wakulima hawa mvua zikishagoma na mazao yakishagoma kwa kweli wanakuwa hawana kimbilio lolote lingine, hawana njia yoyote ya kujihami isipokuwa hutarajia msaada wa Serikali, na

kama mnavyojua sasa hivi huu ni mwaka wa pili vijiji hivi havijaweza kupata mazao au mavuno ambayo yanaweza kutosheleza kuondoa hilo tatizo la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili ninaloliona ni lile la takwimu sahihi, ninavyoelewa mimi ni kwamba takwimu zinatayarishwa au zinachukuliwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika sina uhakika kuhusu *methods* gani wanatumia lakini kwa sababu ni timu ambazo zinatoka huko Makao Makuu, mimi nina uhakika watakuwa wanatumia *sampling methods* kwa hiyo, siyo rahisi wao kwenda katika kila kijiji au katika kila sehemu inayohusika wakapata takwimu ambazo ziko sahihi. Nadhani wanaweza kuwa wanashirikiana na watu wetu waliopo katika Manispaa lakini kwa bahati mbaya katika takwimu ambazo zilitumika katika kuamua kiasi gani cha mgao wa Dodoma Mjini kwa maana ya hivyo vijiji kwa kweli ulikuwa hautoshelezi. *(Makofi)*

Sasa tatizo hili lina athari zake, athari kubwa ni kwa wale wananchi wenyewe kwa sababu afya zao tunashukuru Mungu kwamba hakuna ambaye ameshafariki sasa hivi kutokana na ukosefu wa chakula, lakini kwa kweli walio wengi wana hali mbaya kiafya.

Pia hata kisaikolojia kwa sababu hawa wananchi ambao wako katika vijiji hivi wanapakana na wenzao ambao wako Dodoma Vijijini, sasa ni eneo hilo hilo upande mmoja wenzao wanapata msaada ambao unaelewaka na wao wenyewe wanapata kidogo kwa hiyo, hili nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kwamba lawama kweli kwao Serikali kwa wale wanaohusika na ugawaji zimekuwa ni kubwa mno. Mara nyingi chakula hiki kikipelekwa kwenye vijiji tunaonea huruma wale wanaohusika na ugawaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyojua viongozi wa Serikali huko vijijini wanatokana na sisi. Sasa hili sitaki kulisemea lakini nadhani linaweza likatuletea balaa ambayo hatustahili. Serikali imeamua kwamba itatoa misaada ili watu wasipate shida, lakini sasa hiyo misaada isije ikaleta tena sura mbaya kwamba Serikali haijafanya chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu ni kwamba Wizara ipitie kwa uangalifu sana takwimu ambazo zinatumika. Hapa nilipo nina takwimu ambazo nawashukuru watu wa Manispaa wamezitoa. Nadhani kwa sababu hili tatizo linawagusa sana, wamekuwa wakilisimamia kwa karibu sana.

Kutokana na takwimu zao ni kwamba watu ambao hawana uwezo hununua chakula kwa miezi kumi ijayo ni 54,407 ambao mahitaji yao ya chakula kwa miwezi kumi yaani kuanzia Julai hadi Aprili, 2007 ambapo mvua zitakuwa zimenyesha *inshallah* ni tani 6,412. Wale ambao wana uwezo wa kununua chakula kwa bei nafuu ni 1,013,764 na mahitaji yao kwa kipindi hicho hicho ni kama tani 13,678. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara isikie kilio chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kuja kwenye suala la kilimo cha chakula katika jimbo langu na kwa Dodoma kwa ujumla. Kama inavyojulikana kwa kweli nchi

yetu ni ya ukame, ni *the semi arid area.* Ile miaka ambayo mvua inakuwa siyo nzuri kwa uhakika lazima njaa inakuwepo. Lakini pamoja na hayo watu wa Dodoma kwa kweli wana jitihada sana ya kulima mbali mara nyingine huwa wanakosea wanalima mazao ambayo hayastahilimi ukame.

Hii mara nyingi huwa inatokea kama kukiwa mfululizo wa miaka miwili, mitatu ya mvua nzuri. Sasa sisi viongozi wa Dodoma tukiongozwa na Mkuu wetu wa Mkoa tumedhamiria kwamba kwa mwaka huu au wa msimu huu ujao tutafanya kampeni kubwa sana ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanalima mazao ambayo yanastahimili ukame. Mazao hayo ni mtama na uwele. *(Makofi)*

Lakini katika hili tungeomba wenzetu wa Wizarani nao pia watusaidie tuwapatie motisha hawa wakulima. Motisha kwa maana gani? Mahindi hayana shuruba kubwa sana katika kuyatayarisha ili upate unga kwa sababu teknolojia inaweza ikatumika. Mashine za kukobolea zipo na mashine za kusagisha zipo.

Lakini mtama na uwele bado hiyo kazi lazima ifanywe kwa mkono. Hilo nalo labda wenzetu watusaidie wafanye utafiti, najua sio kitu ambacho kinaweza kikafanyika mara moja lakini watubunie mashine za kukoboa na kusagisha mtama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii suala la umwagiliaji maji ili kuleta ufanisi zaidi katika kilimo limezungumziwa. Nafurahi sana na tunashukuru na tuna imani kwamba na sisi Dodoma hatukusahauliwa katika mgao wa hizo fedha za kuleta mabwawa na shughuli nyingine zozote za umwagiliaji.

Kwa hapa Dodoma mabwawa tuliyonayo ni machache. Hapa nazungumzia Dodoma Mjini tunayo mabwawa ya Hombolo na Mpunguzi. Mabwawa madogo lakini yamekuwa yakitumika na vijana wetu katika umwagiliaji mdogo mdogo wa mbolea, umwagiliaji wa mboga mboga hasa nyanya na vitu vingine hivyo.

Sasa ni matumaini yetu kwamba mabwawa mapya yatajengwa na haya ambayo ni ya zamani kwa kweli kwanza yaliyo mengi yameshakuwa *silted,* mchanga umeshajaa mle ndani kwa hiyo, maji yanayoingia humo ni machache.

Kwa hiyo, tunaomba sana katika mkakati huo wa kuleta kilimo cha umwagiliaji Wizara itutupie macho ili angalau na sisi tuweze kupiga hatua.

Lakini pia kwa Dodoma Mjini wakati *CDA* inafanya mipango yake kulikuwa kuna eneo ambalo linaitwa *green belt* lengo ilikuwa ni kwamba hawa watu wa Miuji, Vyeyula na Msalato walipewa *plot* kubwa sana nadhani hekta moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ilikuwa ni kwamba umwagiliaji ufanyike kwa ajili ya *market gardening,* mboga mboga na vitu mbalimbali. Matokeo yake ni kwamba maji sasa hivi Dodoma Mjini ni bei ghali sana kwa hiyo umwagiliaji huu hauwezi kufanyika. Tunaiomba Serikali ifanye mpango maalum ama kuchimba visima,

kuwasaidia hawa watu ambao wamepewa maeneo makubwa kwa malengo ya kuleta uzalishaji lakini hawawezi kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele imeshalia sasa mimi ningeomba kabla sijagongewa kengele ya pili nizungumzie zao la mizabibu. Zao la mizabibu kama vile limekufa lakini sababu kubwa ni ukosefu wa soko. *Winery* mpya ilifunguliwa Hombolo lakini mpaka sasa hivi haijaweza kufanya kazi vizuri labda Waziri anaweza akatuelezea tatizo ni nini lakini kwa kweli zao hili linaweza kuwa mkombozi wa watu wa Dodoma lakini limekufa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Ephraim Madeje, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijaahirisha kikao cha leo nimepokea vi-*note* hapa vingi vikihoji Mheshimiwa Mwenyekiti wewe kanuni hiyo uliyoisema unaifahamu, kwa nini hutaki kuieleza hapa ndani ya Bunge kwa faida yetu sisi wengine wote?

Naomba Waheshimiwa Wabunge niwaambie kwamba kwa kuzingatia ule muda ilibidi tuendelee, lakini nilitaka kuisoma baada ya kumaliza shughuli zetu tusikatishe muda.

Kanuni hiyo ni kanuni ya 49 na inahusu Kanuni za Majadiliano na kanuni hiyo 49(1) inasema: “Mbunge akitaka kusema aweza ama kumpelekea Spika ombi la maandishi au kusimama kimya mahali pale, lakini hataanza kuzungumza mpaka Spika amwite ama kwa jina au kwa wadhifa wake na kumruhusu kusema na hapo ndipo ataanza kuzungumza akielekeza maneno yake kwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge akimaliza kutoa maelezo yake atakaa kwenye nafasi yake na hapo Spika atamwita Mbunge mwingine aliyepeleka ombi la maandishi ama la kuzungumza ili aendelee.” Inaendelea.

Lakini kanuni hiyo hiyo ya 49 ya majadiliano namba (8) inaendelea kusisitiza inasema kwamba: “Katika mjadala wowote Mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya nyadhifa zao na sio majina yao.” Vile vile inaendelea kusema: “Wabunge wengine wote watatajwa kwa kutumia neno Mheshimiwa kabla ya jina la Mbunge huyo.”

Waheshimiwa Wabunge, lakini tunaona kanuni ya 53 (c) ndiyo inasisitiza kwamba hairuhusiwi Mbunge kukatisha kati ya Spika na Mbunge anayezungumza. Hiyo ni kuashiria kwamba anayeendesha kikao ni Spika na sio Waziri wala Mbunge yeyote atakayetajwa kwa jina kwa mujibu wa kanuni zilizopo ndani ya kanuni yetu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba kwa kweli tuzingatie taratibu hizo. Kama tutaendelea kuwa tunazisoma tu kila mara katikati tunapunguza muda wa kuchangia hoja zetu kwenye Hoja za Serikali zinazoletwa. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo ninaahirisha Kikao hiki cha Bunge kwa siku ya leo na tutakutaka tena kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu wa Bunge. *(Makofi)*

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 6 Juni, 2006 saa tatu asubuhi)*